Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 24 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe.Zuberi Ali Maulid ) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 94

**Mgawanyo wa Magari katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli na Halmashauri ya Wilaya ya Longido**

**MHE. OMAR SHABANI KWAANGW' (K.n.y. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Kwa kuwa , Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya mpya na kwamba wakati wa kugawa Wilaya ya Monduli na kuzaa Wilaya mpya ya Longido kulikuwa na magari chakavu ambayo yameendelea kutumia fedha za Halmashauri ya Longido ya mara kwa mara.

(a) Je, Serikali itatoa lini magari kwa ajili ya Halmashauri ya Longido ambayo haina magari ya kufanyia kazi?

(b) Je, kwa nini Serikali haikutoa kipaumbele kwa Halmashauri hizo mpya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer , Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuzingatia kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Longido ni mpya na ina uhaba wa vitendea kazi, Serikali ilitoa fedha kwa kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa katika Halmashauri na maombi maalumu *(special request)* ili kununua magari mapya yatakayosaidia katika uendeshaji na utoaji wa huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Fedha hizo zilitolewa kama ruzuku katika mwaka wa fedha 2007/2008 na tayari magari yafutayo yalishanunuliwa kupitia Wizara ya Miundombinu:-

.Gari Namba STK 5340 aina ya *Toyota Landcruiser;*

.Gari Namba STK 5462 aina ya *Toyota Landcruiser;*

.Gari Namba STK 4987 aina ya *Toyota Hilux double Cabin;*
na
.Gari Namba STK 5408 aina ya *Toyota Landcruiser* kwa ajili ya Mkurugenzi Mtendaji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti , magari yote hayo niliyoyataja yamenunuliwa kutokana na fedha za ruzuku toka Serikali Kuu kupitia Bajeti za miradi na maombi maalum katika mwaka wa fedha 2007-2008 . Kutolewa kwa fedha hizi ambazo zimewezesha kununuliwa kwa magari hayo manne ni dhahiri kunaonyesha jinsi Serikali ilivyotoa kipaumbele cha vitendea kazi katika Halmashauri Wilaya ya Longido

**MWENYEKITI**: Ahsante, swali la nyongeza Mheshimiwa Kwaangw'.

**MHE.OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya Halmashauri ya mji wa Babati ambayo nayo ni mpya yanafanana na Wilaya ya Longido ambayo ni mpya kutokana na kukosekana kwa magari, au vitendea kazi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba Halmashauri ya mji wa Babati nayo ifikiriwe kupatiwa maombi maalum kwa sababu haina vitendea kazi na hasa magari.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti , kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Kwaang' kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nikubaliane na Mheshimiwa Kwaang' kwamba Halmashauri hizi na Wilaya hizi mpya ambazo zimeanzishwa kwa kweli kwa kuanzia zimeonekana kwamba zina hali ya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magari ambayo wamechukua kutoka kwenye Halmashauri za zamani mengine yalikuwa ni mabovu na yanakuwa ni mzigo hata kama unayatengeneza yanaharibika mara kwa mara. Kwa hiyo, nina kubaliana naye na ninapenda ku-*declear interest* hapa kwamba na mimi ninayo Wilaya mpya Wilaya ya Siha iliniweze kueleweka vizuri ninavyozungumza hapa kwa hiyo nina maslahi na jambo hili. *(Makofi)*

Ninachoweza kusema hapa ni kwamba tunachofanya ni kwamba hizi Halmashauri na Wilaya mpya zimepewa kipaumbele. Sasa hivi Serikali imeamua kwamba hatutaagiza magari mengine mapya kwa sababu tunataka kuelekeza nguvu zetu kwnye suala la kilimo, lakini tumeiomba Serikali ikubali kwa Halmashauri hizi mpya ziweze kupata kibali maalum kwa ajili ya kununulia magari na vitendea kazi vingine kwa ajili shughuli zake.

Kwa hiyo, pia Halmashauri ya Wilaya ya Babati kama anavyosema Mheshimiwa Kwaang' itakuwa ni katika zile Halmashauri ambazo tutajaribu ku-*consider*.

**MWENYEKITI:** Mheshimwa Telele kwa swali la nyongeza.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali hivi karibuni imeanzisha utaratibu wa kununua magari ya Halmashauri zote nchini kupitia Wizara ya Miundombinu na kwasababau utaratibu ule Wizara inachukua muda marefu, ina – *accumulate* maombi yale alafu na baadaye ndio inunue magari lakini wakati huohuo bei ya magari inaweza ikapanda.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kutizama upya utaratibu huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Telele, Mbunge wetu wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Kwanza nieleze kwa nini magari yote yalionekana kwamba yanunuliwe katika *pool* moja, na msimamo wa Serikali ni kwamba magari yote yanunuliwe kupita Miundombinu. Ilionekana kwamba ukinunua magari yote kwa pamoja katika utaratibu huu maana yake ni kwamba hata *discount* unayoipata pale yaani unafuu wa bei unakuwa ni mkubwa zaidi kuliko kila mtu kujinunulia yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tumepokea malalamiko anayozungumza Mheshimiwa Telele kwamba kumekuwa na matatizo kwa kwa sababu kumekuwa na ucheleweshaji. Kwa hiyo, tunajaribu kuangalia tena upya sasa utaratibu mzuri ambao unawaweza kusaidia katika mpango huu lakini kwa sasa msimamo uliopo wa Serikali ni huo, Lakini jambo hili ni jambo ambalo limetufikia kwa hiyo tutalitafakari na kwa kweli tutaona kwamba ni tatizo basi tutaishauri Serikali ili iweze kutekeleza kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Na. 95

**Tanzania Kujifunza Kutoka Botswana juu ya Kupambana na Rushwa**

**MHE. LUCAS LUMAMBO SELELII (K.n.y. JOHN P. LWANJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ripoti ya Mwongozo wa wazi wa Rushwa wa Kimataifa ya mwaka 2007-2008 ilizitaja nchi za Kiafriaka kwamaba zinaongoza kwa Rushwa Duniani;na kwa kuwa ripoti hiyo ilitaja Botswana kama ni nchi pekee ya Afrika iliyoko kwenye nchi 50 zenye kiwango kidogo cha rushwa duniani inashika nafasi ya 27:-

(a) Je, ni kwa njia gani Botswana imeweza kupambana na rushwa na kufanikiwa kuwekwa katika kundi la nchi 50 Duniani zenye kiwango kidogo cha rushwa?

(b) Je, kawa nini Tanzania imeshindwa kujifunza mbinu na mikakati ya kuzuia na kupamabana na rushwa toka Botswana, ambayo ni rafiki wa Tanzania toka kupata uhuru?

(c) Je, ni wataalamu wa ngapi wa TAKUKURU wamepelekwa Botswana kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi na mrefu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA )** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi,naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuwa Botswana ni nchi mojawapo katika bara la Afrika iliyotajwa na Taasisi ya *Transparency International* kuwa miongoni mwa nchi 50 duniani zenye kiwango kidogo cha rushwa. Kwa mujibu wa ripoti ya *Transparency International* ya mwaka 2007, Nchi ya Botswana imetajwa kushika nafasi ya 38. Aidha nchi ya Afrika ya Kusini imetajwa kushika nafasi ya 43. Katika taarifa hiyo Tanzania imetajwa kushika nafasi ya 94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kila nchi duniani ina mikakati na njia zake ambazo hutumia katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Hata hivyo, nchi za Botsawana na Tanzania ni wanachama wa *SADC,* upo ushirikiano wa karibu katika eneo la kupambana na rushwa hivyo njia na mikakati katika nchi hizo hunashabihiana.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Tanzania na Botswana ni nchi rafiki na zimekuwa na ushirikiano wa karibu katika masuala mbalimbali likiwemo la kuzuia na kupambana na rushwa . Hivyo sio kweli kwamba Tanzania imeshindwa kujifunza mbinu na mikakati mipya ya kuzuia na kupambana na rushwa kutoka Botswana.

Aidha ni mategemeo yetu ni kwamba ushirikiano wetu katika sekta hii utaendelea kukua na rushwa itaendelea kupungua na ikiwezekana kutokomezwa kabisa nchini. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya wataalam wa TAKUKURU waliopelekwa nchini Botswana kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi ni maafisa 4. Hata hivyo, Tanzania imekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya mafunzo ya vita dhidi ya rushwa katika nchi za Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Forum Against Corruption)* ambayo Botswana pia ni Mwanachama ambapo mafunzo mbalimbali ya kitaalam katika katika eneo la kupambana na rushwa yamekuwa yakitolewa. Kwa sasa Botswana wameleta maombi kuja nchini Tanzania kujifunza mbinu na mikakati inayotumiwa na Serikali ya Tanzania katika kuzuia na kupambana na rushwa. Kutokana na urafiki na mahusiano mazuri baina ya nchi hizi mbili, Tanzania imekubali kutoa mafunzo kwa maafisa 50 wa Botswana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Idara hii ya TAKUKURU mara nyingi inapitia na kuzungumzia sana rushwa ndogondogo na kuacha rushwa kubwa ambazo hasa zinatokana na mikataba mibaya inayoingiwa na wataalam wetu. Je, Ofisi ya Rais Idara ya utawala bora iko tayari kuwapeleka maofisa wa TAKUKURU na maofisa wa Serikali kujifunza namna nzuri ya kuandika mikataba ambayo inaonekana kuna mianya mikubwa sana ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika majibu yake Mheshimiwa Waziri ametaja Tanzania ni nchi ya 94 katika mlolongo kimataifa. Na wenzetu wa Botswana na Afrika ya Kusini angalau wako chini ya nchi ya 50.

Je, ni mikakati gani iliyopangwa na Serikali, kuhakikisha kiwango chetu cha rushwa kinashuka ili kupandisha nchi yetu Tanzania angalau iwe chini ya nchi 20 au 30 katika mlolongo wa mstari wa rushwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selelii, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikubaliani na Mheshimiwa Selelii kuhusu kwamba TAKUKURU inashughulikia rushwa ndogondogo tu. TAKUKURU inashughulikia rushwa ndogondogo pamoja na rushwa kubwa na kama anavyojua kuna kesi nyingi ambazo TAKUKURU inaendelea kuziendesha katika mahakama zetu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika swali lake ameuliza kuhusu Serikali kupeleka maafisa wetu kujifunza jinsi ya kuandaa mikataba, hili linafanyika na ilikwishaelezwa katika Bunge hili kwamba tayari utaratibu unafanywa kuhakikisha

maafisa wetu wa Serikali ikiwemo wale katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wanapata *skills* bora zaidi za kuweza kuandaa mikataba.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selelii anataka kujua ni mikakati gani. Serikali kwa kupitia TAKUKURU ina tekeleza mkakati wa kupambana na rushwa nchini ,mkakati wa kitaifa unaitwa *NASAF* 2 ambao kwa kweli unafanya kazi kubwa unaendesha *seminars* , mkakati huu ambao kwa kweli unafanya kazi kubwa unaendesha *seminars* , kuhakikisha kwamba katika kila idara za Serikali na katika kila Wizara kuna *intergrit committees* ambazo zinashughulikia kuangalia kwamba kuna uadilifu katika utekelezaji wa kazi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mikakati hii iliyowekwa na Serikali ni pamoja na kuwepo na sheria hii mpya ya rushwa 2007 ambayo Sheria ya zamani ilikuwa na makosa manne tu. Na katika yale makosa manne makosa ya mikataba yalikuwa hayajitokezi, lakini sasa sheria mpya ya kuzuia rushwa ina makosa ishirini na nne na hivyo katika sheria hiyo inajitokeza makosa mbalimbali ambayo yanahusiana na masuala ya rushwa .

Mheshiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mikakati ipo na ndio maana hata nchi ya Botswana wanakuja kwetu kujifunza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mzindakaya, nimekuona kwa swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Inavyoonekana ni kuwa wananchi wanatangaziwa kesi nyingi sana zinazokamatwa lakini matokeo hayatangazwi kuna nini?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu swali lake Mheshimiwa Mzindakaya kama ifuatavyo:-

Kesi ni kweli ni nyingi zinatangazwa lakini kama ulivyo utaratibu wa kesi za jinai siyo utaratibu kuanza kuandika kesi za rushwa. Maana yake tuna kesi nyingi za rushwa zinazoendelea zaidi ya mia tatu katika mahakama. Kwa hiyo, haitakuwa rahisi kuwa tunatangaza kesi ya fulani amehukumiwa hivi au vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kukujulisha tu ni kwamba kesi hizi zinaweza zikafaamishwa kwamba watu wamekamatwa . Lakini ni lazima zifuate utaratibu wa kisheria . Lazima upatikane ushahidi wa kutosha na baada ya kupatikana ushahidi wa kutosha ndipo kesi hizi zinahukumiwa kwasababu tunaendesha utaratibu wa sheria ya Hymuiya ya Madola (*Commonwealth Legal System)* ambayo ni lazima mtuhumiwa naye apate haki ya kujijitetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kesi nyingi ambazo zimehukumiwa. Wakati mwingine wengine wamechuliwa hatua za kinidhamu na wengine wameshushwa vyeo, zile zingine ambazo ushahidi haukutosha. Lakini kwa ushahidi uliotosha

wamehukumiwa inavyopaswa lakini mahakama haina utaratibu wa kutangaza hukumu zake.

Na. 96

**Wawekezaji Hewa Katika Ranchi ya Kitengule**

**MHE. GOSBERT BEGUMISA BLANDES** aliuza:-

Kwa kuwa ranchi ya kitengule iligawiwa kwa wawekezaji mbalimbali kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe ; na kwa kuwa baadhi ya wawekezaji hao wameshindwa kutumia ranchi kwa malengo yaliyokusudiwa:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa baadhi ya wawekezaji wamehodhi ardhi bila kutumia?

(b) Je, Serikali inaweza kutaja majina ya hao wawekezaji hewa?

(c) Je, ni lini Serikali itanyang'anya ardhi wawekezaji hao na kuwapatia ardhi wafugaji wa Karagwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Bagumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wizara yangu inalitambua tatizo la baadhi ya wamiliki wa maeneo ya ranchi kuchelewa kuwekeza katika vitalu walivyopewa kutokana na sababu mbalimbali. Umilikishaji wa ranchi ndogo katika maeneo ya *ranch* ya Taifa *(NARCO)*, ikiwemo ranchi ya Kitengule ulitokana na uamuzi wa Serikali kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri Na 2 wa mwaka 2002. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa waraka huo Serikali iliamua kugawa baadhi ya maeneo ya Ranchi za Taifa katika vitalu vya wastani wa hekta 2,000 hadi 4,000 na kuvimilikisha *(sub –lease )* kwa wawekezaji binafsi Watanzania wenye nia na uwezo wa kuviendeleza kwa shughuli za ufugaji wa kisasa na kibiashara. Kulingana na utaratibu uliowekwa na Serikali wawekezaji wanamilikishwa maeneo hayo kwa kupewa Hati Miliki ya matumizi *(Sub-Lease)* na ardhi inabakia mali ya *NARCO.*

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ranchi ya Kitengule wawekezaji waliomilikishwa ranchi kwa utaratibu huo ni tisa (9) , ikiwemo Kampuni ya Sukari ya Kagera yenye eneo la hecta 30, 688 lilitolewa kwa ajili ya kilimo cha miwa na ufugaji. Lengo la kampuni ni kuongeza uzalishaji wa sukari nchini na kutumia mabaki ya mazao ya sukari *(by product)*

ili kunenepesha mifugo. Tumeambiwa kampuni imekwisha wekeza ng'ombe 370, kukarabati baadhi ya majengo na kusafisha sehemu ya shamba.

Kwa upande wa vitalu, uwekezaji umefanyika katika vitalu saba (7) kati ya vinane (8) na kuna kitalu kimoja cha *MCI WORLD WIDE LIMITED* ambacho mwekezaji wake bado hajaanza kuwekeza. Wawekezaji katika vitalu saba ni pamoja na *Kiteto Agro Business Ltd.* Ambaye anadai ana ng'ombe 719, *Abakundaine Trustee* anayesema ana ng'ombe1,703, *Mtebu Investment Co.Ltd.* amedai ana ng'ombe 553, *Charles Burchard Lwa butondogoro* anayedai ana ng'ombe na mbuzi 109, *Edivedius Ritta Kassano* anayedai ana ng'ombe 262, Laurian Kasenene Rubega yeye anasema ana ng'ombe 398 na mbuzi 216, mwisho ni Bungengele *Farm* anayesema ana ng'ombe 210.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua ya kuwapa notisi ya kunyang'anya vitalu hivyo wamiliki 94 ambao hawajawekeza na wale ambao uwekezaji wao sio wa kuridhisha. Notisi hiyo ilikuwa kwa miezi sita na muda wake umekwisha. Kwa sasa, Wizara yangu inafanya uhakiki ili kuwanyag'anya wawekezaji ambao hawajatekeleza agizo hilo.

Baada ya uhakiki huo maeneo hayo yatatangazwa upya na yatatolewa kwa wawekezaji wengine makini, wakiwemo wafugaji wa Karagwe kulingana na taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

**MHE.GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Ingawa siku zote anakosea jina langu anaita Blendes wakati mimi naitwa Blandes.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba kampuni ya *Kagera Sugar* imepewa eneo la *hector* 30,688 eneo ambalo ni kubwa. Lakini *Kagera Sugar* mpaka sasa hivi wameweza kuweka mifugo ipatayo mia tatu na sabini , kiwango ambacho ni kidogo sana cha ng'ombe katika eneo la *hector* 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu ni je, kwa kuwa kampuni ya *Kagera Sugar* imeshindwa kutumia eneo hili kwa makusudi yaliyokusudiwa. Je, ni lini Serikali itawanyag'anya eneo hili na kuwapatia wafugaji wa jimbo la Karagwe. *( Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Swali la pili baada ya *ranch* ya Kitengule kugawiwa kwa wawekezaji wadogowadogo pamejitokeza mgogoro wa mpaka wa ardhi kati ya wananchi wa kijiji cha Katanda, Kibwera na Mshabaiguru Kata ya Kianga hali ambayo inaelekea kuvunjika kwa amani. Na kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikiitaka Serikali iende pale kutatua mgogoro huo na hawafiki. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kutatua mgogoro huo. Nakushukuru Mwenyekiti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kumpongeza kwa namna anavyotuuliza maswali mengi tunapokuja hapa Bungeni kuhusu mifugo. Pia inaonekana kuwa anafuatilia matatizo ya wafugaji wake na yeye ni mfugaji. Kwa hiyo nampongeza sana. Kuhusu *Kagera Sugar* kufuatana na uamuzi wa Baraza la Mawaziri ulitolewa December, 2004 walitoa *hector* 30,688 hili eneo lilitolewa kwa ajili ya ufugaji pamoja na kupanua kilimo cha miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti , hadi sasa kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi wanazo ng’ombe 370 katika hili shamba, na wameanza kufyeka na kukarabati sehemu zingine.

Kufuatana na utaratibu uliowekwa na Serikali tunayo masharti kumi na tisa mtu anapopewa kurithi shamba kama *Kagera Sugar* inavyosema sasa kama tutakuta kwamba tutakapokwenda kuhakiki kama tutakuta sehemu kubwa ya shamba hili hajalitumia vizuri basi hatutasita kulichukua sehemu iliyobaki na kuwagawia watu wengine *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba kwa sasa hivi kumekuwa na maongezi kati ya vijiji vilivyopo na *Kagera Sugar*. Na inaonekana kwamba *Kagera Sugar* yuko tayari kutoa *hector* 2,000 kwa ajili ya wafugaji waliopo na hata wale wengine ambao wanazunguka lile shamba tayari mazungumzo yamefanyika na tayari na wako tayari kuwapatia wana vijiji sehemu fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunangojea hayo yakitimilika ili tuweze kuwasaidia Wananchi wa huko. Lakini sehemu ya pili ni kweli kwamba kuna migogoro na ninashukuru kwamba Wizara yangu imekuwa ikiyashughulikia pamoja na uongozi wa Mkoa. Lakini inaonekana kwamba hivi karibuni wamefikia makubaliano kwamba Wananchi watapatiwa eneo na *Kagera Sugar* imekubali na wale wawekezaji.

Mheshiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kwamba haya yanatatuliwa namwahidi Mheshimiwa Blandes kwamba Wizara yangu tutalifuatilia hili suala. Tutapanga na Mheshimiwa Waziri kama itabidi niende, nitaenda na kama Mheshimiwa Waziri akinituma nitaenda na yeye mwenyewe akipenda tutaenda. Lakini nitalifuatilia hili jambo kwa karibu. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Blandes kuwa nitalifuatilia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ndugai, nimekuona kwa sawali la nyongeza.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali moja la dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika zoezi la kugawanya ranchi za Taifa ranchi ya Kongwa iliamriwa na Serikali kwamba yenyewe isigawanywe ibakie ilivyo. *(Makofi)*

Na ranchi hii imekuwepo kwa zaidi ya miaka sitini katika miaka hiyo sitini na zaidi ambayo ranchi hii imekuwepo wananchi wanaozunguka ranchi ya Kongwa hawajawahi kufaidika na *ranch* hii kwa kujengewa angalau darasa moja la shule ya chekechea.

Mheshimiwa Spika, sasa je, kwa ahadi zile amabazo zilitolewa na Serikali kwamba Wananchi watafaidika na hawafaidi. Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kuwa sasa iko haja ya kuigawanya ranchi Kongwa kama zilivyogawanywa ranchi nyingine nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na uvuvi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Job Ndungai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumewahi kutembelea ranchi ya kongwa ambapo tulienda na Mheshimiwa Mbunge na wakaniambia kwamba kuna matatizo. Na mimi nikaagiza kwamba ranchi ikae na wenyeji wanao izunguka ili waweze kutatua matatizo hayo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uongozi wa ranchi ulikutana na wenyeji, ng,ombe ikachinjwa, wakala na wakakubali kwamba sasa mambo yameisha.

Sasa ninalolisema ni kwamba kuhusu mabati hilo sio kitu kikubwa sana, sana tutarudia tuseme jamani wasaidieni. Kufuatana na waraka wa Baraza la Mawaziri na 2 ya 2002, lilisema kwamba hiyo ya ranchi iwe ya mfano.

Kwa hiyo, hatutaweza kuvunja huo uamuzi wa Baraza la Mawaziri ila tutakachofanya ni kuhakikisha kuwa kuna mahusiano mazuri kati ya uongozi wa ranchi na wenyeji wanaoizunguka ili waweze kuwapa kidogo hata mabati hayo ya kujengea au kuwajengea hata darasa mojaau madarasa mawili hivi kwa mwaka. Hiyo siyo mbaya uhusianao huo, tukahakikisha kwamba upo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri tunaendelea katika Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Janista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho. *(Makofi)*

Na. 97

**Uwezeshaji wa mpango wa Uzalishaji Bora wa Mazao**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mpango wa maendeleo na ukuzaji wa uchumi wa mwaka 2008/2009 unalenga kuongeza uzalishaji bora wa mazao wenye kuleta tija na kuongeza nguvu ya umiliki wa soko kwa ufanisi; na kwa kuwa katika Jimbo la Peramiho wananchi wameanzisha kilimo cha miwa kwa ajili ya kutengeneza sukari na *bioethanol* itoayo

nishati na kwamba nguvu ya Halmashauri kupitia miradi haitoshelezi kuimarisha mradi huo:-

Je, Serikali Kuu iko tayari kuongeza nguvu za kifedha na kimafunzo katika kufanikisha mradi huo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kufuatilia kwa karibu uwekezaji katika uzalishaji wa sukari Mkoani Ruvuma. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mhagama kwamba Serikali inatoa kipaumbele kwenye uzalishaji wa sukari humu nchini ili kutosheleza mahitaji ya kitaifa na vile vile kuzalisha ziada kwa ajili ya soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ushauri wa Mheshimiwa Mhagama, Wizara yangu ilituma watalaam wa Bodi ya Sukari kuchunguza kwa karibu uwezekano wa kuendeleza zao la miwa mkoani Ruvuma katika mabonde ya Wilaya za Songea, Mbinga na Namtumbo. Kwa jumla watalaam walibaini kwamba upo uwezekano wa kulima miwa na kuzalisha sukari mkoani Ruvuma. Mapendekezo ya kitaalam ni ujenzi wa kiwanda cha kati aina ya *Khandsari*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatoa wito kwa uongozi Mkoani Ruvuma kuhamasisha sekta binafsi ndani na nje ya mkoa kuwekeza katika aina ya kiwanda kilichopendekezwa. Wizara yangu itaunga mkono jitihada hizo. *(Makofi)*

Aidha, kupitia Bodi ya Sukari Serikali itaendelea na utoaji wa mafunzo kwa wakulima wa miwa kwa ajili ya sukari na kuwasaidia kupata mbegu bora za miwa. Vile vile ninazishauri Halmashauri za Wilaya Mkoani Ruvuma kujumuisha uendelezaji wa kilimo cha miwa katika mipango yake ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya (*DADPs*).

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika majibu ya Naibu Waziri anasema kwamba sasa ni wakati muafaka kwetu kuendelea kuhamasisha sekta binafsi na hivyo hivyo baada ya uhamasishaji huo Serikali itaunga mkono jitihada hizo.

(1) Kwa kuwa tayari uhamasishaji huo umeshafanyika na sekta hiyo binafsi ni wale wakulima ambao wameshaanza kazi hiyo katika Mkoa wa Ruvuma Wilaya ya Songea. Sijui hiyo sekta binafsi nyingine anayoitaka ni sekta gani labda iwe na Wazungu ama Waarabu. Mimi sielewi, kwa uhamasishaji huo, uko tayari na ndiyo ahadi iliyotolewa na Serikali. Sasa ni lini wanakuja kutekeleza ahadi yao ya kuwasaidia hawa

wakulima? Huo uhamasishaji siyo *physibility Study* inayochukua miaka ishirini, kazi hiyo imekwishakamilika.

(2) Kwa kuwa umuhimu huu wa sukari na nishati ya *ethanol* ni suala la kimsingi na linajulikana kwa maendeleo ya nchi hii ya Tanzania na wananchi wa Litisha, Magagula, Kilagano, Lilambo wameshaanza kazi hiyo na imebakia hatua ya Serikali kuunga mkono na Naibu Waziri alishaahidi hivyo. Je, anataka kuniambia kwamba majibu yake yataendelea kuwa ahadi tu na siyo utekelezaji, leo anawaambia hivyo wananchi wa Jimbo la Peramiho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika Wizara ya Kilimo tuna programu mbili kubwa ambazo zinaendelea sasa hivi. Kuna programu hii ya *ASDP* ambayo kule Wilayani inatekelezwa kwa *DADPs*. Hapo ndipo tunapoweza kusaidia kilimo hiki cha miwa. Hatuna programu nyingine kwa sasa. Vile vile nimjulishe Mheshimiwa Mhagama kwamba Serikali haijengi viwanda, wanaojenga viwanda ni sekta binafsi. Lakini Serikali inaandaa mazingira kwa ajili ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za ujenzi wa kiwanda na uwekezaji katika kiwanda cha kati kama nilivyokieleza ni bilioni mia mbili na wakulima hawa wa Ruvuma wanatakiwa wawe na hekta elfu kumi ili waweze kuzalisha sukari tani laki moja kwa mwaka ambayo inahitaji miwa tani milioni moja. Kwa maana hiyo lazima wakulima hawa wajiandaye kwa kiasi kikubwa cha fedha lakini vile vile kwa kiasi kikubwa cha ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la pili linafanana na jibu la kwanza. Uwezekaji katika *ethanol* unahitaji eneo kubwa wa zaidi ya hekta elfu kumi na kuzalisha sukari zaidi ya tani laki moja. Kwa hiyo, sisi tunachoweza kufanya ni kwamba fedha zinazotolewa kwa ajili ya *DADPs* zinaweza zikasaidia lakini wakishaanza tutaangalia uwezekano mwingine wa kuwasaidia lakini Serikali haijengi viwanda. *(Makofi)*

Na. 98

**Kilimo cha Machungwa Kilombero**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Wilaya ya Kilombero, Kata ya Taweta Masagati, kunalimwa sana machungwa ambayo aina yake haipo sehemu nyingine hapa Tanzania; na kwa kuwa Machungwa hayo yameingiliwa na ugonjwa ambao wananchi hawaelewi tiba yake:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kupeleka watalaamu wa kitengo cha *horticulture* Tengeru ili kwenda kubaini ni ugonjwa gani unaoshambulia matunda hayo?

(b) Je, Serikali itatoa msaada gani wa huduma za kiugani ili uzalishaji wa machungwa hayo uwe wa kibiashara kwa ukombozi wa wananchi kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHARIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepeleka watalaam wa *horticulture* kutoka kituo cha utafiti cha Katrin Ifakara. Watalaam hao walitembelea vijiji maarufu kwa kilimo cha machungwa vya Taweta, Ipinde na Tanganyika katika Kata ya Masagati ambako walichunguza michungwa kuhusiana na ugonjwa huo. Wataalam waligundua kwamba miti ya michungwa inasumbuliwa na ugonjwa wa ukungu unaotokana na vimelea aina ya *"phytopthora SPP"*. Dalili kuu za ugonjwa ni miti ya michungwa kukauka na mingine kufikia hatua ya kupasuka sehemu ya shina hadi kwenye mizizi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutafiti na kuzalisha aina bora zaidi za mbegu inayokinzana na magonjwa mbali mbali ukiwemo unaosababishwa na vimelea vya *phytopthora SPP*. Aidha ili kilimo cha michungwa kiwe cha kibiashara na mkombozi wa wananchi kiuchumi Serikali itaendelea kuwaelimisha wakulima yafuatayo:-

(i) Kung'oa michungwa iliyoathirika na kupanda michungwa mipya pamoja na kuihudumia kwa kuzingatia Kanuni za kilimo bora cha machungwa.

(ii)Kusisitiza umuhimu wa kunyunyuzia dawa michungwa ambayo bado kukauka kwa kutumia dawa ijulikanayo kama *bordeaux mixture* ya kukinga ya michungwa dhidi ya ugonjwa huo wa ukungu.

(iii)Serikali ipo katika mchakato wa kuendeleza bustani(*nursery*) za matunda mbalimbali michungwa ikiwemo, ili kuwezesha uzaishaji wa matunda hayo kuwa wa kibiashara na hatimaye matunda hayo kuwa wa kibiashara na hatimaye ukombozi wa wakulima kiuchumi.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu hayo ambayo ni faraja kwa wakulima wa michungwa Kata ile ambayo wamesumbuka kwa miaka mingi, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kabla sijauliza swali la nyongeza naomba niishukuru Wizara ya Miundombinu kwa kuunganisha Kata hii na Kata ya Idamba, Njombe ambayo kwa miaka 48 walishindwa kuwasiliana kwa kipande cha kilomita 40 tu? *(Makofi*
*)*

(a) Kwa kuwa Kata hii ya Taweta Masagati iko kilomita zaidi ya mia mbili ishirini kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Je, Wizara itakuwa tayari kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ili tuwajengee wananchi hawa soko kati ya Taweta na Idamba ili waweze kuuza mazao yao ikiwemo machungwa, asali na mpunga?

(b)Kwa kuwa kituo cha *Katrin* ambacho Naibu Waziri amekitaja huwa kinapewa fedha kidogo sana na mwaka huu tumeahidiwa kwamba Bajeti ya utafiti itaongezwa. Je, kituo hicho pia kitaongezewa fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na yeye kabisa kwamba maeneo hayo ambayo kwa kweli yana mazao ambayo wananchi wanaweza wakauza ili yasiharibike, kuna haja kabisa Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko kufanya utafiti ili kama uwezekano waweze kujengewa soko.

Kulikuwa na programu ya masoko ya kimataifa sijui itakuwa imefikia wapi. lakini kwa kutumia fedha za *DADPs* pia wanaweza wakajenga soko ambalo linalingana na fedha ambazo zinakwenda Wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kituo cha Katrin kuongezwa fedha, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli vituo hivi tunaviongezea fedha pamoja na bodi za mazao haya na niseme kituo hiki kitaongezewa fedha mwaka huu tofauti na mwaka jana na tutaendelea kuongeza fedha kwa kadri Serikali inavyojiweza.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa tatizo hili la mazao mchanganyiko, likiwepo zao la michungwa , dengu alizeti na mazao mengine ufumbuzi wake ni kuwa na bodi ya mazao haya, hapo ndipo mvutano kati ya kila Mbunge kuongea na Serikali utapungua?

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa sheria ya kuunda Bodi ya mazao mchanganyiko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada kwa ajili ya kuanzisha sheria ya bodi ya mazao mchanganyiko utaletwa mwezi Novemba katika Bunge lako Tukufu, kwa ajili ya majadiliano ili tuweze kuwa na Bodi hiyo. Nakuhakikishia kwamba Novemba Muswada huo utafika hapa.

Na. 99

**Usambazaji wa Umeme Kibakwe kwa Mpango wa *MCC***

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mpango wa *MCC*, Jimbo la Kibakwe lilipatiwa umeme kutoka kijiji cha Kibakwe kupeleka umeme Kata ya Wota na kutoka kijiji cha Lenge kupeleka umeme kijiji cha Pwaga:-

Je, Serikali haioni kuwa, kutoa umeme kutoka Iyenge moja kwa moja hadi Pwaga kwa kupitisha msongo huo porini haileti manufaa kama kutoa umeme huo Kibakwe kupitia vijiji vya Chamtumile, Ikuyu, Luhundwa, Kidenge, Munguwi hadi Pwaga.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapa Bungeni wakati wa kujibu swali la Mbeshimiwa Mbunge tarehe 4 Julai, 2007 kuhusu mradi huo wa umeme kupitia vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mbunge, *TANESCO* ikishirikiana na mshauri mwelekezi wa mradi wa MCC, ambaye ni *ESB International*, imepitia mapendekezo ya awali ya kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali yaliyochini ya mpango wa *MCC* vikiwemo vijiji Jimboni Kibakwe kwa lengo la kuboresha mapendekezo hayo ili yaweze kunufaisha wananchi wengi zaidi na kufikisha umeme wenye nguvu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maboresho hayo kwa upande wa Kibakwe njia ya umeme ikitokea Kibakwe kupitia Chamtumile, Kidenge hadi Pwaga ikiwa na urefu wa kilomita 26.8 tofauti na njia ya kilomita 23 kutoka Iyenge hadi Pwaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la kibakwe kuwa Serikali inatambua umuhimu wa umeme kufika katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ndiyo maana tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha umeme unafika maeneo hayo.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini kumpongeza sana Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia kwa karibu sana mradi huu wa umeme ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kibakwe. Tunamshukuru sana kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupa na sisi tunamwahidi kuendelea kulipa fadhila kwa ushirikiano wake huo anaouonesha katika Wizara yetu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri ya Waziri mahiri wa Nishati na Madini na Naibu wake kwa ushirikiano wanaotupa pale Wizarani lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru tu kwa kawaida mtu mwenye busara unapoomba ombi lako halafu ukapewa kidogo, lazima ushukuru kwa hicho kidogo ulichopata ndiyo uombe zaidi. Mimi niliomba umeme upitie Kijiji cha Chamtumile kutoka Kibakwe, Ikuyu, Luhundwa, Kidenge, Minguwi hadi Pwaga, lakini wamesema hawatapita Ikuyu sasa utapita Chamtumile ,Kidenge hadi Pwaga lakini Minguwi hapa haitajwi na hii haiathiri umbali wowote, umbali ni ule ule wa kilomita 26 kwa sababu ni msongo huo huo.

(a) Je, na Minguwi napo umeme utawaka?

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni lini mradi huu utaanza na matarajio ni lini utaweza kukamilika.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu kijiji cha Minguwi, suala hili linazungumzika niendelee kumwomba Mheshimiwa Mbunge tuzidi kuwasiliana kwa kushirikisha watalaam wetu, shirika la *TANESCO* lakini pia Mkandarasi mshauri tuone kwamba hapatakuwa na madhara kwa gharama ambazo zitahitajika kuunganisha eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu swali la pili ni lini mradi huu utaanza, utekelezaji wa mradi wa *MCC* kama ambavyo tumekwishakusema katika nyakati tofauti tofauti, ni kwamba umeshaanza tangu mwaka jana na sasa hivi hatua tuliyonayo tunaendelea na zoezi la kuwapata Makandarasi katika eneo ambazo mradi huu wa *MCC* unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyokumbuka mradi wa *MCC* unahusu mikoa sita na katika mikoa sita kuna Wilaya nyingi, sasa hivi tunaendelea na zoezi la kuwapata makandarasi hao na tunatarajia ifikapo mwezi wa nane zoezi la kuwapata makandarasi litakuwa limeshakamilika na tayari wataingia *site* kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa miradi hii.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:**Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa vijiji cha Nkhambi, Chunyu, Msagali, Kisokwe na Idilo wanausubiri kwa hamu mradi huu wa *MCC* na tayari *survey* imeshafanyika, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri amesoma Mpwapwa anavielewa vizuri sana vijiji hivi. *(Makofi)*

Je, kijiji cha Msagali na Berege ni kama kilomita 12, Waziri atakubaliana nami sasa vijiji vya Berege, Mzase pamoja na Mima nao wangefikiriwa kupata huduma ya umeme?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba vijiji hivi alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge navifahamu vizuri na kama alivyosema kwa usahihi mimi ni miongoni mwa wale waliosoma katika shule ya Sekondari Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kama ambavyo nimemhakikishia Mbunge wa Kibakwe kwamba masuala haya yanazungumzika, kwa sababu *survey* kwa ajili ya mradi wa MCC imeshafanyika, nimshauri pia Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa kwamba awasiliane na ofisi yetu tuone kama jambo hili linawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kutumia nafasi hii kumhakikishia kwa jambo ambalo lina *element* za kitalaam halafu lisipotekelezeka iwe lawama kwa Serikali kwamba iliahidi kitu ambacho hakiwezekani.

Kwa hiyo, nimkaribishe Mheshimiwa Mbunge tujadili kwa kushirikiana na watalaamu wetu tuone kama inawezekana lakini kama haitawezekana tutaendelea kutumia fursa zingine za kutumia mifuko kama ya mifuko kama ya Wakala wa Nishati Vijijini, tuone kama tunaweza ku-*accommodate* maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaombea. *(Makofi)*

Na. 100

**Kuanzishwa kwa Mahakama ya Kitaifa ya Uhalifu wa Kivita**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

(a)Je, kuanzishwa kwa mahakama ya Kimataifa ya uhalifu wa kivita *International Criminal Court* hadi sasa kumesaidia vipi kuimarisha na kukuza amani, demokrasia, sheria, haki za binadamu na maendeleo endelevu?

(b)Je, nchi inayokataa kujiunga na Mkataba wa Rome wa Mahakama hiyo ni utaratibu gani unaweza kutumika kuiadhibu hasa pale inapovunja haki za binadamu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mahakama ya kimataifa ya makosa ya jinai *ICC* ilianzishwa kwa mkataba wa Roma ambao ulianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2002. Tanzania iliridhia Mkataba huo tarehe 20 Agosti, 2002 na kukubali masharti yake yote.

Jukumu kuu la mahakama ya *ICC* ni kushughulikia makosa ya jinai ya kimataifa kama vile mauaji ya halaiki (*genocide)*; makosa dhidi ya binadamu yaani *(Crime Against Humanity)*, makosa yatokanayo na vita ( *War Crime)*, kama yalivyoainishwa katika ibara ya 5 ya mkataba wa Roma ikiwa makosa hayo yamefanyika baada ya tarehe 1 Julai, 2002. Lengo ni kuhakikisha kwamba mtu yeyote anayetuhumiwa kutenda makosa haya anafikishwa katika mkondo wa sheria na hataachwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mahakama inaendesha uchunguzi kuhusu malalamiko ya matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanayofanyika katika nchi nne za Kiafrika, Uganda, *DRC*, Afrika ya Kati, kama zilivyowasilishwa na nchi hizo

ambazo zote ni wanachama wa *ICC*; na Darfur (Sudan) kama ilivyowasilishwa na Baraza la Usalama la umoja wa mataifa kwa kuwa Sudani si mwanachama wa *ICC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa uchunguzi wa kimataifa na taarifa zinazotolewa na wahanga, mamilioni ya raia wameuawa nchini Uganda, *DRC*, Afrika ya Kati, na hata Darfur kutokana na mauaji ya halaiki na yale ya kuangamiza, ukatili, ubakaji, ubakaji wa hadharani, raia kupotea, matumizi ya watoto wadogo kama askari wa hadharani, raia kupotea, matumizi ya watoto wadogo kama askari wa vita na hata utumwa wa ngono *(Sexual Slavery)* kuanzia 2002.

Ni dhihiri kwamba mahakama ya *ICC* kwa kuyaona makosa haya na kuyafanyia uchunguzi kwa nia ya kuwafikisha wahusika kwenye mkondo wa sheria, inasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha demokrasia, sheria haki za binadamu na maendeleo endelevu kwa kuwa kumeleta uelewa na hofu kwa kiasi kikubwa miongoni mwa jumuiya ya kimataifa kwa kujua kwamba:-

(i) Ukiukwaji wa haki za binadamu utaendena na adhabu inayostahili na hivyo kutapunguza kwa kiasi kikubwa au kutokomeza kabisa ukiukwaji huo.

(ii) Haki na usalama wa raia ni budi viheshimiwe.

(iii) Kushiriki katika kudumisha na kuheshimu utawala wa sheria ndiyo njia pekee ya kuleta amani na maendeleo endelevu ulimwenguni kote. Ni vema ikaeleweka kwamba, kwa malengo ya *ICC* kunategemea kwa kiasi kikubwa ushirikiano unaotolewa na nchi zote duniani hususani nchi wanachama wa mahakama hii.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za kimataifa, nchi hujiunga na mkataba wowote kwa hiari, hailazimishwi.

Hata hivyo kwa kuwa nchi karibu zote duniani ni wanachama wa Umoja wa Mataifa, maamuzi ya umoja huo ikiwa ni pamoja na yale yanayotolewa na vyombo vikuu vya umoja huo, ni lazima yaheshimiwe na kutekeleza na nchi zote. Nchi ambayo si mwanachama wa mkataba wa Roma inaweza kuwajibika chini ya mkataba huo kwa kutoa ushirikiano kwa mahakama ya *ICC* pale itakapohitajika kufanya hivyo, endapo Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa litathibitisha kwamba kumekuwapo tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu katika nchi hiyo. Baraza hilo litalazimika kwa mujibu wa mkataba wa Roma, kuwasilisha tuhuma hizo kwenye mahakama ya *ICC*. Kwa njia hii basi nchi hiyo italazimika kushirikiana na mahakama ya *ICC* na kuheshimu maamuzi yake.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kufafanua kuhusiana na chombo hiki muhimu kwa ajili ya demokrasia katika nchi yetu, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi ya Marekani ni kati ya nchi ambayo inashabikia sana suala zima la demokrasia, haki, uhuru, na usawa kwa wote, lakini baada ya kufuatilia nimegundua ya kwamba Marekani ni kati ya nchi ambayo haijaridhia mpaka leo. Kwa nini Marekani anakataa kuridhia mkataba muhimu huu ambao unajenga demokrasia katika nchi.

(ii) Kwa kuwa, sote tunafahamu Mahakama yetu ya Arusha ambayo hivi karibuni itafunga ofisi zake ambayo imekuwa ikishughulika na mauaji ya halaiki kule Rwanda. Kwanini tusitumie nafasi hii ili kuiomba mahakama ya *ICC* iliyopo Mjini Hague, Uholanzi ikafungua kanda ya Afrika ili kuendelea kupambana na viongozi waovu katika bara hili na kurudisha heshima ya Mwafrika popote ilipo ili Mahakama badala ya kusubiri kwenda Hague, Arusha ifanye kazi hiyo kwa ajili ya Bara lote la Afrika?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mhehsimiwa Mwenyekiti, awali Marekani ilipinga au ilipiga kura kupinga kuanzishwa kwa Mahakama ya *ICC*, lakini tarehe 31 Disemba 2000 Rais Clinton bila kutegemewa alibadili maamuzi hayo na kuweka saini mkataba huo. Lakini aliweka saini kwa kusema kwamba hatamshauri mrithi wake kupeleka mkataba huo Bungeni kuridhiwa. Wakati Rais Bush alipoingia madarakani utawala wake ukatangaza kufuta saini hiyo, kwa hivyo siyo tu Marekani haijaridhia lakini hata saini haijaweka kwa sababu saini ile ilifutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya Marekani Kutosaini mkataba ule zipo nyingi lakini mbili kubwa ni kwamba inahisi kwamba mkataba huo unaingilia *(National sovereignty* ) yao. *(Makofi)*

Pili kwa mujibu ya Katiba yao kuridhia mkataba wa aina hiyo wa kimahakama inabidi ku-*ammend Constitution* yao, kwa sababu Katiba yao inaweka wazi kwamba *Supreme Court* ndiyo chombo cha mwisho cha maamuzi kwa Marekani na kwa hivyo hawawezi kuruhusu chombo kingine cha Mahakama kuridhiwa na Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti hizo ndiyo sababu mbili kubwa, lakini hata hivyo, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi maadamu Baraza la Usalama litaona kuna haja ya kiongozi yeyote yule kwa vitendo alivyovifanya dhidi ya haki za binadamu ina haki ya kumwasilisha *ICC* hata kama siyo mwanachama wa *ICC*.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kutosaini mkataba huo nchi haiwezi kuepuka kupelekwa mbele ya *ICC* na sheria kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la pili ni kweli tunamajengo mazuri kule Arusha ambayo yanamaliza muda wake mwaka ujao na tayari tumekwishaomba kwa *ICC* wakati Rais wa *ICC* alipotembelea Tanzania hivi karibuni kwamba kama kutatokea haja ya Afrika kuwepo kwa *Regional Administration* yeyote basi majengo ya *ICTR* yafikiriwe na Wizara yangu itafuatilia haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Waheshimiwa Wabunge, swali hili peke yake limechukua dakika kumi na nne pamoja na maswali ya nyongeza, naomba tuendelee. *(Makofi)*

Na. 101

**Vitambulisho vya Uraia Kutolewa kwa Wakimbizi**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imedhamiria kutoa vitambulisho vya uraia kwa wananchi wote nchini:-

(a)Je, kwa nini vitambulisho hivyo vitolewe kwa wakimbizi waliopo nchini na si Watanzania?

(b)Je, endapo wakimbizi watapewa vitambulisho Serikali haioni kuwa pindi wakirudi kwao watu hao watatumia vitambulisho hivyo kufanyia ujangili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba vitambulisho vitakavyotolewa ni vitambulisho vya utaifa na sio vya uraia kama alivyobainisha Mheshimiwa Mbunge katika swali lake. Vitambulisho hivi vitatolewa kwa Watanzania wote walio na umri wa miaka 18 na kuendelea na wageni wote waishio nchini kihalali. Wageni hao ni pamoja na wakimbizi na raia wote wa nchi mbalimbali wenye vibali vya kuishi hapa nchini.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, vitambulisho vitakavyotolewa kwa wakimbizi vitakuwa vitambulisho maalum na vyenye muda maalum wa kutumika ambapo kabla ya kuondoa hapa nchini Wakimbizi wote watapaswa kurejesha vitambulisho hivyo.

Aidha, vitambulisho hivyo vitabainisha uraia wa kila mkimbizi na mkimbizi atabaki na uraia wa nchi yake. Iwapo Mkimbizi atarejea kwao na kurudi nchini kinyemela na akaamua kufanya ujangili/uhalifu basi atachukuliwa hatua kama ilivyo kwa wahalifu wengine hapa nchini. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize kama ifuatavyo.

Kwa kuwa amesema kwamba wakimbizi watakaporejea nchini kwao vitambulisho vile vitarejeshwa. Je, kwa hao wageni ambao wameingia kihalali hapa nchini na wakapewa vitambulisho hivyo. Je, na wao watavirudisha vitambulisho hivyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo na wao watarudisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mafupi na kutokana na muda Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Lakini nitaendelea ili kumaliza haya maswali yaliyopo. *(Makofi)*

Na. 102

**Ombi La Kufanya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa EAC Mwaka 2010 Kigoma**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** liuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge na wa Bunge la Tisa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niliomba Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2010 (ambapo Tanzania itachukua Uenyekiti) ufanyike Kigoma na Serikali ikasema inatafakari ombi hilo.

(a)Kwa kuwa, kuna faida kubwa kwa miji inayoandaa Mikutano kama hiyo kama vile kutangazwa na kuongeza watalii na wawekezaji; na kwa kuwa, sasa kuna *facilities* za kutosha kuandaa Mkutano huo kwa kuwa hifadhi za Gombe na Mahale zinaweza kutoa fursa kwa Marais kuona utajiri wa maliasili tulizonazo. *(Makofi)*

Je, Serikali iko tayari kuanza mchakato wa mkoa wa Kigoma kuwa mwenyeji wa Mkutano huo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kulifanya jambo hili liwe desturi ili miji mingi nchini ifaidike na *EAC?*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nikupongeze kwa vazi rasmi la viwango. Kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya kwa kuomba mkutano huo ufanyike nje ya Makao Makuu ya Jumuiya kunaambatana na gharama mbalimbali.

Kwa mujibu wa taratibu za Jumuiya ya Afrika Mashariki nchi ikiomba kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi, inatakiwa kulipia gharama za Mkutano kama vile Ukumbi, Shajala, Uchapishaji, Maji, chai, chakula, burudani, gharama za usafiri kwa wajumbe wakati wa mkutano na kadhalika.

Aidha, Nchi iliyoomba hulazimika kulipia gharama za usafiri, malazi na posho ya kujikimu kwa Watumishi wa Makao Makuu ya Jumuiya watakaoshiriki kwenye Mkutano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo niliyotoa hapo juu, hivyo kuomba kuwa mwenyeji wa mikutano ya aina hiyo nje ya Makao Makuu ya Jumuiya ni ya gharama kubwa. Kwa hiyo, itategemea sana na hali ya kiuchumi. Hali ya kiuchumi ikiruhusu kufanyika kwa mikutano ya aina hiyo kwa Kigoma na kwingineko linaweza kuwa jambo zuri kwa maendeleo ya kiutalii na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naomba nichukue fursa hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Kigoma, akiwemo na Mheshimiwa Mbunge, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuutangaza Mkoa wa Kigoma, kiutalii na uwekezaji.

Na 103

**Fedha za Mikopo Kwa Wafunzi wa Vyuo Vikuu Nchini**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, iko Bodi ya Mikopo ambayo inatoa mikopo kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya juu kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa wanafunzi wanaosomea Sheria katika Chuo cha Tunguu- Zanzibar wa mwaka wa nne (4) hawapati fedha za *field/research:*-

Je, Serikali inaweza kutoa sababu za msingi kwa nini wanafunzi hao hawapatiwi fedha kwa ajili ya *Field* na *Research.*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu unazingatia Sheria Na.9 ya mwaka 2004 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo pamoja na mwongozo na vigezo vya utoaji mikopo ambavyo hutolewa kila mwaka kabla ya kuanza mwaka mpya wa masomo.

Aidha, utoaji wa mikopo ya mafunzo kwa vitendo pamoja na utafiti huzingatia mihula ya kalenda ya chuo. Mikopo ya mafunzo kwa vitendo na utafiti hutolewa tu pale ambapo mafunzo au utafiti husika unapofanyika ndani ya mwaka wa masomo au kipindi cha kozi husika.

Iwapo mafunzo kwa vitendo au utafiti unafanyika baada ya mwanafunzi kuhitimu masomo yake, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haiwajibiki kutoa mikopo kugharimia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa *"Zanzibar University"* wanaolalamika kutokukopeshwa mikopo ya mafunzo kwa vitendo, ni wahitimu wa kozi ya Sheria katika chuo hicho.

Wanachuo waliohitimu masomo yao sio wanafunzi tena na hivyo hawastahili kupewa mikopo yoyote chini ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Baada ya kuhitimu Shahada ya Sheria, wanasheria wapya wanapaswa kujiunga na *"Law School of Tanzania"* kama ilivyo kwa wanasheria wanaohitimu katika vyuo vikuu vyote nchini.

Mheshmiwa Mwenyekiti, kipengele cha 2 cha Sheria na. 5 ya mwaka 2007 iliyoanzisha " *Law School of Tanzania*" kinaweka bayana kuwa Sheria hiyo itatumika kwa wahitimu yeyote wa kozi ya Sheria kutoka chuo chochote cha elimu ya juu kilichopata ithibati hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo Kikuu cha Zanzibar ni kati ya vyuo ambavyo ithibati yake imetolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Hivyo tunawashauri wahitimu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar wajiunge na "*Law School of Tanzania*" baada ya kozi yao.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, kwa sababu zipi za msingi, hata kufikia Chuo Kikuu cha Zanzibar ithibati yake kutolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili. Katika umalizaji wa Chuo, inafikia kiwango pale wanafunzi kufanyiwa *graduation*, lakini kwa kuwa bado wako katika *field*; na kama upande wa *field* inachukua kama miezi mitatu (3), wanahitaji *accommodation, meals and so on*. Kwanini, kufikia kiwango hiki wasiweze kupata fedha zao ili kuweza kujikimu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** *TCU* inahusika pia Zanzibar kwasababu elimu ya juu, ni *element* ya Muungano. Kwa hiyo, hilo ndilo jibu lake. Lakini kwa wanafunzi hawa wa *Zanzibar University*, mara nyingi katika kutua mikopo, pamoja na vigezo vingine; Bodi ya mikopo inapenda pia ifahamu taaluma inayotolewa katika programu ile. Kwa hiyo, tunahitaji kupata *prospectus* ya wanafunzi hawa ili tuweze kujua ratiba, wakati gani wataenda katika mafunzo ya vitendo.

Sasa wanafunzi wa *Zanzibar University*, Chuo hiki kilipoombwa kupeleka *prospectus* Bodi ya mikopo Tanzania ili waweze kuchunguza kwamba ni wakati gani wanaenda kwenye mafunzo ya vitendo. Chuo hawakufanya hivyo; mpaka tarehe 22

Juni, 2009, ndio wamepeleka *prospectus* yao. Wakati huo walipopeleka *prospectus* ile haionyeshi kwamba wana mafunzo ya vitendo walipokuwa bado ndani ya Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa hawana vitendo wakati wa mwaka wa nne wa mafunzo yao ni baada ya kuhitimu na ndiyo maana tunasema kwa taratibu zilizopo badala ya *internship*, sasa hivi wanaenda *Law School of Tanzania* na hawastahili kupata mkopo. Naomba uwaelimishe Mheshimiwa Mbunge, na kwamba kwa kweli hawastahili mkopo huu. Badala yake wawachie wadogo zao ambao bado wanaendelea wapate mkopo huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, maswali yamekwisha na muda wa maswali nao umekwisha. Sasa nina tangazo la wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, ambao ni watoto wake wanaosoma shule ya Sekondari Arumeru, Abdul Mohamed Rished na Omar Mohamed Rished. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wanaofuata ni wageni sita wa Mheshimiwa Ephraim Madeje ambao ni viongozi wa Sina *Group Anglican* Dodoma wote kwa pamoja wasimame. Ahsanteni karibuni sana. Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei, ambao ni mwalimu Sixbert Gei na Sister Martha Nakei, kwa pamoja naomba wasimame.

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan, ambaye ni mwanamuziki maarufu wa siku nyingi Komando Hamza Kalala. Tunaomba usimame tukuone, yuko wapi? Haya, bahati mbaya atakuwa labda *basement* kutokana na nafasi finyu.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu wa mwisho, ni wageni wa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ambao ni Juma Said Saanani, Mjunbe wa Baraza Kuu na Mkurugenzi wa Uchagizi *CUF* Taifa, tunaomba usimame. Mwingine ni Salum Rajab Soud, Mjumbe wa Kamati Tendaji, Wilaya ya Temeke *CUF* Dar es Salaam. Ahsante sana. Hayo yalikuwa matangazo ya wageni, sasa kazi. *(Makofi)*

Naomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwamba Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anawatangazia Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wakutane leo baada ya maswali, kwa ruhusa ya Spika, katika Ukumbi Namba 219, jengo la Utawala. *Agenda* ya kikao hicho, ni kupitia na kudhibitisha maoni ya Kamati.

Naomba pia niwatangazie pia kuwa Kamati ya Ardhi Maliasili na Mazingira kwamba leo tarehe 24 mwezi wa sita, 2009 saa saba mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 227. kwa hivyo Wajumbe wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa. Mwisho wa matangazo ya kazi. *(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, Kanuni Na. 49, naomba kutoa Kauli ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 9 Februari, 2009 nilitoa Kauli ya Serikali katika Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika kauli hiyo, nilitoa maelezo kuhusu mipango ya Serikali ya kutoa huduma ya maji vijijini.

Nilieleza pia kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Maji safi na Usafi wa Mazingira Vijijini uliotekelezwa kwenye wilaya 14 nchini kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia kuanzia mwaka 2002 hadi Juni, 2008.

Katika maelezo yangu nilibaini kuwa kati ya vijiji 138 vilivyokuwa vinufaike, miradi ya vijiji 119 ilikamilika chini ya mradi huo ambapo miradi ambayo haikukamilika itatekelezwa kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Vile vile, nilitoa maelezo kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na jitihada za kupata wataalam washauri wa kuzisaidia Halmashauri za Wilaya na Miji kusanifu miradi, na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Vijijini.

Kauli ya Serikali ya mwezi Februari, 2009 ilionyesha hatua iliyokuwa imefikiwa katika kupata wataalam washauri watakaozisaidia Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira.

Kauli ya Serikali ya mwezi Februari, 2009 pia iliainisha suala la Wahandisi wa Maji walioajiriwa kwa ajili ya Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ili kuimarisha utendaji na usimamizi wa Programu. Nilielezea juhudi za Serikali za kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi wa Halmashauri ili kutekeleza Programu ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuandaa Sera ya Maji ya mwaka 2002, mwaka 2007 Serikali ilianza kutekeleza Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Sheria mbili mpya za Maji; Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira zilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2009 katika mkutano wake wa kumi na Tano. Sheria hizi zilisainiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 12 Mei, 2009 na zinatarajiwa kuanza kutumika tarehe 1 Agosti, 2009. Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira inasimamia kupeleka madaraka na wajibu zaidi katika ngazi ya Halmashauri kama Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 inavyoelekeza. Wajibu huu unahusu vilevile usajili na usimamizi wa vyombo huru vya watumiaji maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu hii inatekelezwa na makundi makuu manne ya wadau ambao ni Wananchi, Taasisi zisizo za kiserikali, Madhehebu za Dini, Halmashauri na Serikali Kuu. Mchango wa wananchi katika ujenzi wa miradi ya maji

unaendelea kutolewa kwa njia ya fedha taslimu na nguvu kazi. Lengo ni kuimarisha umiliki wa miradi na uendeshaji wa huduma ya maji. Miradi inayotekelezwa na makundi mbalimbali ya wadau ni ile yenye kuleta matokeo ya haraka na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafi wa mazingira, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inafanya yafuatayo:-

Uhamasishaji wa usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi katika jamii na taasisi. Mafunzo kwa mafundi kutoka kwenye maeneo ya vijiji ambako miradi ya maji inatekelezwa kuhusu kutengeneza aina mbalimbali za maliwato na faida zake. Ujenzi wa maliwato za mfano.

Uhamasishaji na utengenezaji wa aina tofauti ya vifaa vya kunawia mikono. Kuhusika kwa Wizara yenye dhamana ya maji na usafi wa mazingira na afya ya binadamu kunatokana na ukweli kwamba maradhi mengi yanatokana na matumizi ya maji yasiyo salama, kutopatikana kwa maji, au maji mengi yanayofurika au yanayotuama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kupitia miradi ya maji inayoleta matokeo ya haraka, kulingana na mipango na vipaumbele vya Halmashauri zenyewe. Serikali pia imeendelea kutekeleza miradi kupitia taasisi mbalimbali.

Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, miradi ya maji 1,246 kati ya 1,478 iliyokusudiwa kujengwa ilikamilika. Vituo vya kuchotea maji 2,603 vilijengwa na watu wapatao 650,750 walinufaika na huduma ya maji. Wananchi 885,867 walihamasishwa kuhusu usafi wa mazingira, na ujenzi wa vyoo bora vya shimo 1,392 vilijengwa. Ofisi 42 za Idara za Maji za Halmashauri zilikarabatiwa na ofisi 11 mpya zilijengwa. Halmashauri zilizopewa fedha za miundombinu ya maji zilikamilisha utekelezaji wa miradi. Utekelezaji ulifanyika kwa fedha za mfuko wa pamoja (*water basket fund).* Miradi ambayo haikukamilika iliendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Kwa mwaka wa 2008/2009, taarifa zilizotolewa na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri hadi kufikia mwezi Machi 2008, zimeelezea hatua za utekelezaji wa miradi mbalimbali. Miradi ya maji 1,151 kati ya 2,470 iliyopangwa kutekelezwa ilikuwa imekamilika. Vituo vya kuchotea maji 2,873 vimejengwa na watu wapatao 692,000 wananufaika na huduma ya maji. Watu wapatao 527,612 wamehamasishwa kuhusu usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi na vyoo vya shimo 233 vimejengwa. Ofisi tatu za Idara za Maji za Halmashauri za Wilaya za Karatu, Liwale, na Shinyanga zimekarabatiwa. Ofisi nane mpya za Halmashauri za Meru, Kilolo, Ruangwa, Morogoro, Newala, Kahama, Singida na Sikonge zimejengwa. Vilevile, ofisi moja ya Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga imefanyiwa ukarabati.

Kwa ujumla, kati ya mwaka 2007 na mwezi Machi, 2009 jumla ya miradi ya maji 2,397 yenye vituo vya kuchotea maji 5,476 imejengwa au kufanyiwa ukarabati, ambapo watu wapatao 1,342,750 wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwezi Juni 2007 na Juni 2008, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 31.2 kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa yote. Fedha hizo zilitokana na mkopo nafuu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Halmashauri zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji pamoja na kujijengea uwezo. Halmashauri ambazo hazikutimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo zilipewa fedha kwa ajili ya kujijengea uwezo tu.

Kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi pamoja na kujenga uwezo kwa Halmashauri. Hadi mwezi Oktoba 2008 Serikali ilikwishatuma shilingi bilioni 23.02 kwenye Halmashauri na shilingi milioni 490.52 kwenye Sekretarieti za Mikoa. Mwezi Mei, 2009 kiasi cha shilingi bilioni 5.4 zimetumwa kwenye Halmashauri zote nchini kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ikiwa ni gharama za wataalam washauri ambao baadhi yao walianza kazi mwezi Aprili, 2009.

Kwa mwaka huu wa fedha tayari Serikali imetuma shilingi bilioni 28.95 kwa Halmashauri na Serkretariati za Mikoa. Hivyo basi, kati ya mwezi Juni 2007 na Mei 2009, jumla ya shilingi bilioni 60.15 zimetumwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Kiwango hicho cha fedha ni uthibitisho kwamba Serikali inatekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa miradi katika vijiji 10 katika kila Halmashauri ni sehemu tu ya Programu hiyo. Kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2009, Serikali itatuma shilingi bilioni 25.1 kwa Halmashauri zote kwa ajili ya utekelezaji wa Programu. Fedha hizo zitatumika katika kujenga uwezo wa Halmashauri na kugharamia wataalam washauri watakaoanza kazi za usanifu wa miradi ya maji katika vijiji vilivyoainishwa na kila Halmashauri. Kuanzia mwezi Juni , 2007 hadi mwezi Juni, 2009, Serikali itakuwa imetumia jumla ya shilingi bilioni 85.3 kutoka kwenye mfuko wa pamoja wa kutekeleza programu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa programu unahusu pia ukarabati na ujenzi wa mabwawa, hasa katika maeneo kame. Wizara yangu imekuwa ikijihusisha moja kwa moja na ujenzi wa mabwawa ya ukubwa wa kati na mabwawa makubwa. Kazi hii nayo itahamishiwa kwa Halmashauri kama ilivyo kwa miradi mingine itakayosimamiwa na wataalam washauri. Katika mwaka 2008/2009 ujenzi wa mabwawa 18 umefanyika na kufikia hatua mbalimbali za utekelezaji kama nilivyo onyesha katika Jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Programu unahusu pia miradi ambayo inajengwa kwa fedha ambazo hazitoki kwenye mfuko wa pamoja. Fedha hizo huelekezwa na Serikali na washirika wetu kwenye miradi mahsusi. Miradi ya aina hiyo ipo katika Halmashauri nyingi ikifadhiliwa na asasi au mataifa mbalimbali au kwa fedha za mapato ya ndani.

Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Maji wa Moshi Vijijini na Hai unaotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani, Mradi wa Maji wa Monduli na Longido uliotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mradi wa Maji wa Mkoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mara, Mwanza na Tabora unaotekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, na Mradi wa Maji Mkoa wa Shinyanga na Dodoma uliotekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea ya Kusini.

Ipo miradi mingine ya aina hiyo ambayo imekuwa ikitekelezwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali na mashirika ya kidini. Kati ya mwaka 2007 na Machi 2009, inakadiriwa kwamba fedha zilizotumika katika kutekeleza miradi hii na ile niliyoitaja ni shilingi bilioni 123.4.

Jedwali Na. 2 linaonyesha vyanzo mbalimbali vya fedha zilizotumika kutekeleza programu nje ya mfuko wa pamoja wa programu. Utekelezaji wa miradi mbalimbali kupitia mfuko wa pamoja na nje ya mfuko, umechangia katika kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 57.1 mwezi Desemba, 2007 hadi asilimia 58.3 ilipofika Desemba 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza miradi mikubwa ya maji vijijini, maarufu kama Vijiji 10 katika kila Halmashauri, Halmashauri zimeanza kuajiri wataalam washauri ambao watasaidia kusanifu na kusimamia utekelezaji.

Katika Kauli za Serikali za mwezi Julai, 2008 na Februari 2009, nilieleza kuhusu upatikanaji wa wataalam washauri kwa ajili ya Halmashauri, zikiwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la Halmashauri 82 na la pili ni lenye Halmashauri 17.

Halmashauri hizo ndizo zilizowahi kupata mapendekezo ya Wataalam Washauri mapema. Halmashauri hizo 99 sasa ziko katika kundi moja kwa vile zote zimefikia hatua inayofanana. Kundi la tatu lilikuwa la Halmashauri 33 zilizorudia zoezi zima.

Hivi sasa, kuna makundi mawili tu, kundi la Halmashauri 99 na kundi la Halmashauri 33. Mchakato wa kupata Wataalam Washauri umefika hatua zifuatazo kwa makundi mawili ya Halmashauri niliyoyaainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Halmashauri 99 zilizowahi kupata mapendekezo ya Wataalam Washauri, rasimu za mikataba ya Halmashauri 38 zimekwishapata ridhaa ya Benki ya Dunia kwa ajili ya Halmashauri hizo kusaini mikataba kati yake na Wataalam Washauri. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri 25 zimekwisha saini mikataba na Wataalam Washauri tayari wameanza kazi za usanifu wa miradi.

Halmashauri ambazo zimekwishasaini mikataba ni Monduli, Longido, Kongwa, Manispaa ya Bukoba, Chato, Hai, Moshi, Lindi, Kilwa, Liwale, Babati, Serengeti, Bunda, Mbeya, Nanyumbu, Mtwara, Magu, Sengerema, Rufiji, Mpanda, Singida, Mji wa

Korogwe, Lushoto, Muheza na Jiji la Tanga. Kwa maana ya utekelezaji wa miradi, kwa Halmashauri hizi 25 mradi umeanza.

Jumla ya Halmashauri 13 zimepata ridhaa mwezi huu ya kusaini mikataba baina yao na Wataalam Washauri. Hivyo basi, bado zinawasiliana na kampuni zilizoshinda ili kupanga tarehe ya kusaini mikataba hiyo.

Halmashauri hizo ni Manispaa ya Arusha, Karatu, Mpwapwa, Iringa, Kilolo, Mji wa Njombe, Misenyi, Mwanga, Hanang', Mbulu, Ulanga, Geita, Songea na Namtumbo.

Rasimu ya mikataba ya Halmashauri 54 ziko Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kusaini mikataba. Halmashauri hizo ni Arusha, Ngorongoro, Kinondoni, Bahi, Chamwino, Kondoa, Manispaa ya Dodoma. Ludewa, Njombe, Manispaa ya Iringa, Mufindi, Iringa, Makete, Biharamulo, Karagwe, Muleba, Ngara, Bukoba, Kibondo, Kigoma/Ujiji, Kigoma, Kasulu, Siha, Same, Rombo, Mji wa Lindi, Nachingwea, Ruangwa, Morogoro, Manispaa ya Morogoro, Kilosa, Kilombero, Masasi, Manispaa ya Mtwara, Tandahimba, Newala, Jiji la Mwanza, Mji wa Kibaha, Kibaha, Mafia, Mkuranga, Kisarawe, Mji wa Mpanda, Manispaa ya Sumbawanga, Sumbawanga, Nkasi, Mbinga, Manispaa ya Singida, Iramba na Manyoni.

Rasimu za mikataba ya Halmashauri mbili (2) za Temeke na Manispaa ya Moshi zinafanyiwa mapitio na Wizara yangu kabla ya kuziwasilisha Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kusainiwa. Halmashauri tano (5) za Ilala, Bagamoyo, Meru Bariadi na Mvomero bado zinafanya marekebisho katika rasimu ya mikataba yao kulingana na maelekezo yaliyotolewa. Matarajio yetu ni kwamba rasimu za mikataba ya Halmashauri zote 99 zitakuwa zimepata ridhaa ya Benki ya Dunia ifikapo mwisho mwa mwezi Julai 2009, mikataba kusainiwa na wataalam washauri kuanza kazi.

Halmashauri 33 ni zile ambazo zilirudia kutangaza kupata Wataalam Washauri. Kati ya Halmashauri hizo, Halmashauri 32 zimepata ridhaa ya kufungua mapendekezo ya kifedha kutoka Benki ya Dunia. Halmashauri hizo, ni Kiteto, Rorya, Mbarali, Kyela, Jiji la Mbeya, Ileje, Rungwe, Mbozi, Chunya, Kwimba, Misungwi, Ukerewe, Tunduru, Manispaa ya Songea, Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, Maswa, Kahama, Meatu, Kishapu, Bukombe, Pangani, Mkinga, Kilindi, Korogwe na Handeni, Igunga, Sikonge, Nzega, Manispaa ya Tabora, Urambo na Uyui. Halmashauri 1 ya Simanjiro nayo ilirudia kutangaza lakini hakuna wataalam washauri waliojitokeza kutuma maombi ya kufanya kazi katika Halmashauri hiyo. Orodha fupi iliandaliwa kwa utaratibu maalum na kutumwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kuomba walioorodheshwa waandae mapendekezo yao. Orodha hiyo inapitiwa na Benki ya Dunia. Hatua iliyofikiwa na Halmashauri mbalimbali katika kupata wataalam washauri, hadi tarehe 17 Juni 2009, imeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 3 ya taarifa yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika Kauli ya Serikali ya mwezi Februari, ajira za Wahandisi 96 ambao waliajiriwa mwezi Novemba 2006 sasa imekamilika baada ya Halmashauri husika na Sekretarieti za Mikoa kukamilisha ajira za wahandisi 33 ambao walikuwa hawajapata ajira za kudumu ama kwa kuwapatia ajira za

kudumu au nao mikataba mipya. Wizara yangu imefanya tathmini ya wataalam wanaohitajika kukidhi mahitaji ya sekta kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Bado wahandisi na wataalam wengi wanahitajika. Mawasiliano na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yanaendelea ili kuhakikisha kuwa kila Halmashauri inakuwa na wahandisi na wataalam wengine wa kutosha kutekeleza majukumu ya sekta ya maji. Vilevile tunatayarisha orodha ya wahandisi, mafundi sadifu na mafundi mchundo ambao wako katika ofisi za mabonde ya maji ambao tutawahamishia Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jukumu kubwa la kuwapatia wananchi maji safi na salama, kutokana vilevile na ukubwa wa programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini, Serikali inaangalia uwezekano wa kuzifanya Idara za Maji katika kila Halmashauri ziweze kuwa Idara kamili ziongezewe ikama, vifaa na nyenzo ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa tija, ufanisi, kasi na viwango. Katika kuziwezesha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza majukumu yao, Wizara yangu imeagiza nyenzo za kufanyia kazi kwa ajili ya Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Nyenzo hizo ni pamoja na magari 123, pikipiki 252, kompyuta 111 na vifaa vya mawasiliano. Vitendea kazi hivyo vitakuwa vimepatikana na kusambazwa kwa Halmashauri na sekretarieti za Mikoa ifikapo Disemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali kuhusu maji na usafi wa mazingira vijijini, haiwezi kuwa kamili bila kuutaja mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama, hasa kuhusu jinsi vijiji vya Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Shinyanga vitakavyofaidika. Kupitia mradi huu, maji safi na salama yamefika kwenye matanki na magati ya kuchotea maji yamejengwa kwenye vijiji sita vya Wilaya ya Misungwi, vijiji 12 vya Wilaya ya Kahama, vijiji 20 Wilaya ya Shinyanga na tanki la Mhalo litakalohudumia vijiji 16 tarafa ya Mwamashimba Wilaya ya Kwimba. Vijiji 16 katika Wilaya ya Kwimba vilivyokuwa katika mradi wa zamani wa Mwamashimba, Serikali itafanya usanifu mpya wa mradi huo na ujenzi wa miundombinu utaanza mara baada ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuuzindua mradi huu mkubwa na wa kihistoria na kutenga siku mbili za ratiba yake iliyo ngumu kuutembelea mradi na kuukagua na kutoa maelekezo kuhusu umuhimu wa miradi ya maji kuwa endelevu. Nawashukuru Wakuu wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga kwa kufanikisha uzinduzi wa mradi huu. Namshukuru tena Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuthubutu kuanzisha mradi huo. Narudia tena, namshukuru tena Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuthubutu kuanzisha mradi huo na kushiriki katika uzinduzi wake. Nawashukuru Mawaziri wa Maji walionitangulia, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuliwakilisha Bunge lako Tukufu katika uzinduzi wa kihistoria tarehe 30 Mei, 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Serikali inapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini inayoendelea kutekelezwa kwa ufanisi unaridhisha. Changamoto mbalimbali ni pamoja na kukosekana

kwa wataalamu wenye sifa na uzoefu unaikidhi utekelezaji wa programu katika maeneo kadhaa ya Halmashauri zetu. Kati ya Juni 2007 na Juni 2010, kama nilivyosema, Serikali itakuwa imetumia jumla ya shilingi bilioni 85.3 kutoka katika mfuko maalum wa utekelezaji wa maendeleo ya sekta ya maji, yaani *water basket fund.* Shilingi bilioni 123.4 zaidi zimetumika na Serikali, wafadhili na taasisi nyingine katika kutekeleza programu nje ya mfuko wa maji. Napenda kusisitiza tena kwamba fedha za mfuko wa maji zitaendelea kutolewa kulingana na jinsi taarifa za utekelezaji wa miradi na zile za matumizi ya fedha kila robo mwaka zitakavyokuwa zinawakilishwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kusaidiana na Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kukamilisha utaratibu wa kupata wataalamu washauri na kusimamia utekelezaji wa programu kwa ufanisi ili kukidhi dhana ya kuwa na miradi endelevu. Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa zinawajibika katika kusimamia kikamilifu wataalamu washauri hao katika kuainisha vyanzo vya maji, upimaji na usanifu wa miradi katika kuandaa makabrasha ya zabuni za ujenzi ili miradi iweze kuanza kutekelezwa mapema iwezekanavyo. Kwa zile Halmashauri 38 ambazo zimepata ridhaa na nyingine zimesaini mikataba baina yake na wataalamu washauri, ni matumamini yangu kwamba ujenzi wa miradi katika Halmashauri hizo utaanza mapema iwezekanavyo katika mwaka wa fedha 2009/2010. Kauli hii ina majedwali manne, ikiwa ni pamoja na mgawo wa fedha kwa kila Halmashauri kuanzia mwezi Juni 2007 hadi mwezi Mei 2009. Kwa ukamilifu na ili kuweka rekodi sawa, naomba majedwali yasomeke katika *Hansard* kama sehemu ya kauli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, wananchi, taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali, madhehebu ya dini, washirika wetu wa maendeleo na wadau wote wa sekta ya maji kwa kuungana na Serikali katika juhudi zake za kuwapatia wananchi maji safi, salama na ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Maji ni Uhai, Usafi wa Mazingira ni Utu; kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, ahsante kwa kauli yako ambayo inaonekana imelifurahisha sana Bunge. Sasa tunaendelea, Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010*
*– Ofisi ya Waziri Mkuu)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, labda nitoe maelezo machache. Kwanza, namna ambavyo orodha ya wachangiaji imeandaliwa; orodha imeandaliwa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo. Kwanza kuna Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuchangia kwenye hotuba ya Bajeti, hawa wamepewa kipaumbele,

halafu kuna idadi ya Wabunge ambao wameshachangia kimkoa, pia limetizamwa hilo. Vilevile uwiano wa Wabunge wa Majimbo, vyama vya Siasa, Viti Maalum na pande za muungano.

Kwa bahati mbaya, jana baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliondolewa kwa kigezo kwamba wamechangia kwenye hotuba ya bajeti. Kumbukumbu zinaonesha kwamba walichangia kwenye Muswada wa Fedha na sio bajeti. Hivyo tumekubaliana kwamba tuwarudishe kwenye nafasi walizokuwa wamepangiwa awali ili wapate nafasi na haki yao ya kuchangia hotuba. Kwa hiyo, orodha tuliyonayo itabakia kama ilivyo sasa hivi na tutazingatia kama hivyo ambavyo nimekwisha kutoa tangazo na kueleza. Kwa kuanza leo hii niwataje watu wanne ambao watachangia, kwanza kabisa atachangia Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke, halafu na Mheshimiwa Devota Likokola ajiandae. Mheshimiwa Jenista Mhagama, tafadhali.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peramiho, kwa kuweza kutufikisha siku hii ya leo. Naomba tu niwahakikishie wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho, nitaendelea kuwa mtumishi wao mwema na muaminifu nikiwawakilisha katika masuala mbalimbali yatakayowaletea maendeleo wao kama wananchi wa Jimbo la Peramiho, lakini vilevile nitashirikiana na Wabunge wenzangu ili kusaidiana kuijenga nchi yetu ya Tanzania. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe shukrani zangu za dhati sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima, kwa jinsi anavyojitahidi sana yeye mwenyewe binafsi kufanya kazi kubwa ya kuijenga nchi yetu kwa nafasi kubwa aliyopewa na dhamana hii kama Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Mtoto wa Mkulima, ninakupongeza wewe pamoja na Mawaziri wote walioko katika Wizara zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa iliyofanywa ndani ya Jimbo langu la Peramiho. Daraja linalounganisha Tanzania na Msumbiji kupitia Jimbo la Peramiho, Kijiji cha Mkenda, limekamilika na pale sasa tuna *opportunity* kubwa sana ya biashara katika eneo hilo, shukrani kubwa kwa Serikali yangu. Madaraja ya miaka 20 ya kutoka Ndongosi kwenda Nambendo yamekamilika, barabara ya Wino – Ifinga imekamilika, mahali ambako wananchi wametembea kwa miguu kwa takribani miaka 20, sasa magari yanaweza kufika. Lakini naishukuru Serikali, barabara iliyokuwa kero kubwa inayounganisha Namtumbo na Songea Vijijini, Kijiji cha Matimila, nayo imeingia kwenye mpango na inakwenda vizuri. Umeme wa Peramiho baada ya kupambana sana na Waziri wa Nishati mwaka jana, ninaomba kukupa taarifa sasa umeme utawaka mwaka huu na kazi inaendelea kwa nguvu na spidi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kujenga shule za sekondari, tumeweza kufungua *SACCOS* za kutosha na mwaka huu tunafungua shule za sekondari za kidato cha tano na sita mbili, mwaka jana tulishafungua moja. Kiujumla niseme kwamba

mambo yanakwenda, naishukuru sana Serikali yetu kwa maendeleo hayo makubwa kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho na tunaomba kwamba shughuli hiyo iendelee hivyo hivyo na niendelee kusema kabisa kwamba wananchi wa Jimbo la Peramiho wanaendelea kuwa na imani na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye kilimo kwanza, ninaipongeza kabisa Serikali kwa azma ya kuweka kilimo kama ajenda ya kwanza ya maendeleo katika nchi yetu. Ingawa kwenye vipaumbele vya bajeti, kilimo wamepewa fedha kama Wizara ya nne, lakini mimi niseme kwamba si neno. Suala la mbolea ya ruzuku tumelipokea vizuri na hasa kwenye Jimbo la Peramiho. Ninamshukuru mtoto wa mkulima, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuja Jimbo la Peramiho na alitembelea kituo na Kijiji cha Matimila cha mfano katika uzalisahaji wa mbegu bora na mfano wa utumiaji wa mbolea katika kuzalisha mahindi. Kwa niaba ya Jimbo zima la Peramiho, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulijionea maendeleo makubwa na ulimpongeza Afisa kilimo wa Kata kwa kumpa shilingi laki tatu na umemuahidi kumpa u-*DC* atakaposoma na kupata elimu ya kutosha. Ulifurahishwa sana na kazi kubwa iliyofanyika.

Kwa niaba yake, nakushukuru, shilingi laki tatu amezipokea, anasubiri u-*DC* uliomuahidi na yeye yuko tayari kuupokea mara utakapokuwa tayari kumtunuku. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninachotaka kusema kwa niaba ya Jimbo zima la Peramiho, ni kwamba wanachosubiri ni kupata mbolea kwa wakati, zana bora za kufanyia kazi na mbolea hiyo iwe katika bei zinazowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudi katika hoja nyingine ya msingi kabisa, haya yote yataweza kufanikiwa vizuri kama eneo la Wataalamu wa Ugani, litapewa kipaumbele na watathaminiwa kwenye kazi zao. Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisiti kukuambia kwamba, bado nina hofu kubwa kwenye Wizara yetu ya Utumishi kama haitakuwa makini kuangalia na kutoa kipaumbele katika kusimamia suala zima la ajira na maslahi ya watumishi wa umma katika nchi hii ya Tanzania, masuala yote ya elimu, afya na kila kitu hayatakuwa na msingi, hapo ndipo mahali tunapotakiwa kujipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa na leo labda niseme, nilisema mwaka 2007, nilisema mwaka 2008, leo narudia kusema kwa mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka 2007, nimekuwa na kero kubwa sana ya baadhi ya hao watumishi ninaosema kwamba ni lazima wapewe kipaumbele, waangaliwe, ili wasaidie kukimbiza maendeleo hayo kwa kasi kubwa ndani ya Jimbo la Peramiho na nchi nzima ya Tanzania, lakini Wizara ya Utumishi imeniangusha. Niseme nina uchungu mkubwa, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, yupo hapa ndani anaelewa na nimeshazungumza naye mara nyingi lakini ameonyesha kwamba usikivu kwake ni kitu ambacho hakiko karibu sana na utaratibu wake wa kutenda kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hiyo haileti picha nzuri kwenye serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, nina ushahidi wa kutosha. Haya makaratasi hapa, yanadhihirisha mawasiliano yangu kupitia Halmashauri yangu na Wizara ya Utumishi, ili kuondoa kero za wataalamu na watumishi ambao wangeweza

kutusaidia sana katika maeneo yetu, hayana majibu mpaka leo. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye bajeti mwaka huu, Wizara hii ya Utumishi, tumemtengea Waziri huyu fedha za kwenda kutembea ndani ya nchi; mafuta peke yake, tumempa shilingi karibu milioni 300, lakini kama tunampa mafuta ya milioni 300 akatembea kuangalia matatizo ya wananchi haya tu tuliyomletea bado mpaka leo miaka mitatu hajayatekeleza, je, fedha hiyo kweli itasaidia kwenda kutatua kero za watumishi na *extension officers* katika nchi yetu ya Tanzania? Hatutakwenda mbele Mheshimiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *allowances,* Waziri huyu pia ana mafungu amejitengea kwa ajili ya *allowances* ya kufanya kazi kwa niaba ya Watanzania lakini inanisikitisha haya tu ambayo mimi nimemplekea pale Ofisini hajayafanyia kazi, je, hayo ya watumishi wasiokuwa hata na uwezo wa kufikisha matatizo yao huko, yatafanyiwa kazi na nani? Inasikitisha sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao watumishi 12 wengine wana takribani miaka 20, nimemuandikia ili Mheshimiwa Waziri Mkuu, yule mtumishi mmoja uliyempa sifa na kumpa shilingi laki tatu na wale wengine ambao wanafanya kazi kama yeye, waweze kufanya kazi zao vizuri. Wamelalamika kutokuingizwa kwenye *pay roll* mwingine kwa takribani miaka 20. Chanzo cha tatizo hilo ni hao watumishi ambao waliajiriwa toka mwaka 1980 na 2001 kutokuingizwa kwenye *pay roll* bila sababu za msingi na kueleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari hii anaijua muda mrefu. Ofisi ya Waziri Mkuu, iliandika barua tarehe 22 mwezi wa April, ikisema Ofisi ya Waziri Mkuu, imeandika barua tarehe hiyo kwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma ikiomba waangalie uwezekano wa kuwaingiza kwenye *pay roll* ya Serikali watumishi hawa, lakini hata barua kutoka kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, haitekelezwi! Ninaungana na Wabunge wenzangu kusema kwamba ugonjwa wa kutokutekeleza majukumu kwenye Serikali hii, hautatufikisha kwenye maendeleo ndani ya nchi yetu ya Tanzania, inasikitisha sana. Leo hii tunaposema kwamba mtu atengewe fedha *traveling in country,* kutoka milioni 95 mpaka milioni 202, anakwenda ku-*travel* kufanya nini kama majukumu haya yanayofika Ofisini kwake hayatekelezwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisikitisha kwenye *development budget* hapa unaona kabisa kwenye masuala ya *Management Service Division* kwenye Wizara, kuna takribani shilingi bilioni moja, sasa hizi fedha zinatengwa za nini kama hawa watumishi hawapatiwi haki zao? Ni nani atasimamia maendeleo ya wananchi wa Tanzania kama watumishi hawapewi haki na hawaangaliwi kwenye nchi hii? Ninachotaka kukuambia, ajenda hii ninayoiongea, inawahusu Wabunge takribani 49; nimefanya *research,* Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Hapa kuna Halmashauri karibu 49 zikiwemo za Singida mpaka huko Iramba, kwa Mheshimiwa Job Ndugai, hapa wapo karibu sijui nane na kwingineko kwingi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba leo nazungumza mara ya mwisho. Utumishi wa Umma ndio nguzo pekee ya kuleta maendeleo katika nchi yetu na kama watumishi wa umma hautatambuliwa, haya yote tunayoyapanga ya kilimo kwanza,

elimu kwanza, afya kwanza na kadha wa kadha, hayatakuwa na tija kwenye nchi yetu. Suala hili lisiposhughulikiwa, nitawaomba nguvu Wabunge wenzangu 49, nije na hoja binafsi Bunge lijalo ili tuweze kumaliza kero hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali, ajenda hii ya kuleta maendeleo kwa wananchi na hasa vijijini kupitia kwenye sekta ya kilimo ni muafaka kabisa. Ninaomba nichukue nafasi hii nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilipofanya ziara mwezi wa tano na wa sita kabla sijaja Bungeni, niliwaahidi wananchi wa Jimbo la Peramiho kwamba pamoja na maendeleo yote tuliyopata, maendeleo ya elimu na kila kitu, lakini ajenda ya kilimo Serikali yetu ni sikivu, italeta pembejeo kwa wakati, ninaomba kupitia kwako Mwenyekiti, nimuombe Waziri Mkuu, asimamie hilo ili mbolea ifike kwa wakati muafaka, ikichelewa haina maana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la matrekta, ni kweli Halmashauri zetu zimejipanga. Leo asubuhi nimemuuliza Naibu Waziri wa Kilimo, suala la kuimaraisha kilimo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Songea, eneo la kilimo cha Miwa. Ananijibu kwamba Serikali kazi yake ni kuwezesha mazingira lakini sio kupeleka viwanda wala nini! Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati mwingine majibu ya hawa Manaibu Mawaziri wawe wanayatafakari upya, unapotengeneza mazingira maana yake ni wewe kusaidiana na wananchi kuhakikisha kile ambacho kina tija kwa wananchi na Serikali yao na nchi nzima kinafanikiwa. Huwezi kusimama hapa na ukasema kwamba hiyo sio kazi ya Serikali, Serikali kazi yake ni nini na imewekwa na nani? Kama sio wajibu wake kuwasimamia wananchi, ina kazi gani sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali yetu, mapinduzi ya viwanda katika nchi za Ulaya, ndio yaliyopelekea nchi za Ulaya kuwa na maendeleo makubwa na walianza na *cortage industries*, viwanda vidogo vidogo. Ninasoma hapa kitabu cha *development* kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, hizo pesa anazoniambia Mheshimiwa Naibu Waziri, ndio eti nikashughulike nazo hizo kuendeleza kilimo, hebu aniambie ni shilingi ngapi hizo zitakazoweza kama sio kuomba Serikali iongeze juhudi kwetu? Kitengo cha *research* kwenye *development* bajeti Wizara ya kilimo, hakijapatiwa hata shilingi moja, sasa tunafanya nini? Waziri Mkuu anakumbuka, kama hatutafanya *research* na kupata mbegu bora ya mahindi, hakuna uzalishaji wenye tija. Kama hatuna *research* na kupata mbegu bora ya kahawa, ya pamba, ya tumbaku na kadhalika hakuna kilimo chenye tija. Leo tuna mtikisiko wa uchumi wa kidunia, huu mtikisiko umemtikisa kila mtu, Tanzania tunaweza kuchukua *opportunity* ya mtikisiko huo kama tutaboresha kilimo, lakini kama hatutaweza kuboresha kilimo, hatuna maana kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kupitia kwako, ujumbe huu utamfikia Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, atatusaidia kuona tunafanya nini katika kuwa na usimamizi imara na thabiti. Nchi yetu sisi tunaweza kila kitu ili mradi tu tuamue, tuwe na nia moja na ninakuhakikishia kwa miaka hii mitatu niliyokaa kwenye Jimbo la Peramiho, nimegundua wananchi wale wako imara kabisa, wanaweza kuanzisha viwanda, wanaweza kulima na wanaweza kufanya kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikuambie ili kwamba uwe ni shahidi, nchi hii pia inalishwa kwa kiasi kikubwa na chakula kinachozalishwa na wananchi wa Jimbo la Peramiho. Huwaambii kwenda shamba, wanakwenda wenyewe, kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kuona inafanya nini, inawasaidiaje wananchi hawa kwa nguvu zote, pale wanapojipanga wenyewe wasaidiwe na Serikali yetu. Nirudie kusema, kwa kweli kama wananchi wanajitolea kujiletea maendeleo, ni wajibu wa Serikali yetu kuingiza mkono na kusaidiana nao ili waweze kupata maendeleo wanayoyataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusisitiza ajenda ya kwanza. Naunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jana nilipopata habari sichangii, niliumia lakini nashukuru sana Ofisi yetu sikivu na imeniweka, nakushukuru sana.

Kabla sijaanza kuishukuru Serikali, leo asubuhi nimepigiwa simu ninaulizwa, je, Madiwani Viti Maalum hawaruhusiwi kugombea Umakamu Mwenyekiti? Kule Bagamoyo wameambiwa hawaruhusiwi, kwa hiyo, ninaomba jibu la Waziri aki-*wind up* kwa sababu tulishakuwa na Madiwani Viti maalum ambao walipata Umakamu, kwa mfano Mkuranga, sasa naomba jibu lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba niungane na wenzangu kuishukuru Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya, kwa bahati mbaya tu kile kisungura ni kidogo, kwa hiyo, tunaking’anga’ania kilete hapa, kilete kule, kilete kule lakini kwa kweli, ninaomba niishukuru Serikali na hasa Wizara ya Maji. Kero kubwa ya kwanza katika Jimbo langu ni maji na ilani inakubali kwamba kero kubwa ni maji. Nashukuru sana wakati Makamu wa Rais alipokuja kutembelea Wilaya ya Kibaha, alitamka tunaanza mradi wa maji na hivi sasa ninavyokwambia tayari kuna mradi wa maji wa uboreshaji wa huduma ya maji safi kati ya Kiluvya na Mlandizi. Maeneo ambayo tayari mitaro inachimbwa ni Maili Moja, Kata ya Tumbi, Picha ya Ndege, Kwa Mathias, Nyumbu Msangani, Mwendapole, hivi sasa pia tumeanza kuona hata Kata ya Pangani mwanzoni, Visugusugu, Miembe Saba, Visiga, hata sehemu ya Kisarawe, Mzenga, Vikuruti na Mlandizi. Naomba niwashukuru sana, nawaambia wananchi wangu, wale Wakandarasi wanasema tafadhali ombeni maji mita 20, mkishaona mtaro unapita, wanawachimbia bure, zilizobaki wanaendelea. Naomba niishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Maji, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Waziri wa Maji, tena nakupigia magoti sana, kuna mtaa wangu unaitwa Vikawe. Vikawe hawawezi kupata maji kupitia Ruvu Juu, ni lazima wapate maji kupitia Ruvu Chini. Visima kule maji hayatoki, sasa hivi ndoo moja ya maji ni shilingi 500, maji haya mkiyaona mtu wa kawaida huyanywi. Wizara hii ya Maji imefanya juhudi imepeleka mwaka jana milioni 80 ili Vikawe ipate maji kupitia *quick wing*, kwa bahati mbaya watendaji wameisaliti Vikawe. Wakasema milioni 80 kwa sababu huu mradi ni lazima utoke Ruvu Chini, inatakiwa iongezewe pesa na hela hii haitoshi na kwa sababu haitoshi na mwakani, yaani mwaka wa 2008/2009, mtapata pesa nyingi kwa hiyo, hela hii tunaipeleka kwenye Kata zingine na mkichelewa

hela hii itaondoka. Cha kusikitisha mpaka unaingia mwaka 2008/2009, pesa ile ilikuwa haijatumika na ilipofika Vikawe haikupewa hela imepewa milioni 40. Nikaomba basi changanyeni milioni 40 na milioni 80, itakuwa ni milioni 120, tutaomba na kwingine lakini Halmashauri haikufanya hivyo. Hivi sasa nakushukuru kweli kabisa, tumekusumbua, tumekutafutia wataalamu, tumekwenda na ninaomba niishukuru *TASAF* imeomba hela hizi na ninaomba zisimamieni maana hii Kata ya Vikawe inasikitisha. Mkienda kuona yale maji, ninashukuru nimehangaika mimi, Waziri unashuhudia na bahati nzuri pale nilipokuwa nimezidiwa nikamwambia Diwani wangu ambaye ndiye Mwenyekiti, anahangaika, naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa miradi mbalimbali iliyoletwa Wilaya ya Kibaha. Nikiitaja ni mingi muda utakwisha, lakini ninashukuru sana. Lakini ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri, nikiinuka nikisema jambo katika Bunge ni mtu mzima, Mbunge Mzoefu, huwa sisemi uwongo. Nilipokulalamikia suala la Sofu, lilifikia hatua karibu tusielewane mimi na wewe lakini sasa wewe mwenyewe umethibitisha, Serikali imesimamia lakini kwa msukumo wa Chama changu cha Mapinduzi Mkoa, iliwaambia Chama cha Mapinduzi Wilaya angalieni kero hii, haitekelezwi vizuri na watendaji. Walipoisimamia, naomba nishukuru kero ile imekwisha, nakushukuru sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru, baada ya mimi kuwa mkorofi katika Jimbo langu kuhakikisha bajeti ni shirikishi kwamba ni lazima ishirikishe mitaa yangu, nawaambieni ndugu zangu Wabunge, bajeti hii ya mwaka huu imeshirikisha kila mtaa, manaa yake ilibidi nitumie hela yangu kusafirisha viongozi, kuwapa chakula katika kila Kata, kuwaeleza umuhimu wa bajeti shirikishi. Wameshiriki kitu tu kidogo kimekorofisha ni kwamba hii keki ndogo, sasa kuna mengine ninawaomba wananchi wangu tuvumulie tutapewa. Hivyo naomba nishukuru na mimi nilikuwa mfano kwa Wabunge waliokuja wa *IPU* kuonesha Wabunge tunaweza, naomba nishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru *TASAF*, sisi shule kila kata tunayo na ilipofikia hali ya uchumi ya Jimboni kwangu kuwa ngumu, nilisimamia, nikabembeleza, *TASAF* iliweka hela Kibaha Vijijini na sisi tukawaomba wananchi wakakubali, sasa hivi tuna tatizo dogo tu, kuna shule moja ya sekondari ambayo kwa bahati mbaya kuna darasa moja wanakaa chini lakini tumesema tutalishughulikia, hili ni tatizo letu sio la kwenu, naomba nikushukuru sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana hospitali ya Tumbi, kwa bajeti iliyopangwa mwaka huu, nashukuru sana hospitali ile, nimesema asilimia 30 ya *accident* za Tanzania zinatokea pale, naomba nawashukuru sana. Naomba tu tushirikiane, nitamuomba Waziri wa Afya, wale wanafunzi kutoka Muhimbili wakitaka kazi waje kule, kama Kairuki ambao wakita *field work* wanakuja Tumbi. Tunawashukuru sana na ndugu zangu Tumbi ni hospitali nzuri kimbilio la watu, karibuni sana, naomba niwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye matatizo, mimi nilikuwa nalalamika sana, Wilaya ya Kibaha Mjini ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani, haishughulikiwi. Nilikuwa nailalamikia Serikali lakini naomba niwaambieni wenye matatizo ni watendaji, watendaji wa Wilaya ya Kibaha Mjini, unasema Rais kaagiza barabara hata pale mjini ambako kumepimwa watendaji hawaupangi mji, kinachobaki watendaji wa ardhi na wengi kazi yao kuvamia ardhi utafikiri nyani kaoni ndizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa hapa masuala ya vituo vya mafuta, dada yangu Waziri naomba nikwambie kuna vituo sisi kama Madiwani hatujatoa kibali, lakini nilivyofanya uchunguzi vina vibali wanasema Madiwani wametoa vibali, naomba hili ulifuatilie linatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda kutizama pale Maili Moja *stand*, ile *stand* inatoa pesa nyingi lakini nikiomba tufanye *value for money audit*, kuna mmoja akaweka shingo upande, Madiwani mtusamehe hatuweki. Naomba *value for money audit* pale Mail Moja, ile *stand* ina hela nyingi lakini zinachukuliwa, kama mlivyofanya Mkuranga, naomba mfanye na Maili Moja, naomba hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi lakini naomba niseme masikitiko makubwa, Mbunge anahangaika kutafuta pesa kusaidia Serikali, nimezungumza na watu wa *NSSF*, tukae tujadili tupange iwe *stand* kubwa itakayowasaidia wananchi wa Kibaha. Huwezi kuniambia lile eneo ambalo tumelipanga, Maafisa Ardhi wamelihujumu, wameweka vituo vingine mpaka sasa hivi kuna mvutano wameshakula, baadhi ya watendaji wamekula milioni 20 rushwa, baada ya kukaa siri ikafichuka, yule aliyetoa rushwa milioni 20 mwingine sijui katoa milioni 28 ni vurugu tupu. Naomba utuondolee Maafisa Ardhi waliokaa zamani. *Town planner* ni mtu mzuri sana, amenielewa, ananisikia, ameanza kuweka michoro lakini wanamrudisha nyuma na dada yangu Mkurugenzi sijui niseme mpole sana, sijui nimseme ana tatizo gani, maana hata ukimwambia hafuatilii mpaka leo anaishi Dar es Salaam. Leo nalisema hili, watu wote wamesema namtetea lakini leo lazima niliseme anaturudisha nyuma kwa kutoakusimamia watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikitika na nirudie na ninakupigia magoti Waziri Mkuu, Watendaji wenu wametusaliti Kibaha Mjini na wananchi wa Kibaha Mjini lisikilizeni hili ninalolisema, kwamba sisi kwa kutumia nguvu za Mbunge, pesa zake kuzunguka kushawishi watu tumekubaliana maeneo gani yanastahili kuwa mitaa lakini Maafisa wako wametuangusha, ndiyo maana leo nimemsema Mkurugenzi wangu ingawa ninampenda. Hata kama ni Maafisa wake, Afisa Utumishi ndiyo aliyefanya hivyo lakini yeye ndiyo msimamizi mkuu, yeye kachelewesha taarifa niliyoipata juzi, kwamba ile shida yote wananchi waliokaa mikutano yote eti hatupewi tena mitaa kwa sababu kachelewesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubembeleza Waziri Mkuu, nakupigia magoti, chonde kabisa wananchi hawa mtakuwa mmewanyanyasa kwa kiwango kikubwa, yaliyosababishwa na watumishi wenu. Ninaomba mtumishi akihamishwa kusiwe na sababu yoyote, mimi naambiwa kuna mtumishi anasoma, mbona sijaona waliohamishwa,

kaimu sijamuona, nimeuliza wenzangu kuna Kaimu wanasema hakuna. Mtumishi kaenda Mkuranga siku moja siku ya pili karudishwa anasomeshwa, mbona hatujamuona kaimu wakati anasoma? Naomba mtumishi akiondolewa tena mtumishi huyo ana kero, mimi si mwongo, si mnafiki kwa sababu dini yangu inakataa unafiki, ana kero, mhamishe wanaojidai wana vidonda vya tumbo, wanaojidai sijui nini, wapelekeni Dar es Salaam basi wakakae karibu na Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haraka haraka, ahadi za Rais hazitekelezeki, Rais mwenyewe anashangaa, akasema Kibaha kimji gani kwa nini ahadi hazitekelezwe, kumbe wasaliti ni maafisa wetu pale Kibaha, kwanza walijibu jibu la uwongo eti sisi tumetenga ardhi ya viwanda mahali kwingine.

Mheshiwa Mwenyekiti, nakushukuru na niunga mkono hoja hii kwa asilimia mia, naomba Waziri lile la mitaa nisaidie sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri, yenye kutoa mwelekeo. Nampongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Mwanri, kwa ushirikiano wao mzuri ambao wanaufanya katika Wizara yao ya TAMISEMI. Lakini pia niwapongeze Makatibu Wakuu ambao nao ni watendaji wakubwa katika ofisi ya Waziri Mkuu lakini pia katika ofisi ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kazi kubwa wanayoifanya kuweza kuendesha gurudumu hili la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kuukumbuka Mkoa wa Kigoma. Lakini pia, nimshukuru na Waziri Mkuu naye kwa kuungana na Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha Mkoa wa Kigoma unapewa kipaumbele katika Mikoa iliyoko pembezoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa sana, naomba nishukukuru kwa kazi kubwa iliyofanyika tarehe 12 mwezi huu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifika Kigoma kwenda kuzindua barabara ya Mwandiga - Mwanyovu na Kigoma - Kidawe, hii yote ni juhudi ya Serikali ya Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wa Kigoma tunaimani sana na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, tunaona juhudi ambazo zinafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuweza kuhakikisha Mkoa wetu wa Kigoma unaunganishwa na Mikoa mingine ya nchi yetu ya Tanzania. Kwa hatua hii, ninaamini sasa Kigoma tunaanza safari ya kwenda kwenye maendeleo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nikushukuru na salamu zangu hizi uzifikishe kwa Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuukumbuka Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, naomba nishukuru Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya kuhakikisha inajikita katika kilimo na kuweza kuunganisha Mkoa wa

Kigoma katika Mikoa sita ambayo imeteuliwa kuhakikisha inazalisha chakula na kusambazwa katika nchi hii. Naipongeza sana Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amejikita sana katika azma hii ya kilimo kwanza na juhudi zake tunaziona na tangu ameteuliwa kuwa Waziri Mkuu, ameshafika katika Mkoa wetu safari tatu na ameahidi kurudi mara baada ya bajeti. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa nguvu zake na nguvu zetu na sisi hatutamuaibisha, tutaungana naye kuweza kuhakikisha Mkoa wetu unasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila, nisipomshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mheshimiwa Simbakalia, watendaji wa Mkoa wa Kigoma, Wakuu wa Wilaya zote tatu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha Mkoa wa Kigoma unatoka hapa ulipo na kwenda kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkuu wetu wa Mkoa, anafanya kazi kubwa sana, ni mtu anayejituma, ni mtu anayependa kushauri na kutoa maelekezo pale inapobidi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali isituondolee Mkuu wa Mkoa mpaka hapo tutakapokuwa tumeona sasa tunaenda wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma, ni Mkoa uliojaliwa kuwa na rutuba ya kutosha, ardhi ya kutosha, ina mito mikubwa ambayo inachangia kufanya Mkoa ule uweze kuwa Mkoa unaopendeza kwa hali ya nchi ambayo inatakiwa kuzalisha kilimo kama sehemu nyingine. Kwa hiyo, ninaomba fursa hii tuliyopewa, Serikali iweze kutuunga mkono kwa kuhakikisha inatutia moyo sisi wananchi wa Kigoma, kuhakikisha tunaondoka hapa tulipo, kusonga mbele kwa kutumia vipaumbele ambavyo wao Serikali watakuwa wametupatia. Tunaomba tupewe pembejeo wakati muafaka ili tuweze kuzitumia muda utakapokuwa umewadia. Wenzangu wameshasema, pembejeo ya mbolea mara nyingi huwa inachelewa kuwafikia wakulima na ikichelewa kuwafikia wakulima matokeo yake wanalima na wanakosa mbolea wanaanza kupanda bila mbolea, nguvu zao zinapotea bure. Naomba Serikali ilizingatie hili kuhakikisha mbolea inafikishwa Kigoma mapema iwezekanavyo ili wananchi waweze kuitumia kuzalisha chakula hatimaye kukuza uchumi wa Mkoa wetu lakini pia na uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna mabonde mazuri ya Mto Malagalasi, mto Lugusye na Mto Lwiche, tunaomba Serikali iweze kutusaidia kuhakikisha inatuongezea pesa kwa ajili ya kuweza kutumia mabode hayo ili tuweze kuzalisha vilevile kwa kilimo cha umwagiliaji. Bahati nzuri tunaye Eng. Chiza, mara nyingi amekuwa ni mshauri wetu katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itupe kipaumbele katika kuhakikisha inatuletea vitendea kazi kwa ajili ya kutumia mabode tuliyonayo ili tuweze kuzalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayataweza kwenda bila kuwa na barabara inayotuunganisha, pamoja na shukrani nilizozitoa kwa barabara ya Mwanyovu - Mwadiga, Kigoma - Kidawe, kuna barabara ile ya Kigoma, Kasulu, Kibondo mpaka Nyakanazi, barabara ile ndiyo inayounganisha Wilaya zetu za Mkoa wa Kigoma. Kwa hiyo, nayo naomba Serikali ifanye mpango mkakati kuharakisha kuitengeneza barabara ile. Barabara ile itatusaidia kusafirisha mbolea kuitoa Makao Makuu ya Mkoa kusambaza

katika Wilaya zetu za Mkoa wa Kigoma. Najua Serikali yetu ni sikivu itatusaidia kufanya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile bado tunahitaji miundombinu ya umeme, kwa sababu tukiwa na miundombinu ya umeme, wazalishaji watakuja katika Mkoa wetu kuwekeza. Bila umeme na barabara, hatuwezi kupata wawekezaji watakaokuja Kigoma kuja kuwekeza, lakini tukipata vitu hivyo, wawekezaji watakuja kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu tuna mazao ya michikichi ambalo linahitajika katika Mkoa wetu, nchi yetu lakini hata nchi jirani. Kwa hiyo, Serikali ikituunga mkono katika yote haya, tutaweza kukuza uchumi wetu lakini pia tutaweza kuchangia pato la taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani hawatoshi, ni kilio kikubwa cha nchi nzima, tunaomba Serikali iongeze kasi kuhakikisha maafisa hawa wanapatikana na wakipatikana wanapelekwa vijijini, wasikae mjini na wanapofika katika Wilaya zetu wasikae ofisini waende vijijini maana ndiko waliko wananchi. Wananchi wengi hawana elimu ya kutosha, wanahitaji elimu hiyo ili hatimaye waweze kuitumia kuzalisha mazao katika mashamba yao. Kwa hiyo, naomba Serikali nayo ilishughulikie suala hilo ili kuhakikisha Maafisa Ugani wanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja akaona na kikundi kile cha wale Wagani Kazi waliokuwa wanajifunza. Wale wakipewa mafunzo, wakiondoka mahali pale, wataenda vijijni kwenda kufundisha kama walivyofundishwa, hata katika Mkoa wanaweza wakachagua ni sehemu gani Wagani Kazi waende kufundishwa hatimaye wakitoka pale na wao waende kupeleka elimu katika vijijini vinavyowazunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshwaji, naomba wananchi wawezeshwe kwa kutumia MKURABITA watumie hati miliki za kimila ili waweze kukopesheka kwa kukopa mikopo kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, naomba hili nalo Serikali ihakikishe MKURABITA unatumika kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu. Wananchi wengi wamekata tamaa hasa unapowaambia kwamba wanaweza wakakopeshwa wakaenda kuzalisha katika kilimo, wakati mwingine wanakuuliza Mheshimiwa sisi tutakopa tutalipa nini, naomba Serikali itusaidie kuhakikisha elimu inaenda vijijini kuwafundisha wananchi wetu ni jinsi gani wanavyoweza kukopeshwa na Serikali. Wakipewa elimu watajua na wataitumia elimu ile na watajua wafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *voucher* za ruzuku ya mbolea zilizotolewa kwa ajili ya wakulima wenye kipato kidogo, ninaomba *voucher* hizi, ninarudia kusema, naomba *voucher* hizi kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, zisimamiwe ipasavyo kwa sababu mwaka jana limetokea tatizo kubwa, mbolea zilizoenda kule wananchi wengi wamelalamika, nisipolisema humu ndani nitakuwa najidanganya mwenyewe. Mbolea hazikuweza kuwafikia wananchi kwa sababu wale viongozi walioko kule chini wanajilimbikizia wao wenyewe, wanaweza kwenda kuandika majina ya watu ambao hawapo. Viongozi wakubwa hawawezi kujua lakini huku chini ndiko kwenye matatizo, sisi tunalisema hilo kwa sababu wananchi wanatuletea taarifa sisi Wabunge. Unapoenda

Jimboni kutembelea Jimbo lako unakutana na matatizo ya namna hii, wanakwambia kabisa sisi hatuwezi kuchagua CCM, kwa sababu CCM haitujali, mbolea wameleta lakini waliofaidika ni watu wachache. Naomba hata wale mawakala waangaliwe, kwa sababu na wao ni binadamu inawezekana kabisa wanachukua mbolea ile hawaitoi ipasavyo wanaenda kujilimbikizia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hilo kwa sababu sisi tuko mpakani, wananchi wanaweza wasipate mbolea ikavushwa kwenda kuwasaidia wananchi walioko Burundi. Kwa hiyo, ninaomba kabisa kabisa, mbolea itakapopelekwa kwenye Wilaya zetu iweze kutolewa kwa wananchi kwa kutumia utaratibu unaoeleweka. Niliwahi kuongea na mtu mmoja, Afisa, nikamwambia nasikia wananchi wanalalamika kwamba mbolea iliyotolewa wao hawakupata, hebu niambie ilikuwaje? Akaniambia nimpe ushahidi. Sasa fikiria kiongozi ambaye ndiyo anayehusika, unampa taarifa yeye ndiyo anakuambia nipe ushahidi, nani amekwambia! Kwa hiyo, naomba viongozi wale wanaohusika kugawa mbolea hii ya ruzuku watende haki wasijilimbikizie mali wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu.

Awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, watu wote tumeona jinsi ambavyo anawajibika na anafanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, amefanya uwasilishaji mzuri sana kuanzia kwa Waziri wake Mama Celina Kombani, Naibu Waziri Mwanri, watendaji wote wa Serikali Kuu, lakini vilevile tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwashukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, yule aliyetoka Mama Monica Mbega, kwa kazi kubwa aliyoifanya. Mkoa wa Ruvuma katika uchumi tulikuwa wa tatu, kwa hiyo, hii yote inaonyesha kwamba kuna kazi kubwa imefanyika. Lakini tunamshukuru Mungu ametoka mama Monica Mbega, ameingia mama Ishengoma Daktari wa Kilimo. Tunafurahia na Mkoa wa Ruvuma unahistoria ya kuongozwa na viongozi wanawake, alianza mama Makinda akaupelekea Mkoa vizuri sana, akafuata Mheshimiwa Said Kalembo, lakini baadaye wakaona kwamba wanawake hawa ndiyo watapeleka Mkoa vizuri, wakamleta Mama Monica Mbega, sasa wamemleta mama Ishengoma, tunashukuru Waziri Mkuu, uzi ni huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa yote, lakini naomba nitoe mchango wangu ambao utakuwa katika maeneo makubwa manne, eneo la kwanza ni shukrani, eneo la pili ni maombi na eneo la tatu ni maoni na eneo la mwisholitakuwa ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninapenda kuishukuru Serikali, aliye na macho haambiwi tazama, watu wanaosoma ilani ya Chama cha Mapinduzi, wataona mambo yote Serikali imetekeleza, ukianzia kwenye elimu, madarasa yamejengwa na hapa napenda niipongeze sana kwa mabweni kwa watoto wa kike, tunaipongeza sana Serikali. Serikali imejitahidi, hostel Mkoa wa Ruvuma zimekuwa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye mambo ya afya, hospitali ya Mkoa wa Ruvuma imekarabatiwa vizuri na hospitali ya Tunduru inaendelea kukarabatiwa, lakini bado tunaendelea na mikakati na mipango ambayo tumejiwekea, napenda kuipongeza Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile masuala ya barabara, barabara za Manispaa ya Songea, sasa hivi ukifika utakuta ukarabati wa lami unaendelea, hongera sana Serikali, pesa zinafanya kazi na wananchi wanafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye uchumi jamani tuseme nini, wanawake wa nchi hii tumeanzishiwa Benki ya Wanawake, hongera sana Serikali. Katika hili ninapenda kupongeza Waheshimiwa Wabunge wanawake waliochangia hisa za mwanzo kabisa katika benki hii na Waheshimiwa Wabunge wanaume waliochangia, wale ambao bado hawajachangia, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wanaume mchangie ile ndiyo maendeleo ya nchi. Ukimwezesha mwanamke, umewezesha Taifa lakini vilevile kuna wananchi wengi tu ambao wanachangia katika ile benki ya wanawake Tanzania na mfano huu ameuonyesha mwenyewe Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ninaomba wote tuiunge mkono Benki hiyo kama ni uwezeshaji wa wananchi, uwewezeshaji wa wanawake basi kwa kuanzisha benki hii Serikali imepiga bao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, tunavyofanya kazi katika Mkoa wetu Ruvuma, wananchi wanatupa *support* kubwa sana Wabunge wao mimi nawashukuru sana hususani wanawake wa Mkoa wa Ruvuma, ninawashukuru na mwendelee na moyo huo bila kuwasahau Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Ruvuma, chini ya Ruvuma *Press Club* ambayo inaongozwa na Juma Nyumayo. Jana Mheshimiwa Mongella alisema kuna Waandishi wa Habari wachochezi, Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Ruvuma, wamekuwa makini katika kutangaza maendeleo yote yanayofanywa na Serikali yetu, hongereni Waandishi wetu wa Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi, ombi la kwanza, katika kijiji cha Lipinyapinya, Peramiho, kuna mzee anaitwa Peter Gama. Mzee huyu pamoja na wazee wenzake walipigana Vita ya Pili ya Dunia. Waliahidiwa pesa kutoka Serikali ya Uingereza, umri wao unazidi kuwa mkubwa, hofu ya kifo imewakaribia, wanaomba Serikali iwasaidie kabla mauti haijawakuta. Nimetumwa na wazee hawa, ninaomba tafadhali, alipokuwa Mheshimiwa Kapuya katika Wizara hii alihangaika sana lakini sasa hivi Mheshimiwa Mwinyi ni kila siku anapigiwa simu na Wazee hawa anajitahidi lakini ninaona hili linatakiwa uongeze nguvu Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, nyumba za Polisi wa Songea Mjini na ile ya Kituo cha Polisi zina hali mbaya. Nilimwomba Mheshimiwa Masha na ninamwomba atembelee Mkoa wa Ruvuma maana tumetangazwa kwamba ule mji wa Songea ni katika miji salama hii inatokana na wale Askari wanavyotusaidia katika ulinzi lakini nyumba zao kwa kweli zina hali mbaya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza katika hotuba yako umeweka masuala mazima ya hosteli, tuna matatizo makubwa katika Wilaya ya Tunduru, kwa watu wasioifahamu Wilaya ya Tunduru, moja ni Wilaya kubwa lakini mbili ina simba wengi. Kwa hiyo, watoto wanavyoenda shuleni ni hatari kubwa na ukiangalia pale kuna ile *Selous Game reserve*, kwa hiyo, tunaomba kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hayo yote ile bajeti ya hosteli kwa Tunduru, Namtumbo, utusaidie kwa kweli iongezee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la nne, ni juu ya fedha za umwagiliaji. Ulipokuwa unafanya ziara ya kilimo katika Mkoa wa Ruvuma, ulijionea mwenyewe bonde la Mto Ruvuma na ukaahidi pale na ulimsifia sana Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mwandosya, ukasema ni msikivu na atalitekeleza hili kwa haraka, tunaomba kukumbushia, Mheshimiwa Waziri Mkuu, usisahau ile kata ya Subira na kata ya Lizaboni, miundombinu ya umwagiliaji ikiwekwa pale tutapata chakula kwa wingi sana hususan zao zima la mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo maombi, wote kwa ujumla tufikirie sana Wilaya ya Mbinga. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wilaya Mbinga imekuwa ikiongoza kiuchumi karibu miaka yote na inasaidia sana pato la Taifa, lakini miundombinu ya Wilaya ya Mbinga hailingani na uchumi unaongizwa kwenye pato la taifa. Hata ile barabara ya kwenda Mbinga Mheshimiwa Waziri ulijonea mwenyewe na ulikatisha ziara kutokana na miundombinu mibovu iliyoko katika Wilaya ya Mbinga. Watu wengi wanaweza wakajifunza maendeleo endelevu katika Wiliaya ya Mbinga. Kwa hiyo, ninaomba wilaya yetu ya Mbinga isaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maombi hayo nina maoni, kwanza Mtwara *Corridor*. Wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, hawaelewi maana halisi ya Mtwara *Corridor* bila kuiona barabara ya kutoka Tunduru kwenda Songea kwa sababu ina hali mbaya, kila siku kwenye vitabu vya bajeti tumepewa ahadi zinaandikwa kuna pesa, ziko pesa za *MCC*, ziko za BADEA, ziko pesa za *Kuwait Fund* lakini hakuna utekelezaji kule. Kwa hiyo, sisi tunashindwa kabisa kuwajibu wananchi. Ninaomba umuagize Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, kabla hajatoka kwenye hiyo Wizara ya Miundombinu, ajitahidi wakati tunasibiri pesa za nje, atumie pesa za ndani akarabati maeneo korofi kwa kuweka hata lami ya viraka. Jamani Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukienda kule Chacha huwa tunaogopa kukupeleka kwa sababu ni hatari kwa hiyo ni vizuri Mheshimiwa Shukuru Kawambwa akakarabati kabla hatujakuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni juu ya *PPP*, umeizungumza vizuri katika hotuba yako lakini kwa nafasi hii napenda nimpongeze sana Dr. Matomora wa Kituo cha Kiuma Tunduru. Jamani kama kuna wale Watanzania waliowahi kuishi ughaibuni

wakarudi nchini wakaungana na Serikali katika kuleta maendeleo, Dr. Matomora ni mmojawapo. Serikali kwa kutambua mchango wake, ikamuomba ifanye *partnership* naye katika kujenga Chuo cha Ualimu. Mheshimiwa Waziri wa Elimu alikwenda kuzindua akaweka jiwe la msingi makubaliano yale mpaka leo hayajasainiwa, hakuna kinachoendelea, lile jiwe la msingi lilitaka kuibiwa, Dr. Matomora amelichukua ameliweka ndani. Tunaomba Serikali, tunafahamu matatizo ya Mkoa wa Ruvuma, Walimu hakuna, tumwezeshe Dr. Matomora ili tupate Walimu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie juu ya suala la zima la Kilimo kwanza. Katika Mkoa wa Ruvuma, ninaamini huna wasiwasi nao, idadi ya magunia yaliyorundikana katika ghala la Serikali uliyaona kwa hiyo kikubwa tunahitaji mbolea ifike mapema na vilevile elimu kwa wakulima wenyewe. Ukitaka kujifunza Mheshimiwa Waziri Mkuu mkulima akiwezeshwa anafanya vizuri sana, nenda kijiji cha Ugano kule Mbinga utamkuta Mama Chacha analima Kahawa kwa mafundisho aliyopata na TAKRI haiwezekani. nenda kijiji cha Lunyanyu Njombe, utamkuta Mama Lwela naye analima vizuri, anapanda vizuri kutokana na elimu aliyopata ya kilimo lakini vilevile nenda pale katika Chuo cha Wakulima cha Morogoro. Kwa hiyo, wale wote wanaonyesha namna nzuri ya kilimo pale Mkindo. Nina ushauri, ninaomba upange ziara ya Wataalamu wetu waende nchi ya Rwanda wakajifunze mambo yafuatayo; moja ni usafi wa mazingira. Mbili, rushwa. Tatu, usawa wa kijinsia na nne ni suala zima la *performance contract*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wataalamu wakijifunza hayo, wakirudi kukuletea ushauri hapa, nchi hii itakwenda motomoto. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakupongeza, ninakutia moyo na Watanzania tunaridhika na maendeleo yetu tusipojisifia wenyewe hakuna atakayetusifia. Tunafanya vizuri sana na kwa kweli tuendelee vizuri kila mtu nampa pongezi na tuendelee kushirikiana ili kusudi maendeleo ya Tanzania yawe mazuri.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Likokola kwa mchango wa kisayansi. Sasa namwita Mheshimiwa Lucy F. Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Elietta Switi na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu ajiandae.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Awali ya yote, napenda nimpongeze Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii. Kipekee, napenda pia nimpongeze Msemaji Mkuu wa Upinzani, Dr. Willibrod Slaa, kwa hotuba yake ambayo ilikuwa ni nzuri sana kama Serikali ikiamua kuchukua yale aliyokuwa akiyazungumzia kwa namna moja ama nyingine, inaweza ikasaidia katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli, anafanya kazi nzuri sana, anatoa ripoti nzuri sana, ameongea mengi yenye upungufu, kuna Wizara ambazo zinalipa

mishahara hewa. Ninapenda Waziri Mkuu atueleze, wale waliobainika katika kufanya upotevu wa hela za Serikali, wamechukuliwa hatua gani? Kwa sababu tusipompa motisha huyu Mdhibiti Mkuu, yeye anakuwa akitoa taarifa lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa sana sana unakuta mtu anahamishwa kutoka Idara nyingine kwenda nyingine na au kutoka Wizara fulani kwenda Wizara fulani, inabidi muonyeshe ni namna gani mnaweza mkawaadhibu watu hawa ili na yeye aweze kupata moyo wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Shirika letu la *Air Tanzania.* Shirika hili kwa sasa hivi ni kama limekufa baada ya kuacha ubia na *South Africa Airways*, imebaki na ndege moja. Wakaamua kwenda kununua *Air Bus 320*, *Air Bus* ile ilikuwa inatumika na *Air Jamaica*, ilikuwa Salvador, ilikuwa kwenye hali mbaya sana ilibidi itengenezwe kila kitu lakini mkataba wa kusaini ili kuchukua ile ndege kutoka Salvador ulifanyikia Ujerumani ndege iko Salvador. Kwa hiyo, wale waliokwenda kusaini mkataba, hawakujua ndege ilikuwa na hali gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kwamba ndege ile imekodishwa kwa dola 325,000 kwa mwezi, zaidi ya hapo, kuna *insurance*, Ma-*engineer* na bado kuna Ma-*captain* ambao wanatakiwa wakodishwe ili waweze kuendesha ndege ile. Kwa ujumla, ndege ile kila mwezi inalipa dola milioni 100,  sasa sijui kipaumbele hapo cha kwenda kuchukua ndege ile kukodisha kwa dola 325,000 ilitoka wapi kwa sababu kwenye *Pacific Aviation,* ninayo *price list* ya ndege, zinakuwa ni kiasi gani kwani ndege ile ile tungeweza kuipata kwa dola milioni 25. Ukigawanya dola 325,000 ina maana tungepata ndege karibu zaidi ya 10, kwa nini hawakwenda kukodisha *Air Bus*? *Boeing* 373300 unaweza kukodisha kwa dola milioni 17, sasa sielewi walikuwa wanatumia kigezo gani cha kwenda kuchukua *Air Bus* ambayo inahitaji Ma-*Captain* kutoka nje, Ma-*engineer* kutoka nje ambayo tayari hapa Tanzania tuna ma-*Captain* ambao wangeweza kurusha zile *Boeing* ambayo tusingekuwa na *charge* zaidi za kuwalaza kwenye mahoteli, kuwalipa mishahara ya kigeni ambapo tayari Ma-*captain* wetu wana uwezo wa kuendesha zile ndege za Boeing 373300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda mkataba wa ndege hii usitishwe mara moja, warudishiwe ndege yao ile halafu wakodishe ndege za *Boeing.* Naongea hivi kwa sababu ndege ile ilivyokodishwa tangu mwaka jana 2008, Mei, ilianza kazi Juni mpaka mwezi wa Desemba. Tangu mwezi wa Desemba mpaka sasa hivi ndege ile vipo chini na bado inalipa 325,000 kila mwezi na ndege hii imepelekwa kwa *checking*, je, iliyvyopelekwa kwa *checking,* ni sisi Watanzania tunalipa na sasa hivi ndege ile iko *due* kwa *major check* ya miaka 12 . Sasa nataka kuuliza ni nani atakayelipa gharama yote hiyo? Ina maana tuliletewa ndege mbovu sasa yule aliyetukodishia ile ndege anangojea sisi tulipe gharama zote hizo, mimi nafikiri hiyo hatutakuwa tunawatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege ile kwa sasa hivi, Serikali ni jukumu lake kuhakikisha kwamba inachukua jukumu la kuikomboa *Air Tanzania* kwa sababu sasa hivi wana deni la zaidi ya milioni 10 *dollars,* hakuna mwekezaji ambaye atakubali kuja kuchukua hayo madeni. Kwa hiyo, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wanachukua deni lile na kuleta ndege nyingine ambazo *Pilots* wetu wanaweza wakazitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kidogo kuhusu utalii na hapa naomba ku -*declare interest* kwamba mimi ni Mdau wa Utalii. Utalii wa Tanzania sasa hivi umekuwa ni wa ghali sana, wenzetu wa nchi jirani wamejaribu sana kupunguza bei ili waweze kupata watalii wengi iwapo sisi tunasema tunauza *quality not quantity* lakini kwa sasa hivi kwa sababu ya mtikisiko wa uchumi duniani, tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunapunguza bei za wageni kuja hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano mdogo tu, mgeni anakuja kupanda Mlima Kilimanjaro, *park fee* ni dola 60, mara sita, *hut fee* ni dollar 50 mara tano, kuna *rescue fee dollar* 20, *guidance porter 20 dollars* ambayo kwa ujumla wake inakuwa ni *dollar* 650 na mwenye kumleta mtalii bado hajaweka *profit* yake ya kumlaza hotelini, ya kulipa wale ma-*guide*, bado yule mtalii hajanunua *ticket* yake ya kufika hapa. Kwa maana hiyo, mtalii mpaka aweze kufika Tanzania siyo chini ya *dollar* 4000 mpaka 5000 kwa sasa hivi, wengi hawawezi, wenzetu Kenya wamehakikisha kwamba wameshusha *park fees* zimekuwa mpaka *dollar* 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwa sasa hivi kwa sababu kuna mtikitisiko wa uchumi duniani tufanye *promotion* hata ya sasa hivi mpaka Desemba tushushe *park fee* ili jumla ifike hata dola 420 kwa sababu sisi wa *Private Sector* tumeshafanya upande wetu, tumepunguza *profit* zetu lakini Serikali bado haijafanya lolote, Serikali nayo ingetusaidia ili Watalii waweze kuja hapa bila hivyo itakuwa ni ngumu sana kwa watalii kuongezeka. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Rais pale Kilimani, naomba kunukuu ukurasa wa nane anasema:-

*"Sekta ya utalii ambayo ndiyo Sekta Kiongozi kwa mapato ya fedha za kigeni nayo imebanwa pia. Takwimu zinaonesha 10% ya idadi ya watalii imepungua. Mwaka 2008 tulipata dola 388.2 milioni lakini mwaka 2009 tumepata dollar 302.1 milioni punguzo la dola milioni 87 na mwaka huu itazidi kupungua".*

Kwa hiyo, inabidi kwa makusudi kabisa tuhakikishwa tunapunguza hizi bei ili watalii waweze kuja kwa wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ngorongoro. Wale watu wa *conservation*, waongoza utalii, wana-*charge* gari kuingia *creator dollar* 200 kwa siku bado *park fee* na kila kitu, hiyo ni sawa kabisa ili kutunza mazingira lakini sasa kuna wale wakulima ambao wameingia kwenye mbuga kule Ngorongoro wanalima! Ngorongoro iko katika Seven *Wonders of the World* lakini watakuja kuiondoka kwa sababu kule kunaharibika. Naomba jamani wanasiasa acheni siasa wengi wanatetea wale wakulima wakae kule, siasa ziachwe kabisa ili ile mbuga yetu tuweze kuiendeleza na izidi kubaki palepale kwenye *Seven Wonders of the World.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie miundombinu ya Dar es Salaam. Tumekuwa tukizungumza mara nyingi msongamano wa magari Dar Es Salaam, wengi wamezungumza. Lakini pamoja na nia ya Serikali ya kusema watatengeza *flying overs* lakini huu ni mkakati wa muda mrefu, kwa mkakati wa muda mfupi, mimi ninashauri zile

*feeder roads* ambazo ni *ring roads,* wazitengeneze hata kwa kiwango cha changarawe ili magari madogo yaweze kupita kwa namna moja au nyingine ili waweze kupunguza msongamano wa magari katika jiji letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia kuhusu Daraja lile lililopo pale Chama katikati ya *Shoppers Plaza* na *TMJ hospital*, mvua zikinyesha hakuna alama ya daraja pale. Nimeshasema kuna watu wanaweza kufa pale, kuna tatizo kutengeneza lile daraja? Lile daraja siyo *expensive* sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ruhusa yako, niko tayari kutengeza lile daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gari zinazozoa takataka Dar es Salaam. Wale wafanyakazi wanaozoa takataka Dar es Salaam hawana vitendea kazi, magari yale ni mabovu na sijui wanapewaje leseni. Mimi ninashauri magari yale yapelekwe kwenye vyuma chakavu na wenye kupata hizo *tender* wahakikishiwe kwamba wanapewa *condition* kwamba gari ya takataka inatakiwa iwe namna gani, liwe jipya, walikague ili waweze kuzoa zile takataka kwa sababu zinaleta magonjwa. Takataka zinadondoka barabarani, kuna magonjwa ya milipuko Dar es Salaam ukizingatia mifereji ile ya maji safi na maji taka iko wazi haijafunikwa, kuna mazalia ya mbu na uchafu tele Dar es Salaam, kwa nini wasifuate ushauri kutoka kwa Mheshimiwa Keenja? Mbona Mheshimiwa Keenja alipokuwepo wakati ule, mji ulikuwa msafi kabisa? Waende wakatafuta ushauri kwake alifanyaje mpaka mji ule ukawa msafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamalizia, hapa Bungeni Wabunge wote kwa sasa hivi naona wengi wanawanyooshea Mawaziri vidole, wanalalamika lakini mimi sidhani kama wanatenda haki. Wabunge wote tulikuja ndani ya Bunge hili, tulikula kiapo, tutaitumikia na tutailinda nchi ya Tanzania na kila mtu kwa imani yake alishika kama ni Biblia au ni Quran  na wasioamini kwa sababu wanaamini kuna kitu kiko juu yetu waliapa pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonisikitisha hata katika kitabu chetu kitakatifu cha Biblia, kwa sababu ya muda sitaweza kusoma lakini kwa wale ambao hawana Biblia nitaweza nikawasomea baadaye. Hosea 4:1-3 na Hezekiel 18:24, inasema ukila kiapo ukifuate na wanasema wale wanaoongea uongo watakufa na wengine kwa sababu ya uongo tutakuja kuangamia na tutaiteketeza nchi hii, ipo katika vitabu vitakatifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kusema hivi ni nini? Unakuta kuna Wabunge wanachangia hoja, wanaikosoa hoja, wanalalamika sana mpaka wanawanyooshea vidole Mawaziri, lakini wakifia mwisho wanasema wanaunga mkono hoja mia kwa mia. Nawaomba, acheni huo unafiki hata Mwenyezi Mungu haimpendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakuita sasa Mheshimiwa Eliatta Switi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynab Matibu Vulu na Mheshimiwa Dunstan Mkapa ajiandae.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako, sasa niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa mikakati inayoendelea ili nasi Mkoa wa Rukwa tuweze kupata barabara za lami. Serikali hii wote tunajua inaongozwa au inasimamiwa na Mheshimiwa Mizengo K.P. Pinda, Waziri wa Jamhuri ya Muungano na Rais wake Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Nasema ahsante sana kwa Chama cha Mapinduzi, kwa kutuzalia watu hawa wenye uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuwa wakati wote amekuwa akiwapa moyo watu wa Rukwa kwamba barabara ya lami itajengwa kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga. Nimemshuhudia mimi mwenyewe, Mheshimiwa Rais wetu, akiwa Maputo akiongea na Watanzania wanaoishi huko kwamba kwa kweli barabara ya Tunduma – Sumbawanga itajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kwamba sina haja ya kuzitaja barabara hizo kwa sababu zilitajwa na mwenzangu Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, ila niseme kuwa wana-Rukwa sasa wajiandae nao kupokea raha ya uhuru wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiongelea barabara hizi, naomba niishukuru Serikali kwa kuwa iliona uko umuhimu wa kufufua barabara ya kutoka Mwimbi kwenda Mozi Zambia. Barabara hiyo, inatuunganisha sisi na nchi hiyo jirani ya Zambia nayo ina kilomita 14 tu na ilitengewa shilingi 45 milioni mwaka jana na barabara hiyo ikafufuliwa. Naiomba Serikali sasa ijiandae upya ili barabara hiyo inayoanza Kayengesa kwenda Mwimbi kilomita 60, Kawimbe kilometa 60 mpaka Mozi iwekewe lami maana inatuunganisha na nchi jirani.

Lakini barabara hiyo ikitoka Mwimbi kwenda Ulumi mpaka Mambwekenya mpaka mtula, nayo pia naomba iwekewe lami kwa sababu inatumika na watu wa DRC na Zambia kufika kwetu Tanzania lakini pia kule Mtula kuna soko la Kimataifa. Naomba Serikali itengeneze barabara hizo kwa lami. Serikali ikifanya hivyo, tutaimarisha biashara na DRC na Zambia. Hivyo basi, nichukue fursa hii kuiomba Serikali iongeze juhudi au mipango ili tufanikiwe kutengeneza barabara hizo.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Kanuni ya 68 lakini inaongozwa na Kanuni ya 64 (1) (g) ambayo inakataza mtu yeyote kutumia lugha ya kuudhi au inayomdhalilisha mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati msemaji aliyemaliza kabla ya huyu anayechangia sasa, amesema watu wanaolalamika sana na baadaye wanasema wanaunga mkono hoja, ni wanafiki. Lugha hii inaudhi na inadhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako, kwa kuwa kwa ninavyofahamu mimi, kulalamika au kusemea Majimbo yetu ni haki yetu lakini pia kunasaidia tu Serikali kuzingatia katika kutekeleza yale ambayo tunadhani wanaweza kuchukua fursa hii kuyasikiliza na kuyarekebisha na siyo kuunga mkono kwamba ni upungufu na ni unafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Simbachawene kwa mwongozo huo. Mimi labda niseme tu kwamba Mheshimiwa alipokuwa akichangia alikuwa akifanya *quotation* ya Biblia kwamba hizo aya ndiyo zilikuwa zinasema hivyo. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba tunaendelea tu na hili suala tumuachie tu, Mheshimiwa lakini hutotakiwa tena kuendelea kutumia lugha hiyo kwa sababu ni kweli itakuwa inaudhi, imekulinda Biblia ambayo umei-*quote*, tunaendelea.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu uniongezee ili niweze kuchangia.

**MWENYEKITI:** Sawa, Mheshimiwa endelea.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Ukurasa wa 40, amesisitiza matengenezo ya barabara zetu uwe wa viwango na uangalizi wake uwe wa makini. Inasikitisha kwa kweli. Sisi Watanzania tumekuwa tukijenga barabara zetu kwa gharama kubwa, tukitumia pesa za ndani na pesa za nje, halafu watu wanachukua sululu wanachimba hizo barabara na kuweka matuta *(speed humps).* Sidhani kama inakubalika kweli kuweka matuta katika barabara za kuu, lakini hii sisi inatendeka. Kwani haiwezekani Watanzania tukatumia alama za barabara badala ya kuweka matuta ya namna hiyo?

Mbona watu wengine katika nchi nyingine wanafanya hivyo? Ikiwa wako watu ambao hawawezi kufuata alama za barabara basi waadhibiwe lakini si haki kuweka matuta ya namna hiyo katika barabara kuu. Barabara kuu hizi sasa hivi zina madhara yanayoeleweka. Moja ni kwamba sasa tumeharibu barabara zetu, lakini la pili ni kwamba magari yanaharibika haraka na wakati mwingine hata *sterling* zinaweza kufyatuka na magari yakapoteza mwelekeo na ajali kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia hasa kipande cha Milima ya Udzungwa ambapo barabara imewekewa viraka vingi na wakati mwingine mashimo haya yanakuwa yamekaa pale kwa muda mrefu sana mpaka kusababisha Madereva kukwepa barabara na kupita pembeni ambayo inaweza kusababisha magari kutumbukia mtoni. Wakati mwingine magari yamegongana kwa sababu barabara hiyo ina kona nyingi katika eneo la Ruaha. Magari yanagongana kwa sababu Madereva huwa wanakwepa mashimo.

Dereva anakwenda *sight* ambayo siyo ya kwake halafu anakutana na gari mbele na kwa hiyo wanagongana. Barabara hizo wakati mwingine zimesababisha wavamizi kuvamia magari kwa mfano kipande cha Tunduma – Mbeya katika maporomoko yale zimewekwa hizo *speed humps* na majambazi hungoja palepale. Kwa hiyo, wanavamia na inaweza hata ikahatarisha maisha ya wasafiri watumiao barabara hiyo. Wale wote wanaotumia barabara ya Tunduma – Mbeya wanaweza kuniunga mkono katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kilimo kwanza. Kwa Mkoa wa Rukwa, kilimo kwanza ni jadi yetu na hili neno najua linatuhamasisha ili tuongeze uzalishaji. Kilimo kwanza, kadri Serikali inavyoona ni kuongeza mazao lakini ili tufanikishe haya na sasa naomba kwa kupitia Bunge lako Tukufu, elimu ipelekwe kwa wakulima ili wajue kutumia matrekta wanayopewa na Halmashauri au wanayonunua wenyewe. La pili, wapewe hamasa ya namna ya kutumika mbolea, mbegu na madawa ya kuua wadudu. Mkoa wa Rukwa, Mbeya, Morogoro, Iringa, Kigoma na Songea kama ilivyoanishwa, Serikali inapaswa kuwapa kipaumbele katika kuwapatia pembejeo na vile vyote vinavyohusu kilimo. Hiyo imeainishwa vizuri lakini tunapenda ili kuwahamasisha wakulima wote waweze kushiriki katika kuzalisha basi Serikali iangalie upya namna hawa wakulima wa kawaida wanavyoweza kupata *package* ya mbolea kwa sababu *package* hii ina mifuko miwili ya *Urea* kwa shilingi 48. Mbegu ya Mahindi kilo 10 shilingi 13200/=, Minjingu shilingi 48,000/= jumla ni shilingi 109,200/=. Wengi wa wakulima hawa wa kawaida huu ni mzigo mkubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali itafute namna nyingine ambayo wakulima hawa wanaweza kupata *package* hii kwa matunda mazuri. Kilimo bila umwagiliaji hatufiki mbali, lakini kwa muda mdogo tu uliopita Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ameainisha vema masuala haya. Kwa hiyo, naomba basi iharakishwe namna gani tunaweza kukitumia hiki kilimo cha umwagiliaji ili kufanikisha kauli mbiu hii ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuruhusu kilimo cha Mbono mkoani Rukwa na ujenzi wa kiwanda kilichojengwa na kampuni ya Prokon ya Ujerumani. Hivi sasa vijana au wajasiriamali wameanza kutengeneza sabuni kutokana na mafuta ya Mbono. Lakini pia nao wameanza kukamua mafuta ya *Bio-diesel* kwa kutumia mafuta ya Mbono. Watu wa Rukwa, tunashukuru sana kwa sababu hii imeanza kuiweka Rukwa katika sura mpya badala ya kutumika tu zao la msimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali sasa iwasaidie Wajasiriamali hawa wadogo wanaofungua viwanda vidogovidogo ili waweze nao kusaidiwa katika kupunguza umaskini Rukwa kwa kuwa wakulima wa Mbono nao pia watategemea sana watu hawa na watakuwa nao wamesaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji. Mkoa wa Rukwa hupata mvua nyingi, lakini maji haya yote huingia ardhini na mengine yanapotelea huko katika Maziwa ya Rukwa na Tanganyika. Japokuwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji amefafanua hapa lakini bado tunaomba iharakishwe juhudi kwa Mkoa wa Rukwa kuvuna maji ili wana Rukwa waondokane na magonjwa ya kuhara na homa ya matumbo ambayo sasa ni sugu ndani ya Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa ni giza ukitoa Sumbawanga na Mpanda, ambao hata nao umeme wao hauna uhakika. Tumeahidiwa jenereta kwa Sumbawanga lakini Mkoa ni mkubwa mno tunahitaji kupata umeme wa gridi ili umeme huu uweze kufika vijijini na sisi tuweze kuweka viwanda na tupate maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI. UKIMWI kama tulivyoambiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni tishio bado, maambukizi mapya yanaendelea na takribani watu 2,000,000 wanaishi na virusi vya UKIMWI. Lakini ukiangalia katika fedha zilizotengwa, fedha za ndani hakuna, fedha za wafadhili ni shilingi bilioni 103, 174,068, 600. Wasiwasi wangu ni kwamba sasa hivi, dunia imekumbwa na mambo mawili. Mabadiliko ya hali ya hewa na mtikisiko wa uchumi. Je, endapo hawa wanaotusaidia kutuletea hela watapunguza matumizi haya, itakuwaje? Ina maana Watanzania wengi wanaoishi na virusi vya Ukimwi watakufa kwa kuwa, hatuwezi tena kupata dawa za kupunguza makali ya Ukimwi! Wala hatutakuwa na uwezo wa kuhamasisha kupunguza kasi ya maambukizi ambayo sasa hivi Serikali inajitahidi kwa kadri ya uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hali ya barabara za Rukwa, kwa maana hiyo, ndiyo maana imetenga shilingi Bilioni 4,000, 560,000, kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Mpanda na Bukoba. Mheshimiwa Masilingi, aache tu kuwa na wasiwasi, hizi fedha tutazigawana bila wasiwasi, ili sote tuweze kufaidika na fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwanza, kukushuruku kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ambayo leo hii ni bajeti yangu ya nne toka niingie katika nyumba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Naibu wake na Watendaji wote kwa hotuba nzuri ambayo wameiwasilisha na sisi tumeipokea.

Baada ya pongezi hizo, naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kupitia ilani yetu ya uchaguzi. Sote ni mashahidi, tumeona miradi mbalimbali iliyofunguliwa ukiwemo ule wa daraja la pale Ruvu kwangu Mkoa wa Pwani, maji Mkoa wa Mwanza, barabara nyingi zimeongezeka, hospitali na shule. Lakini kama vile haitoshi, hii ni kwamba, wamepokezana kijiti, yeye kakipokea kutoka kwa Mheshimiwa Rais Mstaafu, Benjamin William Mkapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Mkapa na yeye anastahili apate pongezi zake kwa sababu, ana mchango wake ambao umetufanya tufikie hapa tulipo. Amehimiza shule kwa kupitia Mradi wa MMEM, MEMKWA na MMES na shule hizo kupitia awamu hii ya Nne, kila Kata sasa hivi ina shule za msingi na shule za sekondari, kwa hiyo, haya ni mafanikio makubwa sana. Halikadhalika Maji, Afya na Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge tuna kazi kubwa sana ya kusimamia maendeleo katika nchi yetu na hasa kwenye Majimbo yetu tunayotoka. Iwe sisi wa Viti Maalum, iwe wale wa Majimbo, lakini sote kazi yetu ni moja, hatuna sababu ya kugombea fito kwa sababu sote tunajenga nyumba moja ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu gani? Kwanza nataka nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais, kupitia Chama cha Mapinduzi, kwa jitihada zake za kuona ni kiasi gani Wanawake tunaweza kufanya kazi. Ameweza kuchagua Mawaziri Wanawake na Manaibu, wamefanya kazi kwa uwezo wao, hawajamuangusha Mheshimiwa Rais, vilevile na sisi Wabunge wa Viti Maalum, jana tumeweza kupata pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mzindakaya akisema kwamba, Wanawake wa Viti Maalum wanachapa kazi. Sasa ndugu zangu, wa Majimbo mkituona tunafanya kazi, sisi wote tunajenga nyumba moja, hatuna sababu ya kugombea fito, tunachokifanya tunahitaji maendeleo kwa wananchi wetu na tuna ushirikiano na nyinyi, kwa hiyo tunapojitokeza kufanya kazi na ninyi mtusaidie na mtusemee panapohitaji kusemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, wananchi wanatutegemea sana lakini tatizo tunalolipata, mimi nitaanza kwanza kwa Mkoa wangu wa Pwani, tumepewa watendaji katika Halmashauri zetu, lakini kwa bahati mbaya Mkoa wa Pwani, naomba niufananishe na hii ninarudia nafikiri ni mara ya pili au ya tatu, hizi nyumba zetu za kiasili tulizojenga zina nyumba kubwa mbele na nyuma kuna banda la uani, Wazungu wanaita *servant quarters, s*asa Mkoa wa Pwani, tumekuwa kama banda la uani. Kwa nini nasema hivyo? Mkoa wa Pwani, uko jirani sana na Mkoa wa Dar es Salaam, maendeleo yote yanayofanyika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kiini chake kinatoka Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakula kinacholiwa Mkoa wa Dar es Salaam, naweza kusema asilimia 65 kinatoka Mkoa wa Pwani. Mkoa wa Pwani ndio tunaolima, mikoa mingine inachangia lakini hakuna anayeona, kwa nini nilitoa mfano wa nyumba kubwa na banda la uani? Nyumba za banda la uani ndiyo kuna jiko, vyombo vinaoshwa huko, kwa hiyo chakula kinapelekwa kule mbele, tayari kwa kuliwa na maliwato iko huko, kwa hiyo shughuli zote zinafanyika huko uani, kule nyumba kubwa kunakopelekwa vyakula, hajulikani aliyefanya kazi ile nani, watu wanakisifia chakula mezani na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kilio chetu Mkoa wa Pwani, tunaona jinsi gani Dar es Salaam inavyoharibika katika miundombinu, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie hili katika utengenezaji wa miundombinu. Tuwe na miundombinu ya uhakika, maeneo yatengwe yajulikane, hapa ni shule, hapa ni hospitali, hapa nyumba za kuishi, sio sasa hivi Mkoa wa Dar es Salaam, umebadilika una sura nyingine kabisa na ile sura kimazingira ni hatari *is a bombshell* wakati wowote linaweza likalipuka tukaathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mkoa wa Pwani utizamwe, naomba sana na watendaji wetu katika Halmashauri zetu za Mkoa wa Pwani, isiwe pale ndiyo pahala

pa kutupia takataka. Tumepokea watendaji kutoka katika Halmashauri nyingine, wengine walifanya vizuri, lakini wengi waliofanya vibaya wamesukumiwa kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Pwani, nasema watumishi hao wabovu hatuwataki na itapobidi tutasimama kidete tutawaondoa. Tutakwenda mbio kwa Mheshimiwa Waziri mhusika, imeshindikana basi tutajua jinsi ya kufanya. Kama mlango, tutafunga, kama viti tutaondoa. Sisi tunataka maendeleo, hatuwezi kila siku kuwa wa mwisho. Barabara tunazotegemea ni hizo mbili na tukisema tufunge, hakuna atakayekwenda sijui Mwanza, sijui Tabora, sijui Shinyanga, hakuna. Hata ndege tutafunga njia kwa sababu ndege zote lazima zipite Mkoa wa Pwani, tutafunga inapobidi, tunahitaji maendeleo, hatuna chuo, hatuna kitu chochote. *(Makofi/kicheko)*

**MBUNGE FULANI**: Mnazo ngoma!

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoma kila kabila linacheza na kama hujacheza ngoma basi wewe hujawa Mtanzania halisi. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kusema ni kwamba, ufike wakati tuangalie ni kitu gani tunakifanyia Mkoa wa Pwani, tuweze kuona na sisi tunafika pahala tunapata maendeleo yetu. Sisi tunalima, tunashukuru sana Mheshimiwa Rais, ametangaza Kilimo Kwanza, tunalima Korosho, tunalima Mpunga, tuna mabonde na sasa hivi tumetengeneza *schemes* katika Wilaya mbalimbali, Mkuranga, Rufiji na Bagamoyo lakini *schemes* hizo za umwagiliaji tunahitajai tupate msaada wa Serikali ili kuweza kuimarisha hizo *schemes* ili wananchi wa Mkoa wa Pwani, waweze kulima. Tuna mabonde ya kutosha, mabonde yale yakipata utaratibu mzuri wa umwagiliaji, tuna hakika Mkoa wa Pwani, tutajilisha sisi wenyewe chakula na Watanzania wote na hata kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwanza, kitatusaidia sana sisi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, amelisema lakini tunaomba Serikali iweke mkakati. Mkakati wa kwanza tunaomba, Bodi ya Mazao mbalimbali iundwe. Sisi ni wakulima maarufu wa zao la muhogo lakini cha kushangaza, muhogo ule hauna sera yoyote inayoulinda, wakati muhogo ni zao ambalo halihitaji mvua, halihitaji mbolea na wakulima wengi wa Mkoa wa Pwani, tunalima zao la muhogo. Leo hii sisi tukilima muhogo ukatengenezewa *scheme* ya kupata sera nzuri ya kuweza kuuza nje, bodi za mazao zikatutafutia soko na kadhalika, nina hakika zao la muhogo litaleta tija Mkoa wa Pwani na si tija tu, litasaidia kuinua kipato cha mwananchi wa Mkoa wa Pwani, unyonge na umasikini utatutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya matunda vilevile, jamani tuleteeni viwanda, *Public Private Partinership* itengenezewe mkakati mzuri, wananchi wana nafasi ya kuhodhi *shares* katika viwanda. Sio kila siku tu viwanda vile waje wawekezaji, sisi hatupati kitu, tuajiriwe, mshahara shilingi 10,000, 15,000 haitoshi! Tunahitaji na sisi miongoni mwetu tuwe mamilionea, tuwe na utajiri wa aina Fulani, sio tu kila siku tuwe sisi waajiriwa, wawekezaji wanakuja katika ardhi yetu wanaweka viwanda, mazao tunalima sisi, tunachokipa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongeze lingine suala la afya. Afya ni haki ya msingi kama ilivyo maji, ni haki ya msingi kwa mwananchi yeyote Mtanzania. Mkoa wa Pwani, katika suala la maji kuna maeneo tumeweza kufikia kiwango cha asilimia 65, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Wafadhili mbalimbali kama Japani na kwingeneko lakini bado haitoshi, tunahitaji miundombinu ambayo itatusaidia kupeleka maji hasa Wilaya ya Kisarawe. Ardhi ya Kisarawe, *water table* iko chini sana na inapopatikana maji yake yanakuwa na chumvi. Tunaomba sana Serikali iangalie jinsi gani itaweka miundombinu ya kuvuta maji kutoka Mto Ruvu, Mto Rufiji na kuwafikishia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, katika afya, tunaona wakati umefika Serikali iangalie na kutoa kipaumbele cha kutoa mafunzo kwa wingi kwa Wauguzi, Madaktari na wataalamu mbalimbali wa afya. Tunakwenda kwenye kujenga kituo cha afya katika kila Kata, je, kama hatuna watendaji katika vituo hivyo vya afya, hayo yatakuwa ni majengo ambayo hayatakuwa na maana au unaweza ukaenda ukakuta Kata nyingine Muuguzi ndiye huyohuyo anayezalisha, ndiye huyohuyo anayetibia. Sasa tumwombe Mwenyezi Mungu, Muuguzi huyo asimpe maradhi, akiumwa yeye, Mama hazai, Mtoto haugui, Baba haugui, kwa hiyo, tunaomba hili suala liangaliwe ili idadi ya Wauguzi na Madaktari iongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahimiza watu walime lakini barabara za vijijini si nzuri, sasa mazao yale yanapelekwa vipi sokoni? Tuangalie uwezekano wa hizi barabara, tuangalie pia njia nyingine za kupata mapato katika miundombinu kwenye bandari zetu. Tuna bandari ya Mtwara, tuna bandari ya Tanga, tuna bandari ya Dar es Salaam na kuna bandari moja siikii ikitajwa hata siku moja, sijui ina mkosi gani bandari ile, Bandari ya Lindi. Ile bandari inahitaji ifufuliwe tu ili wananchi nao waweze kupata ajira pale na hali kadhalika nchi jirani wanaweza wakatumia kupeleka mizigo yao pale na hiyo itafungua njia ya kupatia pato la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kutoa pongezi tena kwa Mheshimiwa Rais, kwa Chuo Kikuu cha Dodoma. Ni chuo cha aina yake, kinahitaji kipate Walimu wa kutosha na kinahitaji sisi tuweze kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu bora na elimu hiyo itatoka katika shule zetu, tuhakikishe watoto wetu pia tunawapeleka shuleni lakini Serikali itusaidie kutuwezesha majengo ya maabara, vilevile iweze kutusaidia kupata mabweni, kina Fataki wamezidi, mimba za mashuleni zimezidi, tunaomba hayo yafanyike ili tuweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii ya bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo amewasilisha hapa na nafikiri ina mwelekeo mzuri kwa maendeleo ya nchi kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninapenda pia nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Celina Kombani, ambaye ameonesha uwezo mkubwa kabisa kuimudu Wizara hii katika kazi zake za kila siku, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kumpongeza rafiki yangu Mheshimiwa Mwanri, ameonesha pia kumudu ofisi hii, kwa kweli ametoa mchango mkubwa kumsaidia Waziri wa Nchi na hayo yameonekana na hata kule tulipokuwa naye kwenye Kamati ya *LAAC* alikuwa ni mpambanaji mzuri sana, tulikuwa tunamwita *bottom line. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Waziri Mkuu kwa kweli watendaji wako pale ofisini ni watu wenye ushirikiano mzuri, Katibu Mkuu, Mama Tarishi, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Nyimbi, Mama Macha, ndugu Kabuje na pia Mama Njovu, hawa watu wote kwa kweli wanatusaidia sana tukienda pale kwa matatizo mbalimbali, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Anatory Tarimo, huyu ameusaidia sana Mkoa wetu wa Mtwara kupiga maendeleo, amepata matatizo sana tulipokuwa tunaanza na mtindo wa stakabadhi ghalani, alipata vikwazo kwa sababu wananchi walikuwa hawaupendi mtindo huu lakini kutokana na elimu yake aliyoitoa kwa wananchi, sasa hivi mtindo ule unakubalika. Lakini vilevile, nimpongeze *DC* aliyeondoka, Mheshimiwa Msangi, kwa kuwa, alikuwa nguzo kubwa ya maendeleo katika Wilaya yetu ya Nanyumbu. Vilevile nimpongeze na kumkaribisha *DC* mpya, Mheshimiwa Fatma, ambaye amekuja hivi karibuni, ameanza kazi vizuri na anaonyesha kuwa ana uwezo mkubwa wa kuimudu kazi hiyo, hivyo namkaribisha sana kulisukuma gurudumu la maendeleo la Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naiomba ofisi ya Waziri Mkuu, imsaidie Mheshimiwa Fatma, anaishi katika mazingira magumu sana, nyumba aliyojengewa haina samani, umeme, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu imsaidie aweze naye kujisikia kwamba, ni miongoni mwa Ma-*DC* wanaojaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kutoa pongezi zangu kwa Watendaji wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu, wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, Ndugu Nkya, kwa kweli wameonyesha ushirikiano mkubwa, tunasukuma nao gurudumu la maendeleo pamoja na nadhani baada ya muda, Nanyumbu itaongoza katika maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo, ninapenda nianze na suala la elimu. Wilaya ya Nanyumbu, iko pembezoni mwa nchi, ilikuwa ni uwanja wa mapambano wakati ule wa ukombozi Kusini mwa Afrika, maendeleo pale yamekuwa duni hasa katika sekta ya elimu, hatuna shule za kutosha, majengo yaliyopo ni hohehahe, kuna shule zingine bado ni za nyasi katika karne hii, kwa kweli huwezi kuamini kwamba, tupo katika karne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande mwingine ni uhaba wa Walimu. Nanyumbu tuna uhaba mkubwa sana wa Walimu, tunaletewa orodha ya Walimu kuja pale, lakini wanaokuja kuripoti ni wachache mno. Sasa tunaomba hapa angalau Walimu wale wanaoletwa kule wapewe angalau posho ya mazingira magumu, waweze kumudu kazi pale na waweze kujiona kwamba, tunawajali, hasa upande wa shule za sekondari Walimu ni wachache sana. Nimetembelea shule karibu zote za sekondari, Maratani, Ikangaula, Napacho na kwingineko, tatizo la Walimu katika shule za sekondari ni kubwa mno. Tunaomba pia tuletewe Walimu wa masomo ya sayansi kwa sababu Taifa hili litakuwa na Wanasheria na Walimu tu lakini uvumbuzi hautakuwepo. Sasa hivi tunasema Kilimo Kwanza, tunahitaji wanasayansi katika sekta ya kilimo na sekta ya mifugo, naomba sana ofisi ya Waziri Mkuu, itusaidie angalau tuletewe Walimu wa sayansi katika Wilaya ya Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ya wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu, ni maji. Nchi ile ni kame sana, sasa hivi tayari nimeshaletewa malalamiko sehemu mbalimbali za Wilayani kwamba, tuna tatizo kubwa la maji. Tunaomba Wizara husika na ofisi ya Waziri Mkuu, itusaidie suala hili la maji kwani ni kero kubwa mno, akina mama wanateseka, wanaamka usiku wa manane kutafuta ndoo moja ya maji, siyo tanki, ni ndoo moja ya maji, naona Mheshimiwa Mwandosya unaniangalia, lakini naomba nikueleze kwamba, Wilayani kwangu Nanyumbu tuna kero kubwa sana ya maji, ukienda Chitowe, Lumesule, Mikangaula, Napacho, kote Wilayani tatizo ni maji. Tone la maji kulipata ni kazi kubwa mno. Nawaonea huruma sana akina mama wanavyopata tabu. Wanaamshana na waume zao usiku kwenda kutafuta ndoo moja ya maji, sasa huko usiku kuna mambo mengi, kuna wanyama wakali, kuna nyoka na vinginevyo ambavyo vinaweza kuwadhuru. Tunaomba mtuangalie hilo, Waziri wa Maji ninapokuja ofisini kwako usidhani kwamba, nakupotezea muda, kwa kweli kero kubwa ya maji Nanyumbu inatusumbua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ambayo nimekuwa nikiizungumza sana hapa ni ya wanyamapori. Jamani wapiga kura wangu wanauawa sana na Ndovu. Nimesema juzi kwamba, mwezi wa Kumi na Mbili, siku moja tu, Tembo mmoja ameua watu watatu na tarehe mbili mwezi wa Tatu, mtu mwingine aliuawa tena na Tembo. Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Maliasili, tunaomba mlione hili kama ni janga la Wilaya ya Nanyumbu. Nakuomba Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, ufanye ziara Wilayani kwangu ukutane na wananchi wakueleze matatizo yao, mazao yanaharibiwa, watu wanakufa, watu wanakaa katika hali ya hofu, nilishamwambia siku moja Mheshimiwa Mwanri, alipokuja kwamba, katika mkutano huu ukiona watu wanapukutika basi ujue kwamba, Tembo yupo karibu anakuja, utabaki peke yako, ila ukiniona na mimi naanza kukimbia basi na wewe unifuate. Ninachotaka kusema ni kwamba, Wizara inayohusika pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, itusaidie kwa kweli, Tembo wanaharibu mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la miundombinu. Tunashukuru sana Serikali inajenga barabara ya kutoka Masasi mpaka Mangaka, lakini barabara ile tunaomba Wizara ya Miundombinu, iiangalie kwa macho mawili kwa sababu ubora wake unatia shaka, hata alipokuja Mheshimiwa Mwanri, tukamweleza tukamwambia haina

mifereji, maji yanatuama mengi hata kabla haijaisha. Kwa hiyo, naomba sana mtusaidie kuona barabara ile inakuwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ombi langu lingine ni kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani. Kituo cha Polisi pale Mangaka, kipo lakini Polisi wake wanaishi katika mazingira magumu sana. Hawana, nyumba, hawana vitendea kazi, Wilaya ile ni kubwa, wana gari moja tu wanatakiwa kupeleka wafungwa wao mahabusu Masasi, umbali wa kilomita 56 kila siku. Ninaomba Wizara husika itusaidie kuongeza vitendea kazi hasa magari na pikipiki na Polisi wale wajengewe nyumba, wanakaa mitaani huko kwenye nyumba ambazo ni mbavu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Kilimo Kwanza. Kauli mbiu hii ni nzuri sana hata sisi Wilayani Nanyumbu, tutaipokea kwa mikono miwili lakini sasa bado mkulima wa Nanyumbu, anatumia jembe la mkono. Tumefurahi kuona kwamba, katika bajeti kuna matrekta ambayo Halmashauri itaagiza, huu ni ukombozi na ninatumaini sasa hata ile kauli mbiu yetu ya kule Nanyumbu naomba niinukuu *’Chitu Unihuma’* sasa hivi itaendelea vizuri kwamba, wananchi sasa wataweza kulima kwa bidii na kuongeza mapato yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni nishati. Wilaya ya Nanyumbu haina umeme, tukitaka kuona umeme tunakwenda Masasi umbali wa kilomita 56, nimefurahi kuona katika bajeti ya mwaka 2009/2010, kwamba, kampuni ya *ARTUMAS* itapewa mkopo kwa ajili ya kuendeleza mradi ule kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa kuwa, Wilaya ya Nanyumbu iko Mkoani Mtwara, nategemea kwamba, watu wa Wilaya ya Nanyumbu nao watapatiwa huduma hii ili na wenyewe waweze kuwa na viwanda vidogovidogo na huduma nyingine hasa pale hospitali, ili waweze kufanya operesheni zao na shughuli zingine za maabara bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni umaskini. Umaskini Wilayani Nanyumbu, ni mkubwa sana ingawa wanasema kitaifa unapungua lakini kwa kweli naomba vigezo hivyo viangaliwe pia na katika Wilaya ya Nanyumbu, wananchi ni maskini na wengine wanashindwa hata kula mlo mmoja kwa siku. Naomba Wilaya hizi za pembezoni mtuangalie, kwani mmetusahau sana, kila siku katikati ya nchi tu huku pembeni mmetusahau. Kama nilivyosema, Wilaya ya Nanyumbu tulikuwa kwenye mapambano kwa muda mrefu lakini nashukuru na nimefurahi kusikia katika hotuba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu, kuna mambo yamenifurahisha ambayo yamepelekwa Wilayani kwangu. Kwa mfano, ujenzi wa hosteli za wanafunzi Wilayani kwangu kwa kweli tatizo la mimba ni kubwa nafikiri hii inaweza kupunguza kasi ya mimba katika Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya. Kama nilivyosema upande wa afya ni matatizo, tuna vituo vya afya vitatu tu na zahanati 14 katika vijiji 77. Kwa kweli vifo vinakuwa vingi na wananchi wengi wanatembea umbali mrefu kwenda kupata huduma ya afya, watu wengi wanafia njiani, watoto wengi wanakufa bila kupata huduma inayotakiwa na wazee wanakufa kwa sababu ya kwenda mwendo mrefu bila kupata huduma ya afya, naomba sana tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, labda kabla hatujaendelea, nitoe tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Uongozi kwamba, kuna kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi katika *Speaker's Lounge* ya ukumbi huu mpya saa 7.00 mchana mara tutakapomaliza hapa. Kwa hiyo, kwa wale ambao wako nje baadaye wajue kwamba, kikao kiko huku kwenye *Speaker's Lounge* mpya saa 7.00 mchana na wale ambao walikuwa labda wanapanga kuondoka, nimeona nilitoe mapema ili wapate habari hiyo.

Sasa tunaendelea, namwita Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Jacob Shibiliti ajiandae.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu, Ofisi ambayo inashughulikia uendeshaji mzima wa Serikali.

Kabla sijaendelea, nichukue fursa hii kutambua mchango mkubwa sana unaofanywa na viongozi wa Mkoa wa Kigoma katika kuleta maendeleo ya Mkoa wa Kigoma. Ninapenda kumpongeza sana Mkuu wetu wa Mkoa, Kanali Simbakalia, kwa mabadiliko makubwa sana, barabara sasa zinajengwa, lakini nashukuru zaidi kwamba barabara zote zinazojengwa hazipo Jimbo la Kigoma Kaskazini kwa hiyo inadhihirisha kabisa kwamba hata wananchi wakiamua kuchagua Upinzani maendeleo watapata kwa sababu wanalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mwandiga/Manyovu Kigoma Kaskazini, barabara ya Kigoma/Kidawe iko Kigoma Kaskazini na Kigoma ina majimbo 7 ya uchaguzi ni Jimbo moja tu ndilo liko Upinzani, Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakupongeza kwenda kufungua barabara ile, naomba radhi sikuwepo siku ile kwa sababu nilikuwa Biharamulo. Unajua tulikuwa wachache huko inabidi kuongeza idadi ya Wabunge wa Upinzani ili tuendelee kuwabana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya michango ya Wabunge katika hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ni ya kiuchaguzi, uchaguzi na mimi nitakwenda kiuchaguzi uchaguzi. Sasa hivi tumejenga mazingira ya kujenga Taifa lenye mgawanyiko mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati nachangia hotuba ya bajeti, nilisema kwamba tunajenga Mataifa mawili ndani ya nchi moja kwa sababu ya mgawanyiko mkubwa na tofauti kubwa sana za kipato kati ya wananchi mbalimbali na nitazungumza kwa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005, Chama cha Mapinduz, kiliahidi kupunguza idadi ya watu maskini Tanzania kwa nusu. Kwa mujibu wa Ilani na

MKUKUTA pia ulionyesha hivyo hivyo. Taarifa ya *Household Budget Survey* ambayo imetoka mwezi Novemba, 2008 inaonyesha idadi ya watu maskini kati ya mwaka 2001 na mwaka 2007 imeongezeka kutoka watu 11,000,000 mpaka 12,700,000. Kwa hiyo, badala ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Kimapinduzi kupunguza idadi ya watu maskini kutoka 11,000,000 mpaka 5,000,000 watu maskini 1,700,000 zaidi wameongezeka Tanzania na hii ni taarifa ya Serikali sio taarifa zangu, *Household Budget Survey* ni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika idadi ya watu 12,700,000 maskini Tanzania ambayo ni asilimia 33.5 ya Watanzania wote asilimia 74 ya watu hao ni wakulima wa vijijini. *74% of poor people* Watanzania ni wakulima wa vijijini, kwa hiyo hali inaonyesha kwamba umaskini umejikita zaidi vijijini. Chama cha Mapinduzi kiliahidi kwenye Ilani ya Uchaguzi mwaka 2005 kwamba watahakikisha sekta ya kilimo inakua kati ya asilimia 8 na 10 ili kufikia hilo lengo la kupunguza idadi ya watu maskini. Toka Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 4 mpaka asilimia 4.1, tunaposema sekta ya kilimo maana yake tunazungumzia *rural economy, rural growth.* Leo tunaambiwa kilimo kwanza, watu wanakumbuka shuka wakati alfajiri imefika, malengo mliojiwekea hamjayatekeleza, hamuelezi sababu zilizowafanya mshindwe kutekeleza malengo hayo na watu wanasema Ilani imetekelezwa kwa asilimia 100, nashangaa sana, takwimu za Serikali zinaonyesha tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Awamu ya Nne inachukua nchi hii, asilimia 11 ya watoto waliokuwa wanazaliwa walikuwa wanakufa kabla hawajatimiza umri wa miaka 5. Leo ninavyozungumza nanyi kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa Tanzania watoto 134 wanafariki kabla hawajatimiza umri wa miaka 5, tunapoteza watoto 800,000 kila mwaka. Mkoa wa Lindi una idadi ya watu 800,000. Ukitaka kujua idadi ya watoto wanaofariki dunia kabla hawajatimiza miaka 5 Tanzania angalia *population* yote ya Mkoa wa Lindi, mnasema mnatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Maternal Mortality Rate*, kina mama wajawazito wanaofariki dunia kwa matatizo ya uzazi. Katika kila wanawake 100,000 wanaopata ujauzito Tanzania wanawake 578 wanafariki dunia kwa matatizo ya uzazi. Takwimu hizi zinaonyesha kila saa inayopita katika nchi yetu kuna mwanamke mmoja amefariki kwa sababu ya matatizo ya uzazi, kila saa. Miaka 48 ya uhuru tunashindwa kulinda afya za mama zetu na ni takwimu za Serikali, mnatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

**WABUNGE FULANI:** Ndio!!!!!!!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 44 ya Watanzania, ni watoto walio chini ya umri wa miaka 15. *Median age* kwa mujibu wa *population* yetu yaani *half* ya Watanzania wako chini ya umri wa miaka 17, asilimia 44 ya Watanzania wako chini ya umri 15, kwa hiyo hii ni *a very young population*. Lakini takwimu za Serikali kwenye vitabu vya Serikali zinaonyesha kwamba asilimia 38 ya hao

watoto ni *stunted,* wamedumaa, kudumaa kutokana na masuala ya lishe. 38% katika kila watoto 10 wa Tanzania, watoto 4 ni *stunted*, tunajenga Taifa la namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijaiona hatua yoyote inayochukuliwa ku-*address* matatizo hayo ya kitakwimu, lakini haiwezekani kukawa na hizi *measures* kwa sababu tunapotunga sera, tunapotunga mikakati tunajiangalia sisi ambao hatupo katika lile kundi la 74% *of the poorest* katika Taifa letu ambalo ni wakulima, mnasema mnatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005, Ilani ya Uchaguzi iliahidi kuongeza ajira. Takwimu za Serikali zimeonyesha Watanzania 2,300,000 hawana ajira kabisa sio *informal* sio *formal,* Mkoa wa Kagera una watu 2,300,000. Ukitaka kujua idadi ya Watanzania ambao hawana kazi nenda uwanja wa Kaitaba kusanya watu wote wa Mkoa wa Kagera ndio Watanzania ambao hawana kazi 2.3 *million*, mnatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndio mambo ambayo tunategemea *in the run up to the election*, tunapoelekea uchaguzi, watu waliopewa nafasi ya kuongoza dola wajibu kwa wananchi. Hatujibu kwa kelele tu za kulalamikalalamika, tunajibu kwa takwimu na takwimu ni za Serikali kwa sababu Idara ya Takwimu iko chini ya Serikali, iko chini ya Wizara ya Fedha, kwa hiyo tunataka majibu haya, mikakati gani inayofanyika kuliokoa hili Taifa maana tunakoelekea ni kubaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, mwaka jana nilizungumza hapa taarifa ya *Poverty in Human Development Report* inaonyesha 78% ya Watanzania hawaaminiani. Katika kila Watanzania 10, ni 2 tu ambao wanaaminiana, Watanzania 8 hawaaminiani. Ndiyo maana watu hawalipi mikopo, ndiyo maana watu wakisikia vi-*scheme* vya ovyo ovyo kama DECI, wanakimbilia kwa sababu *they don't trust the systems.* Wanasiasa hawaaminiani ndio maana kumekuwa na makundi makundi ya kusemanasemana ya kulanianalaniana maana nimesikia juzi kuna Wabunge wanawalaani Mawaziri, Mawaziri wanakasirika, watu wanaambiwa kwamba wanapeleka miradi ya maendeleo kwenye Majimbo yao ni kwa sababu ya *lack of trust*. Tunajenga Taifa ambalo ni *societ fabrics* limekwisha kabisa, hivi ndio vitu ambavyo ningetegemea kwamba hotuba ya Waziri Mkuu iweze kuvi-*address*, tuna tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa natoka Biharamulo, nikapita Igunga pale gari yangu iliharibika nikakutana na Walimu wanalalamika wakaniletea Mkataba ambao wameingia na nimeupeleka kwa Mawaziri hapa waushughulikie na Kampuni moja inaitwa *Blue Finance,* siwezi kuwahukumu hawa kwa sababu sijapata nafasi ya kuwasikiliza na mimi ni mtu wa haki sana. Wamewakopesha Walimu shilingi 400,000/= riba asilimia 231, sababu wanachotakiwa kulipa ni shilingi 1,300,000. Nimempatia Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuona jinsi gani ambavyo Watanzania wanyonge kwa sababu ya ukosefu wa mfumo mzuri wa fedha, Walimu wanavyonyanyasika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa, Mheshimiwa Erasto Zambi, alizungumzia kuhusu Kampuni moja ya *Bayport* na akaweka ushahidi. Leo nimepita tu Igunga watu walivyo-*desperate* na nimempelekea Mheshimiwa Waziri na Mama Kombani ndio yuko anaisoma pale aweze kuona hali ambayo tumeifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu ufisadi. Kamati ya Bomani, nitaiomba kuinukuu katika masuala ambayo alisumbuliwasumbuliwa Dr. Slaa juzi hapa. Alisema hivi Kamati ya Bomani ilipendekeza hivi:-

*"Kwa kuwa malipo ya Dola za Marekani 132,000,000 yaliyofanywa na Benki Kuu kwa Netbank ya South Africa hayana uwiano dhahiri na mkopo wa Dola za Marekani 10,000,000 zilizokuwa zimekopwa na Kampuni ya Meremeta kutoka Netbank, Serikali ifanye uchunguzi kuhusu malipo hayo"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali ambayo Waziri Mkuu aliitoa mwaka jana, taarifa hiyo ukurasa 23, inasema:-

*"Uchunguzi wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali kupitia Benki Kuu kwa Kampuni ya Meremeta na Tangold unaendelea",* Julai mwaka 2008. Hiyo ni taarifa ya Serikali ambayo Waziri Mkuu ameitoa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Waziri Sumari anamjibu ovyo ovyo tu Mbunge hapa, tena Katibu Mkuu wa Chama kinachokua kuliko vyama vyote Tanzania, anamjibujibu tu, *What is a contradiction* kati ya taarifa ya Serikali na majibu ambayo Mawaziri wanayatoa. *CAG* anafanya uchunguzi kuhusu Meremeta na nilichokiomba ni kwamba Serikali isiingilie Sheria ya Ukaguzi inasema kwamba *CAG* ana uhuru wa kufanya uchunguzi wowote, *CAG* ame-*confirm* kwamba anafanya uchunguzi kuhusu Meremeta na tunaiomba Serikali isingilie mpaka taarifa hiyo inapokuja, lakini hapo hapo Serikali…

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mwongozo wa Kiti.

Kanuni ya 68 na pia ningepata utaratibu. Katika kuongea kwa Mheshimiwa aliyekuwa anachangia sasa hivi, sidhani kama ni uungwana. Ukiacha heshima aliyonayo na umri unavyokwenda, kitendo cha kusema Waziri anajibu ovyo ovyo, maana yake Serikali inajibu ovyo ovyo na kwa maana hiyo ni kutokufikiria majibu wanayoyajibu. Lugha hiyo ni ya kuudhi sana na haipaswi kuwa ni lugha ya Bunge na haipaswi kukaa ndani ya *Hansard.* Ninaomba maneno hayo ayafute na aombe radhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, nitamruhusu Mheshimiwa aendelee bila ya kuyatumia hayo maneno kwa sababu hayapendezi.

**WABUNGE FULANI:** Asiendelee!

**MWENYEKITI:** Naomba niendelee kuongea, asiendelee kuyatumia na yafutwe kwenye *Hansard*, naomba uyafute hayo maneno ovyo ovyo halafu uendelee kuchangia.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge hapa alitaka Mawaziri walaaniwe hakufuta kauli yake. Kuna Mbunge hapa leo asubuhi amemshambulia waziwazi Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa Hawa Ghasia, hakuna mtu aliyesimama kuweza…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Zitto, naomba ukae.

**MHE KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya sitayafuta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge usibishane na Kiti, nilichotaka ufanye ni kwamba ufute maneno yako halafu uendelee kuchangia, usianze kubishana na kuanza kutoa *reference* ya mambo yaliyopita, naomba ufute hiyo tu ovyo ovyo halafu uendelee kuchangia, tafadhali sana.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ambayo Waziri alimpatia Mbunge wa Karatu yalikuwa ni ya ovyo ovyo, nasimamia maneno yangu na niko tayari kwa lolote ambalo Meza itaamua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee sasa na mchango wako na hatua zaidi zitafuata kuhusiana na kauli yako hiyo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti - Mwongozo wa Kiti. Wakati Waziri Kivuli wa Wizara hii, alipokuwa anazungumza, alikatazwa kuzungumza baadhi ya mambo pamoja na Meremeta, leo inaruhusiwa tena lile lile alilokataza Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nadhani ni sahihi katika kumbukumbu kwamba Mheshimiwa Waziri Kivuli, alipokuwa akiongea masuala yote yaliyohusiana na Meremeta alitakiwa ayafute na yaondolewe kwanye *Hansard*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto Kabwe utamalizia bila ya kuyazungumza tena masuala hayo kwa sababu uamuzi ulikwishakutoka wakati ule kwamba hayo masuala hayatazungumzwa humu ndani.

Mheshimiwa Kabwe, endelea.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamalizia kwa mambo mawili ya mwisho kwamba lazima ifikie wakati tuhuma mbalimbali za rushwa kubwa zinapotoka, Serikali iweze kuchukua hatua kuhakikisha mambo haya yanakwisha kwa sababu mnapokuwa mnazungumzazungumza kila wakati mambo haya hasa kwa kuzingatia kwamba Taifa letu lina watoto wengi sana, tunarithisha vitu vibaya sana kwa watoto na matokeo yake badala ya kujenga Tanzania imara iliyo moja, tunajenga Taifa ambalo tutakuja kuitwa *fisadistan, Republic of Fisadis,* kitu ambacho mimi nisingependa tujenge Taifa la namna hiyo. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuchukua hatua muafaka

kuhakikisha kwamba hoja zote ambazo Wabunge wanazitoa kuhusiana na masuala ya rushwa kubwa kubwa, zinashughulikiwa ili tufike mwisho na tuweze kufanya mambo mengine ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nilikuwa nasoma kitabu cha Mwalimu Nyerere, ukurasa 94 na sijui, ni kitu ambacho tunaweza tukakijadili namna gani kwa sababu imekuwa ni *tendency* ambayo hata imepelekea Serikali kuweza kushindwa kuchukua baadhi ya maamuzi, ya kuwasema Watendaji wa Serikali yaani *(Civil Servants).* Tarehe 12 Oktoba, Mwalimu alikuwa anafungua Bunge la kwanza la Tanganyika alisema hivi, nanukuu:-

*"Most important of all Members must not under any circumstances attack a Member of Civil Service in this House. If they believe a Civil Servant is acting wrongly and that in justice is inconsequence being done, it is the Minister whom Members must call to account, then his task is to investigate and if necessary to invoke the displinary procedures against the government Servant"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na utamaduni toka Bunge hili la Tisa limeanza kwamba tumekuwa tuki-*attack* sana *Civil Servants* watu ambao hawana fursa ya kujitetea humu ndani na hata imepelekea baadhi ya Maazimio ya Bunge ambayo yalikuwa yanawataja moja kwa moja *Civil Servants* kushindwa kutekelezwa kwa sababu ya taratibu za uendeshaji wa *Civil Service* jinsi ulivyo.

Nilikuwa naomba tujaribu kuangalia kama Bunge kama hotuba hii ya Mwalimu hasa kipengele hiki ambacho nimekinukuu wakati anazindua Bunge kinaweza kikawa ni sehemu ya Kanuni za Bunge ili kuhakikisha kwamba wale ambao ndio *front bench* wanakuwa *responsible* kwa matendo yote ambayo watu wao wanakuwa wanayafanya ili iwe rahisi zaidi utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Kiserikali, kuweza kutumika…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako ume-*expire*.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti - kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Kabwe alipokuwa anachangia alilitaja jina langu kama Erasto Zambi, jina langu ni Godfrey Zambi na naomba *Hansard* isome hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zambi.

Waheshimiwa Wabunge muda tulionao ni kama dakika 10 sasa sidhani kama Mheshimiwa Jacob Shibiliti unamtosha huu?

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Hautoshi Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MBUNGE FULANI:** Nipe mie unanitosha.

**MWENYEKITI**: Sawa basi mimi nachukua mamlaka tu ya Kiti kuamua kwamba muda huu hamtoshi Mbunge yeyot sio yeye peke yake tu na kwa maana hiyo napenda kwanza nitoe matangazo yaliyopo mezani kwangu.

Kwanza napenda kuwatangazia tena Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba kuna kikao hivi sasa tukimaliza tu hapa kinafanyika katika *Speaker's Lounge* ya ukumbi mpya na vile vile naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhusu onyesho la filamu ya *Crimpson Winds* lipo leo saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Mnakumbushwa kwa wale ambao mtapenda kwenda kuangalia hiyo filamu.

Waheshimiwa Wabunge, wakati ikitolewa Kauli ya Serikali hapa, nilipata *notes* nyingi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba ilikuwa imetumia muda wao wa kuchangia. Lakini napenda tukumbushane kwamba kwa mujibu wa Kanuni 49, ile ni kauli halali na inatolewa na Serikali na ipo mara baada ya maswali. Kwa hiyo, watu wasiwe na wasiwasi kwa sababu mijadala kuhusiana na hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Tawala za Mikoa, majadiliano bado yanaendelea, wale wote ambao wamepangwa ambao watazungumza katika kipindi husika watapata. Wasiwe na wasiwasi Kauli za Mawaziri zimo kwenye shughuli za leo kwenye *order paper*, kwa hiyo ilikuwa ni halali. Kwa maana hiyo, napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka jioni saa 11.00.

*(Saa 06.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipohitimisha shughuli za mchana, Mwenyekiti, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, alinikabidhi orodha ya wale ambao watachangia jioni hii. Kwa hiyo, nitawaita watatu wa kwanza kwa kujiandaa. Mheshimiwa Jacob Shibiliti ataanza, atafuatia Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, hatimaye Mheshimiwa Eng. Laus Mhina.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili angalau niweze kufikisha mawazo ya Wananchi wangu wa Misungwi kwa Serikali yetu, ambayo ipo madarakani. Bahati mbaya, simwoni Mheshimiwa Waziri Mkuu, sasa sijui yatamfikia kwa njia hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru wewe, ambaye umekuwa msaada mkubwa kwa Bunge hili kutokana na umahili wako, jinsi unavyoweza kuongoza na kuweza kusimamia shughuli za demokrasia katika nchi yetu ya Tanzania. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ameonesha umahili mkubwa kwa kipindi kifupi ambacho amekuwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo ni hali moja ya heshima ya juu sana katika majukumu yake ambayo ni makubwa kwa taifa letu. Niwapongeze Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wengine

wote, bila kuwasahau Wakuu wetu wa Mikoa, ambao ni Viongozi wanaotusaidia sana katika maeneo ya Mikoa yetu. Nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, timu hii ya Mawaziri ni kama timu ya mpira, ambayo inacheza ndani ya Chama cha Mapinduzi, maana Serikali ni ya Chama cha Mapinduzi. Kutokana na hali halisi ya jinsi wanavyocheza, mimi niseme kwamba wanacheza vizuri; yapo mengi wameyatekeleza tunayaona na yapo ambayo yanahitaji masahihisho tutayasema wayavumilie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilisema kwamba, Wakulima wa Zao la Pamba walianza kuuza zao lao kuanzia shilingi 450 mpaka 550 na bei iliendelea hivyo. Wafanyabiashara nao baadhi walikuwa wameshauza pamba yao kwa maana ya *foward sale* na shughuli iliendelea, lakini baadae imekuja kuonekana wamepata hasara na Serikali yetu imeweza kuwafikiria na baadae kuwafidia hasara hizo ili waweze kuendelea na ununuzi wa pamba na naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika hali hiyo, mwaka jana kilo za pamba mbegu zilizonunuliwa zilikuwa milioni 365. Safari hii zitapungua kidogo kutokana na hali halisi, nadhani itategemea labda inaweza ikafikia kwenye milioni 320. Walipokuwa wanauza, iliwapa moyo kutokana na ile bei waende shambani. Kazi ya Zao la Ppamba ni ngumu sana kuliko mazao yoyote yale, gharama zao tu ziko mpaka kwenye shilingi 380 mpaka 400. Juzi imetangazwa bei shilingi 360, wanakula hasara wakulima hawa. Nakuomba sana Serikali ikubali kutokana na mapendekezo ya Bodi ya Pamba na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamechangia hapa, Serikali iweze kufikiria kuwaongezea ile shilingi 100 ili waweze kufikisha shilingi 450. Hiyo itawafanya hawa wakulima waendelee kulima Zao la Pamba. Hili ni zao lenye matatizo makubwa sana, kwa hiyo, niiombe sana Serikali iweze kuliona hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha ana-*wind up,* alitaka kujibu kwa maana ya kuwa yupo tayari, lakini akasema kwamba, baadae atashauriana na Serikali. Kwa umahili wa Waziri Mkuu, nina imani watakaposhauriana, tutapata jibu ili wakulima wetu waweze kufaidika na Zao la Pamba. Ili Zao hili lifanikiwe, kuna mambo mbalimbali ambayo yanahusika inabidi yatekelezwe. Tuna Chuo cha Ukiriguru, nimekuwa nikiwasemea hapa mara kwa mara, kuna watafiti pale wana matatizo makubwa sana ya maji. Wanaohusika ni Waziri wa Kilimo na Hazina. Imekuwa ni danadana ya muda mrefu; namuuliza Waziri Mkuu; hivi tatizo ni nini pale Ukiriguru mbona wananchi wanateseka hivyo?

Upande wa mafunzo, kuna wanafunzi wasiopungua 300 wataingia pale. Mkuu wa Chuo huwa anachukua lori la Chuo kufuata maji Mwanza mara mbili kwa siku. Tunataka Maafisa Ugani hao. Nipate majibu, haiwezekani kuwatesa wanafunzi, watafiti na familia zao katika hali hiyo. Tupate majibu ni nini kimekwama na ni kwa sababu ipi?

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Halmashauri zetu, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Kombani ni mama ambaye anajitahidi sana. Alipoitembelea Wilaya yetu ya Misungwi, nilimweleza matatizo mbalimbali, ikiwemo barabara yetu ya kutoka Mitindo -

Mondo - Mwanika. Aliahidi ataishughulikia na bahati nzuri yeye mwenyewe, alinitamkia kwamba, kuna shilingi milioni 60 tayari wameshanitumia. Cha ajabu, sijaziona hizo pesa. Kuna matatizo kwenye Ofisi yake, kwa upande wa mainjinia waliopo hapa na mhandisi kule Wilayani kwangu. Serikali inasikia, hawa watu ni wa kuwachukulia hatua mara moja. Haiwezekani Wananchi wa Mondo na Mwaniko wateseke, kwa sababu ya watu wachache. Mheshimiwa Waziri Mkuu, umetamka mwenyewe kwamba, umetoa pesa; kwa nini zipotee hizo pesa?

Fuatilia ili wananchi hao waweze kupata haki yao, sambamba na barabara yetu ya kutoka Kabale kupitia Ng'obo kwenda Mwamboku; tangu ujio wa Mtoto wa Mfalme wa Norway, barabara hiyo haijatengenezwa na nimezungumza hapa hakuna kinachoendelea. Hivi tutakuwa tunatengeneza barabara wanapokuja watoto wa Wafalme tu? Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ichukue jukumu hilo na itekeleze mara moja. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulipoahirisha Bunge kipindi kilichopita, sisi Wabunge wa Mkoa wa Mwanza, tulipata fursa ya kwenda Busanda kusimamia masuala ya uchaguzi. Bahati nzuri, sisi tulipokuwa tumesimamia upande wetu wa Chama cha Mapinduzi, tuliibuka na ushindi wa kishindo na baadae kumpata Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na sasa tunaye hapa Bungeni. Wananchi wa maeneo ya Chigunga niliyokuwa nayasimamia, waliniwasilishia matatizo yao, nina imani Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atakapopata nafasi naye atayazungumza baadhi, lakini nichukue nafasi hii kumsaidia angalau kumsemea. Ile barabara ya kutoka Inyala kwenda Katoro ni tatizo kubwa sana. Tuiombe sana Serikali, imsaidie Mheshimiwa Bukwimba, barabara hiyo iweze kupata pesa ili wananchi wa Maeneo ya Chigunga, Nyachiluluma na Bukondo, waweze kufaidika na barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wetu, Mheshimiwa Kawambwa, yapo maeneo anajitahidi sana; barabara yetu kutoka Mwanango kwenda Misasi mpaka Salawi imetengewa pesa kidogo. Nilikwenda kumwona Katibu Mkuu, alijaribu kufuatilia baadae akaona kuna makosa yamefanyika na akaniahidi ataongeza pesa ili barabara hiyo itengenezwe. Kwa hiyo, hapo sina matatizo nawapongeza na waendelee na utaratibu huo.

Barabara ya Kisesa kuja Usagara imekuwa kwenye upembuzi yakinifu usiokwisha, imefikia mahali sasa wamekamilisha, lakini mbaya zaidi kuna *valuation* mle itakamopita barabara. Wananchi wangu wana shida na hawajui watalipwa lini; sasa ni mwaka mzima wameshafanyiwa *valuation* kwenye nyumba zao na mashamba yao, lakini hakuna malipo yaliyofanyika. Pesa zitakazopatikana watalipa kwa *valuation* ipi kama muda umeshapita namna hiyo?

Niiombe Serikali itakapoamua kulipa, ifanye *valuation* upya na iweze kuwalipa wananchi mara moja ili waweze kuamua vinginevyo, kuliko kuendelea kusumbuliwa kwa utaratibu huo. Tuelezwe mambo yanakwendaje katika upande huo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie eneo la afya; nimekupongeza kutokana na umahili wako wewe mwenyewe, pamoja na Ofisi yako, hasa katika suala la afya za

Wabunge na wananchi wengine kwa ujumla. Ofisi yako imekuwa ikitujali tunapopata matatizo, mimi ni mmojawapo ambaye nimekumbwa na matatizo ya binti yangu Agnes Shoma, Ofisi yako ilinisaidia na baadaye nikampeleka kwenye matibabu na hali yake inaendelea vizuri. Kwa kuwa mazoezi ya Mwenyezi Mungu yapo tu kila leo; ni hivi majuzi tu kijana wangu mmoja aliyekuwa anatoka shule Kahama, alipata ajali akavunjika mkono, anaitwa Manoni na mpaka sasa bado yupo Bugando Hospitali. Tunawashukuru sana wataalamu wetu, wanajitahidi sana. Tusipoishukuru Sekta ya Afya, basi hatuna shukrani. Wanajitahidi sana, katika mazingira magumu sana. Niimbe Serikali, iwafikirie katika suala la mishahara na mapoto yao mengine madogo madogo. Wanafanya kazi kwenye mazingira magumu wafikiriwe na waongezewe vitendea kazi. Matokeo yake, tunapeleka watu nje ya nchi. Kwa hali hiyo, hawa wakishawekewa vitendea kazi, watafanya kazi kutokana na hali ya elimu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la maji. Nimpongeze Waziri wetu, Mheshimiwa Mark Mwandosya, ni mtu ambaye anajituma na anajali matatizo ya wananchi. Kama alivyoeleza yeye mwenyewe, amefuatilia kwa karibu masuala ya maji katika Mji wa Misungwi, hali kadhalika, mradi wetu wa kwenda Kahama na Shinyanga. Ninayo maji Misungwi, sitaki nikusumbue Mheshimiwa Waziri, kwa sababu mara kwa mara tumekuwa karibu na wewe na Watendaji wako wamenihakikishia kwamba, kufikia Jumamosi mabomba yataanza kupelekwa kwenye Mji wa Misungwi na tayari yameshawekewa dawa ili yasipate kutu haraka. Kwa hiyo ni utendaji ambao inabidi tukupongeze Mheshimiwa Waziri, unafuatiliwa kwa karibu sana. Kitu kikubwa ambacho ningependa niiombe Serikali, hasa ndugu yetu Ngeleja, TANESCO itatuangusha katika mradi huu kama asipokaa makini.

Sasa hivi watu wa TANESCO wanategemea kutafuta mkandarasi mwingine wa kujenga njia ya umeme kuanzia Nyapilinga kwenda Nyahiti. Tumshauri yeye kwa kutumia mafundi wake wa TANESCO, wachukuliwe waliopo Misungwi na Mwanza, wajenge wao wenyewe ili waweze kuwaokoa Wananchi wa Misungwi ili waweze kupata maji kwa kipindi kifupi zaidi. Mheshimiwa Mwandosya, naomba uzipokee pongezi zisizo na mfano katika utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mifugo. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 31, mstari wa nane amesema: “Serikali haipendi kuona migogoro hii ikiendelea, kwani inapotokea huambatana na madhara makubwa ambayo wakati mwingine husababisha kupotea kwa mali za wananchi.” Baada ya maelezo hayo; ni hivi majuzi wananchi kutoka maeneo ya wafugaji walikuja kwako na Waziri alipata nafasi ya kutoa tangazo lake humu kwa ajili ya kuahirisha masuala ya kuwafukuza wafugaji katika maeneo yao.

Tayari wafugaji hao walikuwa wameshapoteza mamilioni ya pesa. Sikuona katika kitabu hiki mahali popote ambapo amezungumzia kuhusu kurudisha pesa zao, maana zile pesa hazijawa za Serikali. Mkurugenzi wa Kilosa, amechukua milioni 40 kwa mtu mmoja na risiti tuliiona, inabidi zirudishwe moja kwa moja kwa muhusika. Wamenyang’anywa ng’ombe wakaonekana kwa mtu fulani. Sasa hilo nalo tunachukua muda upi? Waelezwe wafugaji hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, katika Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Busanda, kwa kunichagua. Wamenipa heshima kubwa na mimi nichukue nafasi hii kusema kwamba, nitatumia uwezo wangu wote na nguvu zangu zote, kuwatumikia Wananchi wa Jimbo la Busanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pili ziende kwa Chama changu cha Mapinduzi; ni Chama kizuri na ninakishukuru kwa sababu kimeniteua. Kupitia Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi na niseme kwamba, ahsanteni sana. Shukrani zangu za pia ziwaendee Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, walishiriki pamoja nami kwa hali na mali katika kipindi chote cha kampeni katika Jimbo la Busanda; na niseme ushindi huu umetokana na nguvu zenu na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi, sasa nichukue nafasi hii kuzungumzia masuala mazito yanayotekea katika Jimbo la Busanda. Kwa kipindi kirefu, Busanda kumekuwa na tatizo kubwa la umeme na hii ni kero kubwa sana kwa Wananchi wa Busanda. Nichukue nafasi hii, kulisemea suala hili kwa sababu wananchi wamenituma na mimi nimesimama hapa kuwawakilisha Wananchi wa Jimbo la Busanda. Ninaiomba Serikali, ichukue hatua madhubuti katika suala hili la umeme kwa kuwa ni la muda mrefu. Jimbo hili tangu uhuru halina umeme wakati Majimbo yanayolizunguka kama Jimbo la Geita na Jimbo la Kahama yote yana umeme. Kwa hiyo, Jimbo la Busanda limekuwa kama kisiwa. Ninaomba Serikali inisaidie katika suala hili. *(Makofi)*

Ninafahamu kwamba, kuna mpango mzuri tu wa kuleta umeme katika Jimbo la Busanda na umeme huo unapita katika Kijiji cha Bukoli, Nyarugusu, Lwamgasa na Katoro. Mipango hiyo ipo, lakini ninaomba Serikali iharakishe utekelezaji wa mpango huu, kwa kuleta umeme katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni suala la wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Jimbo la Busanda tumebarikiwa sana, kwa sababu eneo letu lina madini ya dhahabu karibu asilimia 30 au 50 ya ardhi ina madini ya dhahabu. Sisi Wananchi wa Busanda, tunajivunia sana kutokana na dhahabu kwa sababu inatuletea kipato kwa wananchi ambao ni wachimbaji wadogo. Niseme kwamba, katika Jimbo la Busanda, suala la wachimbaji wadogo limekuwa ni kero sana na kwa sababu wananchi wa Jimbo hili hasa katika maeneo yenye migodi ya dhahabu, ambayo ni Nayakagwe, Nyarugusu, Lwamgasa, Kaseme na maeneo ambapo ni majirani kama Katoro; ni maeneo ambayo tunategemea machimbo haya.

Maeneo waliyotengewa wananchi waliopewa leseni hayawatoshi, mimi kama Mwakilishi wao, ninasimama hapa kuiomba Serikali iwaongezee maeneo wananchi hawa ili waweze kufaidika na kuinua hali za maisha yao kiuchumi. Wananchi hawa, uchumi

wao unategemea uchimbaji mdogo mdogo. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali itazame suala hili kwa umakini na utekelezaji ufanyike kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na wachimbaji wadogo wadogo, nadhani sote kwa muda mrefu tumekuwa tukisikia mara mgodi umeanguka watu wamekufa ndani ya mgodi; ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu, inisaidie mikopo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo ili waweze kununua vifaa vya kisasa vya kuchimbia na hapo tutaweza kuinua hali zao za kiuchumi.

Katika hayo masuala mawili, ninaiomba rasmi Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala haya mawili iyape kipaumbele sana, kwa sababu muda wenyewe ni mfupi. Naiomba Serikali izingatie suala hilo na mimi nipo tayari kufanya kazi bega kwa bega na Wananchi wa Busanda kuhakikisha kwamba, maendeleo yanakuwepo katika Jimbo letu la Busanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambapo hata Mheshimiwa Shibiliti ameyazungumzia, lakini kuna mengine ambayo hayajazunguzwa kama suala la elimu. Jimbo la Busanda ni sehemu ambapo kuna mila na desturi, kwa wasichana kutokuzingatia suala la elimu; na kwa vile Serikali imetujali sana, imejenga Sekondari na katika Sekondari hizo unakuta kijiji kimoja kiko mbali sana na shule hiyo; inasababisha wasichana wengi kwenda kupanga katika nyumba ambazo hazina usimamizi mzuri na hili husababisha mimba kwa watoto hawa. Tunashukuru kama watapata mimba tu, kwani wakati mwingine hata UKIMWI wanaupata. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu; katika zile shule za sekondari za wasichana zilizoko Busanda, yajengwe mabweni ili kurahisisha usimamizi wa watoto hawa kwa kuwa bado ni wadogo sana, hawawezi kujisimamia wao wenyewe. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali inisaidie suala hilo, kwa kuwa ni tatizo ambalo wananchi katika Jimbo langu ni kilio chao kikubwa sana. Ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu, inisaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la maji katika Jimbo la Busanda na kwa kuwa tumezungukwa na Ziwa Victoria katika sehemu ya Bukondo, ninaiomba Serikali kama ilivyopeleka maji katika Vijiji vya Misungwi, inisaidie katika Jimbo langu, kwa sababu Ziwa lipo kama km 10 au 20 kutoka Bukondo. Serikali inisaidie kunivutia maji kwenye Kata za Katoro, Butundwe, Nyakagomba, Nyachiluluma, Nyakamwaga na Kamena ili wananchi wangu wafurahie kuwa karibu na Ziwa. Kama ambavyo Wananchi wa Misungwi wanafaidika na sisi pia katika Jimbo letu, tufurahie huduma hii ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishie hapo, niseme kwamba, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani tutakubaliana hapa kwamba, tumepata Mbunge safi; anapanga *points* zake vizuri, zinaeleweka na anatunza muda. Hongera sana *maiden, speech* nzuri kabisa hiyo. Sasa namwita Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nataka nianze kwa kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Nne, kwa juhudi zake inazozifanya katika nyanja nzima ya kuendeleza maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mila zetu za Tanga kuna usemi unaosema shukuru na kidogo hata ukipewa kikubwa pia wewe shukuru. Kwa hiyo, mimi nataka nishukuru, kwa yale ambayo tumefanyiwa na Serikali yetu ya Awamu ya nne hadi sasa. Hii haina maana kwamba, ndiyo tumefikia mwisho wa kuomba, tutaendelea kuomba, lakini hatutalalamika.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mdogo tu katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini, jinsi tulivyofaidika kwa miradi mingi katika awamu hii. Kwanza, kwenye barabara za vijijini tunasema *Alhamdulillah,* leo hii nyingi zinapitika ukilinganisha na siku zilizopita. Kwenye kilimo cha umwagiliaji huko ndio usiseme. Suala la njaa si kana kwamba tumemaliza Jimbo zima, hatutakuwa na njaa lakini baadhi ya maeneo mengi njaa itakuwa kidogo imetupita. Kwa hili tunasema, ahsante sana kwa Awamu hii ya Nne.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye ujenzi wa majosho, kwa wenzetu wale wafugaji baadhi ya sehemu nyingi majosho yemeenea leo hii ukifika kwenye Jimbo la Korogwe Vijijini. Ukija kwenye ujasiriamali, vikundi mbalimbali vimeundwa. Kwa upande wa huduma ya jamii kwa ujumla au huduma ya afya, hatusemi kwamba imeboreka asilimia mia moja, lakini hali ambayo tunayo leo ukilinganisha na miaka iliyopita, ninaweza kusema tumesogea kwa hatua nyingi tu mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda, nianze kutoa mchango wangu kwa upande wa kilimo. Nimefurahi sana, kusikia kwenye hotuba hii kuwa, Serikali imeondoa ongezeko la thamani katika zao la chai.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini, hususan maeneo ya Milimani, tunategemea sana Zao la Chai. Kuondoa ongezeko la thamani, kutamfanya mkulima ajisikie kwamba, kipato chake kimepanda. Vilevile tunashukuru kuondolewa ushuru wa pembejeo za kilimo. Isitoshe pia tumepunguziwa hata ushuru wa mazao kutoka asilimia tano hadi kufikia tatu. Haya hayana budi kupongezwa. Hatuna budi kuipongeza Serikali yetu, kwa inavyomjali mkulima.

Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, inawezekana kabisa kutekelezeka endapo machache yafuatayo yatapewa kipaumbele:-

Kwanza, tutoe kipaumbele kwenye matumizi mazuri ya wataalamu. Pili, tukiboreshe kilimo cha umwagiliaji. Tatu, tujitahidi kupunguza bei ya zana za kilimo. Tufike mahali tuwatumie vizuri wataalamu wetu, kwa maana kazi zao wazifanyie mashambani, wasikae maofisini. Kuwe na mashamba darasa, yatakayomfanya mkulima aelewe maana ya kilimo bora ni nini, kwa sababu atakiona kwa vitendo mwenyewe. Ataona ni jinsi gani Mbolea yetu ya Minjingu inavyotumika vizuri. Leo hii tunasema Mboela ya Minjingu ni mbaya, lakini inawezekana kabisa kwamba, huenda ni matumizi

mabaya ndiyo yanayosababisha mbolea hii ikaonekana ni mbaya, kwani mbolea hii hii katika nchi za wenzetu jirani, inasemekana kwamba ni nzuri. Sasa inawezekana ni kutokana na matumizi mabaya tu, lakini tunapofanya mashamba darasa na tunapotumia vizuri wataalamu hawa wa kilimo, inawezekana kabisa mbolea hii ikaonekana ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa kilimo cha umwagiliaji, mimi nataka niipongeze sana Serikali yetu ya Awamu ya Nne; skimu nyingi sana zimejengwa katika nchi yetu hii kwenye mabonde mengi. Nikichukulia mfano tu, kwa upande wa Jimbo langu la Korogwe Vijijini, kuna skimu karibu 14 katika mabonde yetu machache. Kwenye Bonde la Mto Lengela, kuna skimu nyingi kuanzia Kata ya Kerenge, Kata ya Kwagunda, Kata ya Magoma, Kata ya Mombo na Kata ya Makuyuni kote huko zimejaa skimu za umwagiliaji. Leo hii suala la uzalishaji wa mpunga, ambao tumezoea kuzalisha eka moja, sana sana mtu amepata anapata magunia matatu, manne, matano au sita, sasa tunafikia hatua ya kupata magunia mpaka 34. Hii ni hatua nzuri sana, ambayo tumefikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya sifa zote hizi, sitasita kuzungumzia kuhusu ujenzi wa bwawa katika Bonde la Mto Mkomazi. Kulikuwa na mpango madhubuti wa kujenga bwawa la umwagiliaji katika eneo au kijiji cha Manga-Mikocheni. Mradi huu ulibuniwa takriban miaka 30 iliyopita na nimekuwa nikiuongelea karibu kila kipindi cha bajeti, lakini bahati mbaya hakuna majibu ambayo napatiwa. Haya ni masikitiko makubwa kwa Wakazi wa Korogwe, kwa sababu tunapoteza unywesheaji wa bonde lenye takriban eka 11,000. Nadhani hapa inafahamika ni tani ngapi za mpunga tunazozipoteza.

Mheshimiwa Spika, nadhani sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, labda atupatie majibu thabiti kuhusu mradi huu; je, upo au haupo kuliko kuweka roho za Wananchi wa Korogwe Vijijini juu kwa kitu ambacho hatuelewi na tukiuliza hatupati majibu yake?

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu punguzo la bei ya zana za kilimo. Mkulima mdogo, zana kubwa ambayo anaitegemea hivi sasa ni matrekta madogo kwa maana ya *power tiller*. Ikumbukwe kwamba, katika kipindi cha mwaka uliopita, ilikuja kampuni moja hapa katika viwanja vyetu vya Bunge, wanajiita Farm Equipment. Tukayaona matrekta yale, tukahamasika na tukaenda kuwaeleza wananchi wetu, wakahamasika hata baadhi ya Wabunge tukahamasika na tukaweka pesa zetu kama *advance* ya kupatiwa matrekta yale. Wakati ule tuliambiwa yanauzwa kwa shilingi milioni 5.5. Baada ya takriban miezi sita/saba/nane, hata mwaka mmoja haukufika, matrekta yale tunaambiwa yanauzwa kwa dola 8,000. Hii ni sawa sawa na ongezeko la asilimia 100, kwa maana ya shilingi milioni 11,000. Sidhani kama kweli nia yetu hapa ni kumnufaisha mkulima mdogo! Mkulima mdogo atazipata wapi shilingi milioni 11,000 kwa wakati mmoja? Mimi nadhani hamasa hiyo wameipata, baada ya kuona wananchi wengi wamekwishaingia kwenye mstari au kwenye *line* ya kuhamasika kununua matrekta haya na *demand* imekuwa kubwa, sasa wakaingiwa na tamaa ya pesa. Naiomba Serikali iliangalie hili kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, niingie kidogo kwenye TAMISEMI. Awali ya yote, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, pamoja na Wasaidizi wake, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa jana. Pamoja na mengi tuliyoyasikia, binafsi nimefarijika sana, kusikia kwamba, Waheshimiwa Madiwani wamejumuishwa katika Mradi mzima wa Bima ya Afya. Haya ni maendeleo ya hali ya juu. Vilevile posho zao zimeongezwa na isitoshe wametolewa punguzo la kodi wanapohitaji kununua vifaa vyao vya usafiri. Haya yanaonesha wazi ni jinsi gani Serikali yetu inawathamini Wawakilishi hawa wa Wananchi katika ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Spika, upande wa barabara ambazo nyingi ziko katika Mamlaka hii ya Serikali za Mitaa, kwa kweli nyingi zimefanyiwa matengenezo ya kutosha, nikiongelea hususan katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini, lakini bado juhudi kubwa inahitajika. Nikitoa mifano ya mafanikio ya barabara katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini; leo hii Wananchi wa Bungu, haitawawia vigumu tena kuleta mazao yao, kwa sababu imetengenezwa barabara mpya kabisa ya kutoka Makuyuni kupitia Mbaghai hadi Zege. Leo hii Wananchi wa Kata ya Lutindi, hawatakuwa na matatizo tena ya barabara, kwani Barabara ya Kwabluu hadi Msambiazi, imetengenezwa na inapitika vizuri tu. Barabara ya Kizara – Kwetonge, ambayo kwa miaka mingi ilikuwa imesahaulika, imetengenezeka na inapitika vizuri sana. Barabara nyingi katika Kata za Dindila, Bungu, Vugili, Kwa Bunda na kwingineko, zinapitika.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo tunaliona kwa upande wa barabara ni upungufu wa pesa za kutosha kwenye Miradi ya Barabara. Pesa zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu ni kidogo sana kwa ajili ya barabara. Isitoshe, bahati mbaya hata hizo kidogo wakati mwingine hazifiki kwa wakati muafaka na wakati mwingine hazifiki kabisa katika kipindi chote cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mifano michache tu; katika Mfuko wa Barabara *(Road Fund)*, zilitengwa kiasi cha shilingi milioni 65, lakini zilizofika hadi kufikia Machi ni shilingi milioni 34.4 tu, ambayo ni asilimia 52. Hiki ni kiasi kidogo. Bahati mbaya, utakuta Halmashauri hazikufanya kazi zake inavyotakikana.

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye Programu ya Usafiri, Serikali za Mitaa kwa maana ya LGP, zilitengewa shilingi milioni 23, lakini kiasi kilichopatikana ni cha kusikitisha; ni milioni tano tu, kwa maana ya asilimia 22. Halmashauri nyingi hazikupata kabisa pesa hizi. Halmashauri yangu ya Korogwe ni mojawapo, haikupata hata senti tano. Sasa hatuelewi, pesa zile ambazo zilipangwa wakati wa bajeti zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, ukija kwenye Programu ya Usafiri na Uchukuzi Vijijini, kwa maana ya VTTP, zilitengwa shilingi bilioni 1.9, lakini zilizopelekwa ni shilingi biloni 1.1. Pesa hizi Halmashauri nyingi hazikupata pia, Korogwe Vijijini ikiwa mojawapo. Mimi ningeiomba Serikali yetu, tunapopanga bajeti hapa, basi tuhakikishe kwamba, tunapanga kitu ambacho kinatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo upande wa maji. Naishukuru Serikali yetu, hali ya maji sio mbaya sana katika Wilaya yetu ya Korogwe. Najua kabisa kwamba,

kuna maeneo, kwa mfano, Gemai au Toronto Mbugani, hali haijawa nzuri, lakini maeneo mengi yamepata maji ya visima. Tumetengenezewa visima karibu 36 katika Kata mbalimbali katika Jimbo langu la Korogwe Vijijini.  Isitoshe, kuna Mradi mkubwa wa Kusambaza Maji Mji wa Hare, ambao nafikiri kufikia mwezi wa Saba, Mji wa Hare utakuwa hauna tatizo la maji tena.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu kidogo katika hii *speech* ya Waziri Mkuu, hali kadhalika *speech* ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwanza kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Lolesia, kwa *speech* yake nzuri aliyoitoa. *Experience* inaonesha kwamba, pamoja na kuwa una siku chache sana Bungeni, umefanikiwa kusimama na kuzungumza kwa kujiamini sana na kutoa hoja za wananchi wako.  Hiki ni kitu kizuri.  Wenzio wamekaa miaka miwili, wanashindwa kusimama, kwa hiyo, ni *achievement* kubwa sana.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niingie rasmi kwenye mchango wangu. Mwaka 2005, tulipokwenda kujiuza kwa wananchi kwa maana ya kuomba kura, kila chama kilikuwa na ilani yake na kimsingi ilani huwa inakaa miaka mitano kwa mantiki kwamba, kama umewaahidi Watanzania ndani ya miaka mitano nitawatekelezea kadha wa kadha, hii inamaanisha kwamba, ndani ya kipindi hicho unawajibika kurudi kwa wananchi kuwaambia kwamba, nilikuja kwenu, nikawaahidi hiki na kile, nimekitekeleza kufikia hapa. Sitarajii ilani yoyote kuwa inatungwa kwa madhumuni ya ku-*last* miaka 20, natarajia ni miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika matarajio yangu ya kawaida, mwakani ni 2010, ndio uchaguzi, nilifikiria kwa dhati kabisa, kwanza wakati Mheshimiwa Mkulo anawasilisha bajeti yake; pili, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu, bajeti yake; watuambie kwa ufasaha kati ya zile ahadi nyingi sana ambazo Mheshimiwa Rais aliziahidi ndani ya ilani na nyingine za papo kwa papo, zimefikia wapi kwa sababu mwisho wa siku ule ushindi wa kishindo aliupata kwa sababu ya zile ahadi?

Mheshimiwa Spika, nitatoa mifano michache, ambayo kwa uchache wake hazitimii zile ahadi 144 alizozitoa. Nitatoa mifano michache nikitarajia kwamba, hii labda inaweza ikawa *sample* ya mifano mingine, ambayo imetekelezwa ama la. Suala langu la kwanza, linahusiana na suala zima la umeme.  Mheshimiwas Rais, alipokuwa Ruvuma tarehe 29 Agosti, 2005, alitoa ahadi kwamba, ndani ya miaka mitano atahakikisha kila Wilaya ya Tanzania hii inakuwa na umeme.  Mwaka mmoja huu umebaki, leo hii taarifa ya umaskini na hali ya uchumi, *latest addition*, inaonesha kwamba, katika Wilaya 118 zilizotembelewa, Wilaya 31 hazina umeme kabisa.  Sasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiye Mtendaji Mkuu Serikalini, akija atueleze ndani ya huu mwaka mmoja uliobakia ile ahadi ya Mheshimiwa Rais inatekelezeka ama Watanzania walikuwa wakiingizwa mkenge wapige kura halafu siku zinazidi kusonga mbele?

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili; Mheshimiwa Rais alipokuwa Tunduru – Ruvuma tarehe 26 Agosti, 2005, alisema kwamba, ndani ya kipindi chake cha miaka mitano, atahakikisha kila Mtanzania anapata maji safi ndani ya umbali wa mita 400 kutoka nyumbani kwake. Maji safi na salama, maana sio safi peke yake. Ninatarajia nitapata hayo majibu.

Hali kadhalika aliahidi kwamba, atahakikisha anajenga barabara ya lami kutokea Mtwara – Lindi kuunganisha na Mwanza. Wote mna majibu; Wabunge wa Singida wako hapa wanajua, ndani ya miaka mitano watu wenye hela waweze kwenda kustarehe. Alisema hivyo Mheshimiwa Rais, siyo kwamba ni maneno yangu. Sasa natarajia Mheshimiwa Waziri Mkuu atanijibu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hiyo mifano michache, nirudi kwenye hoja. Tumekuwa tunapitisha fedha sana, lakini kuna matatizo makubwa katika matumizi ya fedha zetu ambazo tunazipitisha hapa. Wakati Waziri wa Fedha anatoa *speech* yake, alitaka kutuaminisha kwamba, katika Taarifa ya CAG ambayo ameitoa mwaka huu wa 2009, masuala yalikuwa yanaonekana yame-*improve*. Hali kadhalika Waziri wa TAMISEMI na yeye alivyowasilisha, alitaka kutuaminisha kwamba, masuala ambayo CAG alikuwa anayahoji yame-*improve*. Hii ni Ripoti ya CAG, toleo la mwisho, ambayo imetolewa tarehe 26 Machi, 2009. Ukurasa wa 13 anasema, hati safi zimepungua kutoka asilimia 73 mwaka 2006/2007 hadi asilimia 70 mwaka 2007/2008. Pamekuwepo na hati isiyoridhisha asilimia tano mwaka 2007/2008 ukilinganisha na asilimia moja kwa ile *auditing* aliyofanya mwaka uliopita. Sasa kutuambia kwamba, taarifa ziko shwari wakati ambapo CAG mwenyewe anasema sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, tukija Wizara ya TAMISEMI, ukurasa wa 30 wa Hotuba unaonesha kwamba, fedha kiasi cha shilingi milioni 232 iliyopangwa kwa ajili ya ukarabati, ufuatiliaji na usimamizi wa Vituo vya Afya Wilayani, zilitumika kwa shughuli tofauti na ilivyokusudiwa. Hii sio sahihi, tunapitisha miradi hapa mnakwenda mnaibadilisha huko, lengo linakuwa halijatimizwa. Malipo ya shilingi 137,271,218.50 yalifanywa bila kuwa na nyaraka ambativu. Hali kadhalika, magari yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 3.4 yaliyonunuliwa kupitia Wizara ya Miundombinu yalikuwa hayajapokelewa.

Mheshimiwa Spika, huu ni upungufu mkubwa kwa fedha hizi, hapa nazungumzia Wizara; ukija kwa fedha za jumla, Auditor anasema; "Hata hivyo, katika mwaka huu wa ukaguzi, Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa 41, zilikuwa hazikushughulikia masuala ya miaka ya nyuma, yenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni moja na bilioni thelathini na sita." CAG amekwenda ku-*query*, kuna matatizo ya matumizi ya fedha, Wizara na Idara za Serikali zinaambiwa leteni majibu kuhusiana na utata wa matumizi hawajibu! Kila siku mnakuja kutuomba pesa. Sasa vitu kama hivi vina umuhimu wa kuangaliwa, pesa hizi ni za wapiga kura wetu, Watanzania maskini, zinaletwa watu wanazichezea.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala zima la Kilimo Kwanza. Suala hili sio jipya, limekuwepo muda mrefu sana. Nimejaribu kupitia bajeti ya maendeleo, kwa sababu unapozungumzia kuendeleza kilimo, maana yake hii bajeti ya kawaida

haiangaliwi kwa kiasi kikubwa, unaangalia bajeti ya maendeleo kwa mantiki kwamba ni kwa kiasi gani miradi imepelekwa kwa wananchi. Nimeangalia Wizara saba ambazo zina kitengo au zina mahali ambapo panashughulika na masuala ya kilimo. Shilingi bilioni 133 katika fedha za maendeleo, kwanza kwa Wizara ya Kilimo peke yake, zimetengwa shilingi biloni 92; katika hizo, shilingi bilioni 90 ni fedha za nje. Tumetoka kumsikia Mheshimiwa anavyolalamika, anasema ametengewa shilingi bilioni 23, zilizokuja ni ama shilingi bilioni mbili au tatu. Haya ndio madhara ya utegemezi.

Mheshimiwa Spika, katika hizi shilingi bilioni 133 za ujumla wa Wizara ya Kilimo na jumla ya Wizara nyingine, shilingi bilioni 23 tu ndio fedha za ndani. Hili ni tatizo. Ukija ukiangalia Mikoa; Mikoa katika bajeti yao yote ya kilimo ni shilingi bilioni 65 zote ni za nje, namaanisha Mikoa ya Tanzania Bara yote, shilingi milioni 55 tu ndizo fedha zetu za ndani.

Mheshimiwa Spika, jana wakati Katibu Mkuu wangu na Kiongozi wetu Msaidizi wa Kambi ya Upinzani, alipokuwa anajenga hoja ya vipaumbele; ni kwa kiasi gani sisi kama wananchi au sisi kama viongozi, tunaangalia *priorities*, alijikuta akiwekewa vikwazo. Shilingi milioni 55 fedha za ndani Mikoani kwa ajili ya kuendeleza kilimo! Wakati huo huo kuna shilingi bilioni eti 30 zimetengwa kwa ajili ya takrima na vyakula. Sasa mama yangu ndio akaharibu kabisa, aliposema kwamba zinanunuliwa fenicha, friji na kadhalika. Kwa hiyo, ina maana ninyi kila mwaka mnanunuliwa friji, sijui fenicha na nini.

Kwa hiyo, vitu kama hivi ni *priorities*, haiwezekani kabisa ukatenga shilingi milioni 55 za ndani ukasema kwamba, hizi ndio fedha ambazo zitatengwa kwa ajili ya kilimo wakati CAG anasema asilimia 70 ya fedha za wafadhili ama haziji au zinachelewa kuja, lakini asilimia 99 ya fedha za ndani tuna uhakika wa kupatikana. Kwa hiyo, nadhani lazima tupange, tuchague na tukubali kwamba, masuala ya kuwa na mabilioni kwa ajili ya viburudhisho hata kama zimedundulizwa katika Departments mbalimbali, hayafai kwa sababu mwisho wa siku, watu ambao wanakuwa *classified* kupata hivyo viburudisho ni ninyi wakubwa, ambao hata mkinyimwa, *you can afford it*; mna *salary* ya kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ni suala ambalo nilikuwa nasisitiza kwamba, huu utegemezi ukiangalia kwenye miundombinu, kuna barabara nyingi sana hazitajengwa, hawa watu ambao tunawategemea, ambao huko nao wanahangaika na uchumi wao, wasipoleta fedha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nimalizie na suala moja dogo, linalomhusu Waziri wa TAMISEMI. Kule Kawe, sitamtaja Londa sasa hivi. Kule Kawe, Wananchi wamekuta maeneo yao ambayo walikuwa wanazikia, yamechukuliwa na yameuzwa kwa mtu pasipo wao kuwa *compensated*. Sasa namwomba Waziri wa TAMISEMI, pamoja na Naibu wake, nawaheshimu, wachapa kazi, jaribuni kuwafuatilia hawa watu ambao hili eneo tokea miaka ya 1960 walikuwa wanazika, baadae wakaambiwa wasizike kwa sababu panatakiwa kufanyiwa maendeleo mengine...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ujumbe umefika lakini.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima kwa uchambuzi wako. Namwita sasa Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani na atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, wakati huo huo ajiandae Mheshmiwa George Simbachawene.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza, niipongeze Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Vilevile niwapongeze Wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutuletea maelezo mazuri ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Pangani na kwa niaba yangu mimi mwenyewe, naishukuru Serikali kwa hatua iliyofikia juu ya Kivuko cha Pangani. Leo sitazungumzia Kivuko cha Pangani, kwa sababu nina uhakika Wananchi wa Pangani wana matumaini makubwa kwamba, Kivuko chao hivi sasa kinaundwa kipya na kiko pale pale Pangani. Wataalamu kutoka nje wanakifanyia kazi na wao wenyewe wakishuhudia maendeleo ya kuunda Kivuko kipya kinavyokwenda. Niishukuru Serikali kwa hatua hiyo na kwamba, itakuwa imetekeleza ahadi yake ya Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimshukuru Waziri wa Maji kwa taarifa aliyoitoa leo asubuhi kwa masuala ya maji na kwamba, Halmashauri nane ikiwemo ya Pangani, zipo katika mchakato wa kufungua mapendekezo ya kifedha na kuzifanyia tathmini. Matumaini yangu ni kwamba, hatua hii itakwisha mapema zaidi ili tuondokane na matatizo ya maji kwa Wananchi wa Pangani. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, ombi ambalo limetoka Halmashauri ya Wilaya ya Pangani juu ya chanzo cha maji cha Boza, ambapo wale waliokuwa wanaishi katika chanzo kile, wanatakiwa waondoke katika hifadhi ile ya maji. Kinachogomba sasa ni kulipa fidia ili waondoke; na kila tukichelewa, gharama ya fidia inapanda na itakuwa ni gharama kubwa kwa Serikali.

Baada ya kusema hayo, sasa nijikite moja kwa moja kwenye Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hitimisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema: "Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kazi za Serikali zilizopangwa kwa Mwaka 2009/2010 na kutoa huduma bora kwa wananchi, ni muhimu Watumishi wote wa Serikali, wawajibike ipasavyo katika kuwatumikia wananchi na kuondoa kero zinazowakabili." Akaendelea kusema: "Nahimiza watumishi wote, kuzingatia maadili ya kazi, kanuni na sheria, pamoja na kufanya kazi kwa bidii na ubunifu na kuepuka

vitendo vya rushwa. Watumishi wa umma wasio waaminifu na wababaishaji, wabanwe na kuchukuliwa hatua za kinidhamu."

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia katika Bunge hili, maneno makali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, ambayo yanakwenda kwa Baraza la Mawaziri. Mimi nianze kusema kwamba, sheria zote na kanuni zote, lazima zizingatie Katiba ambayo ndiyo Sheria Mama.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, nikirudi kwenye Katiba, Rais ndio Kiogozi wetu Mkuu katika Serikali hii. Ibara ya 34(4) ya Katiba yetu inatuambia: "Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muuungano yatatekelezwa ama na Rais mwenyewe moja kwa moja au kwa kukasimu madaraka kwa watu wengine wenye madaraka katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Mheshimiwa Spika, vilevile ibara hiyo hiyo ya 34(5)(b) kinasema: "Yanalizuia Bunge kukabidhi madaraka yoyote ya Kisheria mikononi mwa mtu au watu au Mamlaka yoyote ambayo si Rais."

Mwisho, ibara ya 36(4) inasema: "Masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) hayatahesabiwa kuwa yanamzuia Rais kuchukua hatua za kudhibiti nidhamu ya Watumishi na Utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Mheshimiwa Spika, Rais ana majukumu mengi na Katiba inasema anakasimu madaraka kwa watu waweze kumsaidia na kumshauri katika kutekeleza majukumu yake. Moja ya watu hao ni Mawaziri, Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu Kiongozi, lakini tunae Kiongozi wa Serikali, ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi napata tabu kwa sababu Katiba imesema wazi na Rais ana mamlaka ya kutoa maelekezo yake kwa maandishi. Kwa kutumia Kitabu au Waraka unaoitwa Waraka wa Rais wa mwisho ambao ulitolewa Desemba, 2000 na ambao ninao; Rais ametoa Waraka huu kwa kufafanua madaraka ambayo amewapa viongozi wengine kukasimu ili kumsaidia katika shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, pale Ikulu kuna Katibu Mkuu Kiongozi. Kazi ya katibu Mkuu Kiongozi kwa mujibu wa Waraka wa Rais unasema: "Kazi za Katibu Mkuu Kiongozi ni pamoja na kumshauri Rais katika masuala yanayohusu nidhamu na ajira katika Utumishi wa Umma."

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka 2002, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Utumishi. Sheria hii ya Utumishi kwa maoni yangu, naona kama vile hatukwenda sawa sawa na katiba. Niliuliza maswali hapa, lakini Serikali ikasema iko sawa sawa, sheria ile tuliyoipitisha hapa katika *The Public Service Act, 2002,* ibara ya 4 inasema: "Pamoja na majukumu ya *Chief Secretary; The Chief Secretary shall be the highest ranking disciplinary authority in the* service *and may, in that capacity in relation to any servant, exercise all or any of the powers delegated to a disciplinary authority*."

Mheshimiwa Sipka, Waraka wa Rais haukumpa madaraka hayo Katibu Mkuu Kiongozi. Kwa mujibu wa Katiba, ambayo imesema kwamba, Rais mwenyewe ata-*delegate* kwa kumsaidia, lakini Waraka wake unasema amshauri Rais. Tulipitisha hii sheria sasa Rais ameleta Mawaziri hapa wa kumsaidia kazi, leo ukienda mtaani muulize mtu yeyote; bosi wa Wizara ni nani? Utaambiwa Waziri kwa sababu ndio Kiongozi Mkuu pale Wizarani, sasa katika sheria hii Waziri hatajwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri ndio mtu wa moja kwa moja anayemsaidia Rais. Sasa sijui Waheshimiwa Mawaziri, wanachukua hatua gani au wana meno gani katika Wizara zao?

Ibara ya 6 ya Sheria hii inasema, imempa sasa madaraka Katibu Mkuu wa Wizara. Sheria inasema: "*Every Permanent Secretary, Head of Ministerial Department, Regional Administrative Secretary and Director of Local Government Authority shall…*" Kuna kifungu (b) kinasema: "*Be the Authority in respect of Appointment Confirmation and Discipline of Public Servants other than those appointed by the President.*"

Mheshimiwa Spika, sasa niwaulize Waheshimiwa Mawaziri; toka tumepitisha sheria hii; ni wangapi ambao amewaajiri; ni wangapi ambao ametoa *disciplinary action* ili ionekane kwamba yeye ndio Kiongozi wa Wizara na sheria hii bado haikumtaja Waziri?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Waraka wa Rais, kifungu kidogo cha (3) kinasema, Kiongozi wa Wizara, wajibu wake ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera, kuongoza Watumishi wa Wizara yake na kuwa Kiongozi Msimamizi katika utekelezaji wa mipango na kazi ya watumishi. Leo wanaajiriwa watu ndani ya Wizara, Waziri huna habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo watumishi wanafanya mambo ya ubadhirifu ndani ya Wizara, Waziri kwa mujibu wa sheria huna mamlaka ya kum-*discipline*. Madaraka hayo tumempa Katibu Mkuu, lakini sisi Wabunge tunapokuja hapa Bungeni na kuihoji Serikali, tunamhoji Waziri, hatumhoji Katibu Mkuu. Tutawashambulia Mawaziri, tutasema maneno mengi juu ya Waziri, lakini Waziri kwa mujibu wa sheria, hakupewa mamlaka hayo. Waswahili wanasema; mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Waheshimiwa Wabunge, sisi sote hapa ni *Potential Ministers*, *Potential Depute Ministers* na *Potential Prime Ministers. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba, hivi leo sisi tukienda kwenye nafasi zao, kwa mamlaka ya Rais aliyopewa, anaweza akafanya hivyo; je, tutakubali kushambuliwa kama sisi tunavyowashambulia wao? Hatuna meno. Tutaendeshaje Serikali namna hii? Mheshimiwa Waziri, anapita kwenye korido anamkuta mfanyakazi anamuuliza wewe ni nani? Ooh! Mheshimiwa Waziri, mimi nimeteuliwa katika Wizara yako na nimeajiriwa toka mwaka fulani; hamjui!

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri, Makatibu Wakuu kwa kumheshimu Waziri na kujua umuhimu wa Waziri pale, anakwenda na kumpa taarifa, lakini hawezi kushauriana na kutoa maamuzi, kwa sababu hana maamuzi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo tuliopitisha hii sheria lakini tumetereza. Ninachotaka kusema ni kwamba, hii sheria tuiboreshe, naweza nika-*apply* suala hili hili kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu; hivi watu wote walioajiriwa katika ofisi yako unawajua? Mimi naogopa sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rished, ulitakiwa uisome na nina kushangaa, kwa sababu umesoma sheria. Umesoma pia Katiba kama vile ambavyo *Chief Secretary* hayuko juu ya Rais, kwa mtiririko wa ibara ya 35(1) ya katiba inasema; nanukuu: "Shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na Watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais." Ibara ya 36 uliyoinukuu, Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha au kufuta nafasi za Madaraka ya namna mbalimbali katika Utumishi wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, Mawaziri na Wakuu wa Mikoa, ndio mkono wa Rais. *(Makofi)*

Waheshiwa Wabunge, asikae Waziri hapa akasema kuna sheria imepitishwa na Bunge; mimi siwezi lolote na nini, huyo hafai kwa sababu yeye ni mkono wa Rais, anawezaje kubabaishwa na Katibu Mkuu ama na RAC. Isomeni katiba vizuri, sheria hiyo haikukosewa, tuliitafakari vizuri, Waziri anaweza kumu-*over rule* Katibu Mkuu wakati wowote; atadai taarifa zozote na lazima apewe kwa mujibu wa ibara ya 36. Unapomwona Waziri yeyote yule, amekasimiwa madaraka ya Rais katika sekta inayomhusu. Kwa hiyo, anachotakiwa kukifanya, yeye mwenyewe akae pale akijua kwamba, kwenye sekta hiyo yeye ndio Rais na anawajibika kwa Rais peke yake. Naomba niondoe huu utata, kwa sababu tusipokwenda hivi, tutatoa idhini kwamba, kila Waziri akija hapa aseme bahati mbaya mimi Katibu Mkuu kanishinda, kwa hiyo, samahani sina la kufanya ambalo siyo sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi ajiandae.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kushirikiana na wenzangu katika kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na ile ya Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi na Wananchi wote wa Mbozi, napenda kutoa pongezi sana kwa hotuba hizo mbili ambazo zilisomwa kwa pamoja. Pia naomba nisiwe mtovu wa shukrani, kwa kutoenzi yale yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne, hususan katika Jimbo la Mbozi Magharibi, ambalo kama nilivyosema kwenye hotuba zangu ama maelezo yangu ya hapo awali ni kati ya yale Majimbo ambayo yapo pembezoni.

Tulipoingia madarakani mwaka 2005, Jimbo hili naweza kusema lilikuwa halina miundombinu ya barabara na maji, lakini kwa sasa naweza kudiriki kusema kwamba, kwa nguvu ya Serikali ya Awamu ya Nne, hivi sasa tumeahidiwa barabara ya lami kutoka Tunduma hadi Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, zile kilomita 224, kati yake kilomita 114 ziko ndani ya Jimbo langu. Kwa hiyo, hiyo itakuwa ni faraja katika kuhakikisha tunapunguza matatizo ya usafiri wa Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi. Vile vile mtakumbuka, mwaka jana Serikali hii iliweza kutoa pesa za kujenga Barabara ya Mlowo hadi Kamsamba, ambayo itaungana na ile aliyoiongelea Mheshimiwa Dr. Mzindakaya ya Chilyamatundu - Sitalike – Mpanda. Hii ni njia fupi kuliko ya kupitia Sumbawanga - Tunduma -Mbeya - Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa barabara hiyo, naiomba Serikali imalizie kipande cha kilometa ishirini na tano kati ya Itumbula na Kamsamba, pamoja na Daraja la Mto Momba, ambalo likikamilika, litaunganisha hiyo barabara moja kwa moja kati ya Mbozi na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara zile ambazo kwa pamoja mimi na Mbunge mwenzangu wa Mbozi Mashariki tuliongelea; kutoka Igamba – Msangano – Chitete – Utamabalila – Kamsamba, nayo kwa heshima na taadhima, napenda kusema Serikali imeshughulikia na sasa hivi inatengenezwa vizuri. Hali kadhalika, kuna Barabara ya Chapwa – Namole – Chindi – Msangano, iko mbioni inatengenezwa na naamini kabla ya mwisho wa mwaka 2010, barabara hizi zitakuwa tayari.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara muhimu kabisa ya kutoka Kakozi – Chipumpu – Kapele – Kasinde – Ilonga kuunganisha na ile ya kutoka Matai hadi Kasanga Ziwa Tanganyika, ambayo itarahisisha uwezo wa Wananchi wa kutoka Mkoa wa Mbeya kufika Ziwa Tanganyika na kurejea Mbeya ndani ya saa tano. Naishukuru Serikali kwa hilo.

Sina budi pia kuishukuru serikali kama nilivyokwisha kusema, Jimbo hili lilikuwa na matatizo makubwa ya maji. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, imejitahidi kusambaza maji ya visima na hivi sasa naweza kudiriki kusema, wale wananchi waliokuwa wamekata tamaa hususan wa Tarafa ya Kamsamba na Kata ya Myunga, ambao wakati tulikuwa tunawahimiza wajenge shule, walisema hizo shule nani atasoma wakati sisi hatulali nyumbani; ikifika jioni wake zetu wanaanza kwenda kutafuta maji, wanaporudi na sisi tunakwenda kufanya kazi; hivyo hakuna watoto wanaozaliwa. Sasa wamepata maji na wanafurahi. Kasoro kuna tatizo moja ambalo naweza kusema ni la kiufundi la kwamba, baadhi ya visima havijaweza kutoa maji, lakini mafundi wanafanya marekebisho. Serikali iko mbioni kuanza kufunga pampu za maji kwenye Vijiji vya Ndalambo na Chiwanda, kwa sababu tayari maji yamekwishapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara, naomba nirudie Barabara ya kutoka Kakozi, ambayo itafika Ziwa Tanganyika. Pamoja na kutolewa hizo pesa, kuna tatizo ambalo tunaomba usimamizi wa Wizara ya Miundombinu, pamoja na *TANROADS* na

hata Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi yenyewe inaripoti kwamba, ile barabara inajengwa kama tuta la viazi, kwa hiyo, inaombwa ipanuliwe na ijengwe kwa viwango.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba niongee juu ya Elimu. Napenda nishukuru kwamba, miaka mitatu iliyopita, katika Jimbo la Mbozi Magharibi, kulikuwa kuna shule nne tu za sekondari, lakini hivi sasa tunazo shule kumi na tano. Kulikuwa na watoto ambao wanakwenda shule za msingi arobaini na sita elfu na walimu mia sita sitini tu, lakini hivi sasa kwa msaada wa Wizara ya Elimu, mwaka juzi tuliweza kupewa nafasi za walimu wanafunzi arobaini na mwaka jana walimu wanafunzi mia moja; ninaamini mwaka huu watatupa wengine zaidi ili wakimaliza warudi kufundisha katika zile shule.

Mheshimiwa Spika, tatizo la nishati hususan ya umeme. Jimbo la Mbozi Magharibi, lenye vijiji zaidi ya themanini, lina vijiji viwili tu vyenye umeme ambavyo vipo kwenye Gridi ya Taifa, kwa maana ya Tunduma na Mpemba. Vijiji vingine vyote viko gizani; hivyo naiomba Wizara ya Nishati na Madini, kupitia Shirika la Kusambaza Umeme Vijijini, ifikirie hizi Kata kumi na moja ambazo hazina umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano ya simu, napenda kuishukuru Serikali kwa sababu hapo nyuma kulikuwa hakuna chochote, lakini hivi sasa, Kata tano kati ya zile kumi na moja tumepata minara ya simu na mtu anaweza akasilikiza ama akawasiliana na watu wengine kwa urahisi na tunaamini sehemu iliyobaki itakamilika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, kwa sababu mwanzoni mwa mwaka huu, kati ya watoto waliokuwa wamefaulu ni 40% tu waliokuwa wamepata nafasi ya kuchaguliwa kuingia shule za sekondari, lakini ilipokuja uchaguzi wa awamu ya pili, kwa nguvu za Wananchi na Halmashauri hiyo, 96% ya watoto wameweza kuchaguliwa; hivyo ni 4% tu ndio ambao wameshindwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, naomba nitoe shukrani na pongezi nyingi kwa Mkoa wa Mbeya, kwa maana ya Mkuu wa Mkoa, kwa juhudi zake alizozifanya katika kuhamasisha Mkoa. Katika awamu ya kwanza, watoto waliokuwa wamechaguliwa walikuwa ni 41% tu, lakini mwisho wakati wa awamu ya pili, tumeweza kufikia 97%. Namshukuru sana kwa sababu ni 3% tu ndio walioweza kukosa nafasi ya shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, naomba niisifu Serikali kwa ujumla, kwa suala la elimu, kwa sababu mwaka jana tulikuwa na watoto waliofanya mtihani; 50% ndio walioweza kupata nafasi ya sekondari katika awamu ya kwanza. Awamu ya pili ni 98%. Hiyo inaonesha ni jinsi gani Wananchi walivyohamasishwa na kuweza kujenga shule kwa kipindi cha miezi na kuzifungua ili kuhakikisha watoto wetu wanapata nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee juu ya shukrani zangu kwa Serikali, kwa kuweza kujenga Ofisi ya Jimbo la Mbozi Magharibi, ambayo hivi sasa ipo kwenye hatua za mwisho. Naamini hivi sasa ninavyozungumza, wakati wowote tunaweza kuhamia; hiyo yote ni kwa busara za Serikali yetu ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kutosema kwamba, nimegundua kwamba, kuna Halmashauri ambazo katika kujitafutia vyanzo vyake vya fedha, zimeweza kufanya vizuri. Pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kusema kwamba, kuna maeneo ambayo ukusanyaji haujawa mzuri. Nimeangalia kwa mfano, Mkoa wa Mbeya wenyewe, Halmashauri katika makisio ambayo yalikuwa yamekisiwa zimeweza kupitiliza kile kiwango.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, nitoe pongezi; nilipokuwa naangalia kwenye jedwali hili kwa Halmashauri mbili kwa nchi nzima; ya kwanza ni ile ya Wilaya ya Kyela, ambayo hadi mwezi wa tatu, imeweza kupita makisio yake kwa 700% na Halmashauri ya pili ni Bariadi ambayo hadi mwezi wa tatu, ilipitia makisio yake kwa makusanyo ya asilimia 500%. Naamini kama hawa wameweza na Halmashauri nyingine zinaweza zikafikisha malengo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee mambo niliyoyaona kwenye jedwali. Kwanza ni ule mfuko wa barabara. Nimeona pesa zimekuwa zikipelekwa kwenye Halmashauri kwa awamu. Kwa bahati mbaya, katika nchi hii maeneo mengi ambayo hizi barabara zinatakiwa kujengwa kwa kutumia hizi ni zile ambazo msimu wa mvua unaanza mwezi Novemba hadi Aprili. Sasa hapo ndio wakati ambao kwa bahati mbaya, fedha nyingi zinatolewa. Ningetoa ushauri tu kuwa, tunaomba fedha hizi zitolewe *quarter* ya kwanza na ya nne ili hawa watu waweze kukamilisha hizi barabara, kwa sababu barabara zetu nyingi unapolima mwezi wa pili ama wa kwanza, zinaoshwa na mvua; kwa hiyo, inakuwa hela ile imekwenda na maji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niongelee juu ya pesa zinazopelekwa mashuleni kwa ajili ya uendeshaji wa hizo shule. Nimeona kitu kimoja ambacho kimenishangaza; shule nyingi tunasema hazina vifaa ama yale mahitaji hayatimizwi, lakini nilipoangalia yale majedwali, kuna pesa ambazo zinasalia kila mwaka na hadi inafika mwisho wa mwaka, kuna pesa nyingi tu hizo shule bado zinazo. Nafikiri ipo haja ya kusimamia na kuangalia namna ya kuzitumia hizi pesa, kwani naona ni mamia ya mamilioni ambazo zinabaki katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hii kwa namna nyingine ni kwamba, Halmashauri zetu hazina *absorption capacity*, kiasi cha kwamba, watumiaji hawajui namna ya kulenga hizi pesa zitumike kwa maeneo yapi na kwa vipi.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee tena kuhusu miradi ambayo ingeweza kutusukuma kwetu sisi kule Mbozi. Kwanza, nitoe shukrani kwa Serikali hususan Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa miradi miwili mikubwa; Mradi wa Naming’ongo ambao kwa mwaka wa fedha huu unaoisha, Serikali iliweza kutoa shilingi milioni mia saba hamsini, baada ya mradi huu kuwa umesombwa na maji. Desemba, 2006, baada ya kuwa umegharimu shilingi milioni mia tisa, kutokana na makosa ya ujenzi na uharibifu wa shughuli za kibinadamu, kutokana na magogo ambayo yalikuwa yamejaa kwenye huo mradi. Nashukuru Serikali imeweza kutoa pesa na mradi huu hivi sasa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani kupitia Wafadhili wa DIDF, Mradi mwingine wa Iyendwe, ambao ni mkubwa kabisa; umeweza kupatiwa shilingi milioni mia nne. Kwa hiyo, tutakuwa na mradi wa pili wa umwagiliaji, ambao Mwenyezi Mungu akipenda, mwaka wa fedha ujao tutaanza kuutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa ni miundombinu ya barabara kutoifikia hiyo miradi iliko, naiomba Serikali iharakishe hizo barabara ambazo zimepangiwa kujengwa. Miradi yote hii ya umwagiliaji itazalisha ikiwa itapata soko. Mpunga wa kule hauhitaji mbolea na unakua kweli kweli; ninapenda niwaeleze kwamba, kiwango kikubwa cha mchele unaotoka Mkoa wa Mbeya kwa hivi sasa mchele wa kunukia sana unatoka Mbozi Magharibi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ya pili hiyo sasa.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Siyame. Namwita sasa Mheshimiwa George Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, wakati huo Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya ajiandae.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kibakwe, niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumzia nilichokuwa nimekiandaa, najikuta ninasukumwa na utashi na dhamiri yangu ili nizungumzie jambo ambalo limekuwa likisemwa semwa humu. Kwa kweli sijui kama nitawafurahisha au kuwaudhi wangapi, lakini sio kwa ajili ya hilo, nipo kwa ajili ya kufanya kile ambacho naamini busara yangu inaona ni jambo sahihi.

Mheshimiwa Spika, imejitokeza tabia ya kuzungumzia tena si kwa nidhamu, Viongozi wa Kitaifa waliopita. Lazima Watanzania wafahamu kwamba, kama wanaona machafuko mengi yanayotokea duniani na hasa katika nchi za Afrika ni kuchimba makaburi ya viongozi waliopita; kiongozi anapokuwa madarakani atafanya mema mengi, lakini na mabaya pia yatakuwepo na huo ndio ubinadamu tunaoambiwa katika vitabu vitakatifu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama kumzungumzia kwake kutakuwa kunatumika kuzungumza kwa utaratibu huu wa sasa, kama ambavyo watu wanamzungumzia Mheshimiwa Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu na kusahau yote mazuri aliyoyafanya kana kwamba alikuwa mtu wa ajabu, mimi sikubaliani na siungi mkono wazo hilo na hiyo si tabia na utamaduni wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiruhusu Mkapa akazungumzwa hivi, kesho tutarudi nyuma kwa Mwinyi, baadae kwa Mwalimu na baadae hata kwa Mheshimiwa Kikwete, atakapomaliza muda wake tutamzungumzia hivi. Je, Tanzania itabakia salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia kanuni zetu, hasa Kanuni za Bunge, kwenye ile ibara inayozungumzia mambo yasiyoruhusiwa kuzungumzwa Bungeni, tuone namna gani tunaweza kuwalinda viongozi wa namna hii; tuwe na utaratibu mzuri zaidi wa kuwazungumzia lakini si kama tunavyofanya hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, tangazo: Kibakwe mambo ni shwari. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imetekelezwa kwa kiwango kikubwa. Tunakwenda kwa takwimu, tulipoanza kwa maana ya mimi na Wananchi wangu wa Jimbo la Kibakwe katika elimu ya sekondari tulikuta kuna sekondari tano, sasa hivi tuna sekondari kumi na mbili katika Kata tisa; hilo ni goli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne tumefungua zahanati tano mpya na mwakani tunatarajia kufungua nyingine nne katika Jimbo la Kibakwe; goli la pili.

Mheshimiwa Spika, visima vifupi 34 vimechimbwa katika Jimbo la Kibakwe na watu wanapata maji safi na salama. Mwaka 2005, asilimia ya upitikaji wa barabara ilikuwa ni chini ya asilimia 30, lakini sasa hivi tuko asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wananchi kule wanakaa mkao wa kusubiri umeme; sasa nasema wanaokuja waje, mambo kule ni shwari, ilani imetekelezeka na mambo ni safi. Haukosekani upungufu wa hapa na pale; bado katika hiyo asilimia kumi, uwezekano upo. Kibakwe iko tofauti na eneo lolote katika Mkoa wa Dodoma japo ipo Mkoa wa Dodoma; kuna milima mikubwa na mirefu kama iliyoko Lushoto; kwa hiyo, kufanikiwa au kutengeneza barabara ya kilomita hata tatu tu, unahitaji kuanzia shilingi milioni mia mbili au mia tatu; Halmashauri peke yake kwa Bajeti ya *Road Fund* haiwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Waziri Mkuu, akiwa Waziri wa TAMISEMI, alinisaidia nikapata angalau barabara mbili ambazo zilikuwa hazijawahi kutengenezwa toka nchi ipate uhuru, lakini sasa zinapitika na mambo ni safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali hii, tunaweza tukaenda hata kwenye takwimu nyingine; Mheshimiwa Zitto, alinivutia sana asubuhi alipokuwa akisoma takwimu na kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi haijatekelezwa. Nimwambie tu kwamba, takwimu anazosoma au anazozitumia afanye *comparison* na ndiyo maana ya takwimu, huwezi ukasoma takwimu ya Tanzania peke yake halafu ukashindwa kui-*compare* na nchi nyingine kwa uwiano. Inaonekana kwamba, takwimu zinazosomwa hapa basi Chama cha Mapinduzi kitatekeleza kile kilichopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, malengo ya milenia kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano ni asilimia 54 kwa 1000, sisi tumefikia watoto 91 kutoka huko nyuma ilipokuwa zaidi ya 120. Kwa hiyo, tunaendelea; huu ni mchakato na tufahamu kwamba,

mambo haya hayafanyiki kwa Tanzania kama kisiwa ni lazima tufanye *comparison*; wenzetu nchi za Kusini mwa Afrika wana kiwango gani, wenzetu wa Magharibi wana asilimia ngapi, ukifanya mahesabu *rate* ni hizo hizo, tunacheza humo humo. Kwa hiyo, wananchi wasielewe hapa kwamba, CCM imeshindwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kama ni lengo la milenia siyo 0 kwa 1000, kwa wajawazito nao takwimu iko hivyo hivyo, sasa hivi tupo zaidi ya mia tatu kwa laki moja, lakini malengo ya milenia nayo yanaeleza viwango vyake. Lazima tufanye *comparison*, huwezi ukaihukumu Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu tu unaijaji ikiwa peke yake, linganisha halafu uiseme, wananchi wajue Tanzania ipo kwenye nafasi ipi.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu amesema Kilimo Kwanza kina vitu kama vinne; amezungumzia habari ya utashi, kuwekeza katika kilimo, benki ya kilimo na mikakati.

Mheshimiwa Spika, mimi nizungumzie utashi, siku moja nimewahi kutembea umbali mrefu tu tukifanya ziara katika mikoa fulani, sitaki kuitaja maana wataniambia Mkoa huo ni wavivu, nilitembelea takriban Kata nne, niliwaona waliokuwa shambani ilikuwa wakati wa msimu wa mvua. Waliokuwa wanalima walikuwa ni watoto chini ya umri wa miaka kumi na wanawake, tena wanawake wenyewe siyo wasichana ni wazee na mababu kabisa. Huwezi kumkuta kijana mwenye nguvu yake, yupo shambani anafanya kazi. Kwa hiyo, kwanza ni utashi wa sisi watanzania wote kuamua kwamba kilimo ndiyo mkombozi wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, utashi usipokuwepo, hata tukisema habari ya *power tiller*, tukasema mikopo, mtu atachukua mkopo kwa ajili ya kilimo anakwenda kufungua duka. Kwa hiyo, iko haja hapa na sheria nyingine kama za nguvu kazi na nyingine zitaangaliwa, nguvu kazi nyingi imehamia mjini, vijijini hakuna anayefanya kazi na wengi vijijini wanafikiria kuajiri wenzao tu ndiyo wafanye kazi. Utasikia vibarua siku hizi hawapatikani, lakini unamkuta mtu kachomekea, kaulamba vizuri, haendi shamba! Hatuwezi kuleta Mapinduzi ya Kilimo kwa mfumo huu, mapinduzi ya jambo lolote ni vita. Kwa hiyo, kilimo kitafanikiwa tu endapo watu wote; viongozi, wananchi na wanasiasa tutaamua kipaumbele chetu ni kilimo na sisi sote tutakwenda shambani.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia kilimo katika Mkoa wa Dodoma, kama kuna watu wanafanya kazi sana na kuwa na mashamba makubwa ni Dodoma. Tatizo letu, maana ardhi tunayo na nguvu tunayo, kinachokosekana ni maji. Maji ndio tatizo letu, lakini watu wa Dodoma ni wachapakazi sana katika kilimo na tunalima maeneo makubwa sana, lakini tunachokipata ni kidogo mno. Tunadhani pengine wazo la umwagiliaji linaweza likawa msaada mkubwa kwetu, kwa sababu litatusaidia. Vile vile ni vizuri tukajielekeza zaidi kwenye uchimbaji wa mabwawa mengi Dodoma kadiri iwezekanavyo, maana hatuna mabonde. Tukiwa na mabwawa mengi, tutaendesha kilimo cha umwagiliaji na hata kilimo cha mbogamboga ili kuufanya uchumi wetu uweze kukua.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Waziri Mkuu, kwa kuhimiza sana na hasa kilimo cha *power tillers* na amekuwa akisema kila Mkoa, kila Wilaya na kila Kijiji anachopita. Mimi nampongeza sana, lakini namtaarifu tu kwamba, kadiri tunavyozungumzia *power tiller* kwamba ni ukombozi kwa Mtanzania na wenzetu wachache wanaofanya biashara, wanajua huko ndiko wakawagonge Watanzania; *power tiller* iliyonunuliwa kwa shilingi milioni mbili na laki tano mwaka 2004, sasa inauzwa shilingi milioni sita hadi tisa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa, hapa wameingilia wafanyabiashara na hivyo mashine hizo zitakosa maana, kwa sababu zitakuwa zina gharama kubwa. Hakuna ushuru kwa mashine za kutumika mashambani, lakini kwa nini bei inakuwa kubwa hivyo? Tutafute kampuni ya kichina tuilete hapa itengeneze tuwaambie wakulima wakanunue pale. Mapinduzi yanatakiwa na fujo kidogo, hayaji hivi hivi. Tukiwaambia wanunue kwa akina nani pale Kariakoo, tutawagonga kweli kweli, hakuna mkulima atakayenunua *power tiller,* tutawakopesha lakini watashindwa kulipa kwa sababu wamechukua mashine hizo kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, tutafute kampuni ije hapa, iwe na *centres* kwenye *zones,* watengeneze matrekta na watu wanunue moja kwa moja kwa bei nafuu. Tukifanya hivyo, tunaweza kufanikiwa na kufanya kitu ambacho ni kizuri katika suala zima la kilimo na kuleta haya mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais anasema atatoa bilioni moja moja katika Mfuko wa Uwekezaji katika kila mkoa, wengi tuliamini fedha hizi nia yake ni kwenda kwa wananchi wa kawaida, wale ambao hawana jembe la plau, hawana maksai wa kukokota, watanunue ili waweze kuendeleza kilimo.

Tuliamini kabisa fedha hizo zinakwenda kwa maskini, lakini siku zote ukichanganya mawazo ya kijamaa na kibepari utaishia pabaya, maana mabepari wana njia nyingi; wakasema *International Financial Regulation* sijui imefanya nini, wakatuyumbisha tukaletewa semina hapa Bungeni na mabenki; sasa hivi wako wapi?

Mimi Jimboni kwangu, hizo pesa za Mfuko wa Uwekezaji, hakuna hata mmoja aliyepata na nilitegemea watanunulia majembe na maksai wawili. Wangejikomboa nao kutoka kwenye umaskini ule wa chakula na kipato, lakini mambo hayakuwa hivyo. Tufikirie hicho kiasi kilichobaki cha kumalizia kwamba, angalau basi kiende moja kwa moja kwa watu maskini. Benki wametulaghai, wametuingiza mkenge hawajatupa hiyo mikopo na hawajakopesha mkulima yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu maskini hakupata kile ambacho aliahidiwa na Rais wake, hili liwe ni fundisho kwetu; ninaamini Chama changu kitashinda uchaguzi ujao na Serikali itaundwa, tutafanya marekebisho lakini tuanzie hapa tumalizie mwaka vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Kigoma, wakati huo huo Mbunge wa Ilala, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu ajiandae.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nachukua fursa hii, kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara hii na hasa kwa ufuatiliaji wa haraka wa kazi ambazo mara kwa mara tumekuwa tukiwapa na kupata matokeo yake haraka. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba nizungumzie suala la misamaha ya kodi. Serikali yetu kwa muda mrefu, imekuwa ikifanya utaratibu mbalimbali wa kutoa misamaha katika bidhaa mbalimbali, lakini kwa bahati mbaya sana, sijasikia Serikali yetu ikijikita zaidi katika Sekta ya Uvuvi, kutoa misamaha ya kodi ya zana za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wavuvi wote wa Tanzania, kuwasilisha hoja hii mbele ya Serikali, kuiangalia Sekta ya Uvuvi kwa misamaha ya kodi; kwa mfano, mashine ya kuweza kuendeshea boti, nyavu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuleta mabasi makubwa Dar es Salaam, lakini hakuna hamasa yoyote iliyotolewa kwa wafanyabiashara, waweze kufanya kazi hii kwa haraka na kwa kasi zaidi ili angalau kupunguza ule msongamano wa magari. Naomba Serikali ihamasishe wawekezaji kuleta mabasi haya kwa haraka na tunachohitaji ni kusamehe kodi kwa muda maalumu kwa mwaka au miaka miwili ili kazi hii nayo iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi wa *DART*, hapo awali ulikuwa chini ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Tumejituma, tumejishughulisha hatimaye dakika za mwisho, ukachukuliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika Mradi huu kuna upungufu umejitokeza; sisi kama Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, tuna mali zetu tunamiliki kihalali, lakini Mradi wa *DART* unataka kuchukua mali hizo bila ridhaa ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Tunaomba sana, Mamlaka ya *DART* na Mamlaka ya Jiji la Dar es Salaam, wakae pamoja wakubaliane juu ya mali ambazo wanataka kuzitumia kwa Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye Mji mpya wa Kigamboni, dhana ya Mji Mpya wa Kigamboni ni nzuri, lakini utekelezaji wake; Wananchi wamezuiliwa kuuendeleza Mji wa Kigamboni karibu Kata nne; Kibada, Mji Mwema, Vijibweni na Kigamboni yenyewe. Kabla ya hapo, Wananchi hawa walichukua mikopo benki, sasa hawajazitumia kwa maendeleo waliyoyakusudia; riba zinaendelea, bahati nzuri Waziri alipita kwenye Kata hizi kuhamasisha. Nimetumwa na Wananchi wa Kigamboni, kuyaomba mabenki yanayohusika, kusimamisha riba za mikopo yao kwa sababu kosa hili siyo lao, mikopo ime-*freez.*

Mheshimiwa Spika, katika ziara yetu ya kutembelea na kuhamasisha Mradi huu wa Mji Mpya Kigamboni na Mheshimiwa Waziri, ilitamkwa bayana kwamba, kitaanzishwa chombo cha kusimamia uanzishwaji wa Mji huu wa Kigamboni. Wizara imeshaanza kuingia mitaani Kigamboni, bila chombo hiki kujua kinaanzishwa lini; je, haki na maslahi ya Wananchi wa Kigamboni yatasimamiwa vipi na malalamiko yatapelekwa wapi? Mamlaka hii iko wapi na itaanzishwa lini? Tunaomba tupate ufafanuzi huo ili wananchi tupate ahueni katika mchakato huo.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Kigamboni, sehemu kubwa ina bahari, naiomba Serikali katika mipango yake yote, ihahakikishe inatenga maeneo kwa ajili ya uvuvi. Msitwae maeneo yote, kuwaweka matajiri kujenga hoteli za kisasa, wengine tangu tumezaliwa kazi yetu ni uvuvi. Kwa hiyo, mtakapopanga Mji huu wa Kigamboni, hakikisheni kwamba, mnatupatia maeneo kwa ajili maenedelezo ya kazi za uvuvi tulizozizoea tangu tulipozaliwa. Naiomba sana Serikali ilizingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Mradi wa Kujenga *Refinery* Kata ya Sombangira ama Migomvu, ambayo Wizara ya Ardhi walikwenda kule wakazungumza na wananchi. Naomba tujue, Mradi huu umefikia wapi. Kwa taarifa nilizonazo ambazo siyo rasmi ni kwamba, Mradi huo haupo. Wananchi wamezuiwa wasiendeleze maeneo yao, wamerudi nyuma kwa muda wa miaka hiyo miwili, mitatu. Je, Serikali inasema nini juu ya kuwarudisha nyuma wananchi wetu?

Serikali ichukue jukumu la kuwafidia wananchi hawa, ambao mmewasimamisha kutoendelea kwa kipindi hicho cha miaka miwili, mitatu iliyopita. Nakuomba sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, lisimamie hili na wananchi wanakutegemea; najua hatua inayostahili itachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi wa Maji wa Kisarawe II, DAWASA wamechukua eneo kule ekari nyingi tu, kuna malalamiko makubwa sana. Naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Naibu Waziri wa Maji; alikuja akazungumza na wananchi na hatimaye angalau pumzi za wananchi zimetulia kidogo. Kuna mambo makubwa yafuatayo, ambayo wananchi wangependa kujua, naomba TAMISEMI kupitia kwako Waziri Mkuu tupate majawabu haya:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, eneo kubwa mno limechukuliwa; inashangaza ukilinganisha na miradi mingine ya maji iliyopo Tanzania hii. Pili, watu watakaochukuliwa maeneo yao ya mashamba na nyumba, hawajui watakwenda wapi, kwani hawajapewa eneo mbadala la kwenda kufanya ujenzi na kilimo. Mnatuweka njia panda, naomba sana tupate jawabu hili na tupate maelekezo ya Serikali kuhusu eneo mbadala, ambalo Wananchi wa Kisarawe II watapelekwa. Hawana ugomvi na Mradi, lakini wanataka wajue eneo mbadala watakalokwenda na vilevile juu ya fidia kwa mujibu wa soko huria.

Mheshimiwa Spika, siku ya ziara ya Naibu Waziri, alikuwepo Afisa Ardhi na akaahidi kwamba, atajitahidi kutafuta eneo mbadala na wananchi watapatiwa kwa bei nafuu ili ile fidia watakayopewa, iwawezeshe kujiendeleza na kujitegemea zaidi. Kwa

hiyo, naomba ahadi iliyotolewa na Afisa Ardhi wa Manispaa ya Temeke kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, kwamba watapimiwa maeneo mengine itekelezwe, lakini kwa bei nafuu; zisije zikaja bei za ajabu baadaye.

Mheshimiwa Spika, tuna Shule za Sekondari za Kata, tuna malalamiko makubwa kweli, kila unapofanya mkutano wa hadhara vilio ni vingi; juu ya nyumba za walimu, juu ya maabara na kadhalika. Ninaiomba Serikali, iangalie uwezekano kama inavyotumia Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii kwenye Miradi mingine ya Polisi, Uhamiaji na kadhalika, iangalie uwezekano wa kukaa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kuona kama inawezekana kujenga nyumba za walimu na maabara katika Shule za Sekondari za Kata. Nina hakika, tukikaa nao vizuri, Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii, itasaidia tatizo hili na tutapunguza kero za wananchi na vilevile kuwawezesha walimu kubaki mashuleni. Mwalimu anaripoti leo, kesho anakimbia kwa sababu hakuna makazi, naomba hilo nalo lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi ya majengo, tuna wazee ambao wameitumikia nchi hii, wametafuta uhuru wa nchi hii kwa kuchangia kwenye vikapu na kadhalika, wanapita kwenye Ofisi za Wabunge kwa unyonge, wakiomba kulipiwa kodi ya majengo. Wazee wetu hawa tumewasamehe kwenye afya na kwingineko, tuangalie uwezekano vile vile wa kutafuta njia ya kuwapa ahueni wazee katika kodi ya majengo wasiwe wanahaha.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Viwanja 20,000 Dar es Salaam ni mzuri, Mji unapangwa unakaa kisasa, lakini tuna matatizo kwamba, tumepima viwanja tu je, tutalima wapi ndugu zangu na tutafuga wapi? Lazima tuache maeneo kwa ajili ya kulima na mengine kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda nchi za wenzetu, mjini kabisa unakuta eneo kubwa limeachwa kwa ajili ya mifugo mtu anafuga, tuige mifano kama hiyo. Wenzetu Mawaziri, mnasafiri kila siku mnaona nchi za wenzetu, tuache maeneo ya mifugo na na kilimo.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la wanafunzi Dar es Salaam, tumepata tetesi kwamba, serikali kwa maana ya *SUMATRA*, wanataka kuongeza nauli ya wanafunzi kutoka shilingi mia moja kuipeleka juu. Tunaomba serikali itafakari upya suala la kuwapandishia wanafunzi nauli kwenye daladala lifutwe, tafuteni njia mbadala kuwasaidia watu wanaomiliki daladala.

Mheshimiwa Spika, *TBC* wana Mradi wao ambao wameuomba kupitia Wizara ya Habari na Wizara ya Habari wameupeleka Wizara ya Fedha, lakini bado unasuasua; jinsi ya kuiendeleza na kuiboresha *TBC*. Mradi huu ni mzuri, ambapo *TBC* inaweza kujiendesha kibiashara. Tunaomba sana TAMISEMI, Waziri wa Fedha, na Waziri wa Habari na Michezo, mshirikiane kuwasaidia *TBC* ili Mradi huu uweze kukamilika *TBC* iende kibiashara.

Mheshimiwa Spika, tumepewa Makamanda Dar es Salaam, kwenye Wilaya zetu tuna *OCDs*, lakini hatujawatazama kihadhi za ofisi, wanagombania Ofisi na Vituo vya Usalama wa Taifa, naomba Serikali ijitayarishe kujenga Ofisi za *RPCs* Dar es Salaam, *OCDs* na Kamanda wa Kikosi Maalum cha Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuja kufanya uzinduzi wa Panton yetu mpya MV Magogoni; Wanakigamboni tumefarijika sana. Leo hii tunayo MV Kigamboni inatusaidia, lakini naomba kuchukua fursa hii pia kuiomba Wizara ya Miundombinu, kuhimiza ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Najua mmetusaidia sana kwenye vivuko, lakini tulitaja kwenye ilani kwamba, tutajenga Daraja la Kigamboni, naomba sana suala hili nalo litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, maliasili ya Dar es Salaam ni bahari; wenzetu wana migodi, dhahabu, almasi na kadhalika na wanapata mrabaha. Sisi Dar es Salaam, maliasili yetu ni bahari, ambayo inatumika kwa Bandari ya Dar es Salaam; tumelisemea mara nyingi lakini Serikali inalipuuza. Halmashauri zetu zina majukumu mengi mazito, Jiji la Dar es Salaam linakua kila siku, tunaomba mtugawie asilimia kidogo kutokana na pato la bandari ili Haalmashauri zetu za Dar es Salaam, tuweze kugawana kuendesha Halmashauri hizi kwa ufanisi zaidi. Kwa nini walioko kwenye migodi wapate sisi rasilimali yetu ya bahari tusipate? *(Makofi)*

Mhehsimiwa Spika, takrima imepigiwa kelele sana hapa, tena walioipigia kelele ni wasomi wazuri kabisa, wanasafiri nje ya nchi na Kamati za Bunge na Spika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na wa mwisho kwa jioni hii atakuwa Mheshimiwa Esther Nyawazwa.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja Hotuba ya Waziri Mkuu, pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Kabla ya hapo, napenda kutoa pongezi na shukrani kwa hotuba nyingi ambazo zimetusaidia kutupa mwelekeo wa jinsi ya kuchangia, nikianzia na zile za makadirio ya mapato na matumizi bila kusahau ya Kambi ya Upinzani, ilikuwa ni nzuri sana na bila kusahau Hotuba ya jana ya Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia, napenda niweke wazi msingi wa michango yetu; kwanza, tunaangalia ahadi za Serikali; pili, tunaangalia utekelezaji wake na jinsi gani Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezeka kulingana na ahadi ambazo zilitolewa kipindi kile chote. Lengo ni kuboresha au kukumbusha yale ambayo hayajafanyika ili wananchi waweze kupata yale ambayo walitarajia kupata baada ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, ametengeneza *Strategic Plan* nzuri sana. Kama itafanya kazi na atawezeshwa, Mkoa wetu utapata mabadiliko makubwa sana. Kwa hiyo, nampongeza kwa kazi nzuri anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na muda, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango. Nitaanza na suala la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ambao unatarajiwa kufanyika Mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mizengwe mingi sana katika shughuli hizi za uchaguzi. Mimi ninao mfano mmoja, uliotokea Kigoma katika Kijiji cha Herembe, Kigoma Vijijini. Aliyechaguliwa pale alikuwa ni Mwenyekiti kupitia CHADEMA, lakini bahati mbaya sana, Mkurugenzi wa Halmashauri wa kipindi hicho, aliamua kwa makusudi, kutengua na baadae uchaguzi mwingine ukafanyika. Mpaka leo, kesi iko mahakamani, hata Waziri wa TAMISEMI akitaka nitamletea *case number*.

Mheshimiwa Spika, vile vile kumekuwa na matatizo kwa wale Wenyeviti ambao walichaguliwa, hawapati ushirikiano wa kutosha kwa Watendaji wa Vijiji kwa mfano, Kijiji cha Sigunga na Kijiji cha Kaseke. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba elimu ya kutosha itolewe kwa Watendaji, wafanye kazi na yeyote yule ambaye anachaguliwa na wananchi. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende kwenye Kilimo Kwanza. Tumekuwa tukisikia kaulimbiu nyingi sana kuhusiana na kilimo, lakini tatizo ni kwamba, utekelezaji haupo. Ukiangalia mwaka jana, kilimo pia kilikuwa kwenye kipaumbele, kilikuwa na asilimia saba tu ya bajeti na mwaka huu tunaambiwa Kilimo Kwanza, lakini asilimia ni ile ile saba ya bajeti. Kwa hiyo, tunaona utekelezaji unawezekana ukawa vile vile. Tatizo kubwa ni kwamba, kilimo chetu sisi tunategemea mvua, sasa kama tunategemea mvua maana yake ni kwamba, kukiwa kuna ukame kile Kilimo Kwanza hakiwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu nimemsikia akisema, tunatakiwa tuwaite Wachina waje watengeneze hapa pembejeo kwa ajili ya kilimo, lakini naomba niwakumbushe kwamba, tulikuwa na kiwanda cha ZZK Mbeya na kiwanda kingine cha UFI Dar es Salaam; vyote vimekufa. Sasa badala ya kuleta Wachina waje watengeneze kama Mheshimiwa aliyeongea ananisikia; naomba nimkubushe kwamba, tunatakiwa tushirikiane kuiambia Serikali ihakikishe ZZK Mbeya na UFI Dar es Salaam vinafanya kazi ili viweze kutengeneza pembejeo za kilimo ambazo zilikuwa zikitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona Kilimo Kwanza, kitafanikiwa kama tukiwa na Maafisa Ugani wa kutosha. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameonesha kwamba, ndiyo sasa hivi wanaanza kusomesha Maafisa Ugani wengi. Kwa hiyo, huo ni mpango wa muda mrefu sio wa sasa hivi. Tatizo lingine, hatuna viwanda vya usindikaji.

Tatizo lingine ni miundombinu, sasa hivi ndiyo tunaunganisha barabara za mikoa, kwa hiyo, bado za wilaya na vijiji; hivyo bado kilimo kwanza hakiwezi kufanikiwa kwa sababu unatakiwa utoe mazao mashambani kuyafikisha kwenye soko. Tatizo lingine ni nishati, umeme bado ni kitu cha anasa katika nchi ya Tanzania, kwa hiyo, Kilimo Kwanza hakiwezi kufanikiwa kama mambo hayo hayatatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea suala la matumizi ya Serikali. Naomba matumizi ya Serikali yaendane na hali halisi ya uchumi ulivyo sasa. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake alisema kwamba, amepunguza makongamano na warsha. Hiyo pekee haitoshi, kuna vitu vingi sana vya kufanya kuhakikisha kwamba, tunapunguza matumizi ya Serikali ambayo hayana ulazima.

Mheshimiwa Spika, nitaomba atuambie mikakati mingine ya kupunguza matumizi ya Serikali tukiangalia Wizara zetu, Idara na Taasisi nyingine za Serikali, ikiwemo pia mikoa, tuige mfano wa Bunge; Bunge lilikuwa na kawaida ya kufanya kazi zaidi ya miezi miwili kama na wiki mbili na nusu au wiki tatu, lakini sasa hivi tunafanya kazi katika kipindi cha miezi miwili na kama wiki tatu. Kwa hiyo, Bunge linatakiwa lipongezwe, limeangalia hali halisi, imebidi Wizara nyingine zifinywe zijadiliwe siku moja, lakini ni kutokana na hali hii ya uchumi ili kuendana na hali halisi tusiseme tu bila kutekeleza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee matumizi ya magari, nchi yetu kumekuwa matumizi ya magari ya serikali hayadhibitiwi vya kutosha. Nilikuwa naomba hilo Ofisi ya Waziri Mkuu iliangalie hilo. Suala lingine ni kwamba, nimetoa mfano mwaka 2005, nilikuwa Kigoma sitamtaja ni nani; kulikuwa kuna mkutano unatakiwa kufanyika Bagamoyo, ilitolewa tiketi ya ndege kwa mtu anayekwenda na bado akaandaliwa dereva akapewa mafuta gari itangulie kwenda Bagamoyo, *two days before* yeye kuondoka. Sasa hayo ni matumizi mabaya, anataka tiketi ya *go and return* na bado gari liende; liwe na mafuta na *contingency money*, kwa sababu barabara yenyewe kwanza ni mbaya, linaweza likatokea tatizo lolote.

Kwa hiyo ni matumizi mabaya; kama anakwenda, aangalie kiasi fulani cha pesa ambacho angeweza kutumia kwa gari lile ambalo linakwenda kumsubiria kule *airport*, angekodi hata taxi ni gharama nafuu kuliko kulitoa gari Kigoma mpaka kufika huko na hiyo sio kwa huyo tu ninayemzungumzia, wako wengine wengi, wanaofanya hivyo ndani ya serikali. Kwa hiyo, tuangalie sana. *(Makofi)*

Naomba suala la ununuzi wa magari kiholela liangaliwe, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, Ripoti ya CAG pia imetoa pendekezo lake kwamba, kitengwe Kitengo Maalum katika Wizara ya Miundombinu, kiwe kazi yake ni kununua magari ya serikali na kuwe kuna Mpango Maalumu wa manunuzi ya mwaka, ijulikane kwamba Wizara gani inataka kununua magari mangapi, kuliko manunuzi ya kiholela. Sasa hivi tumekuwa tukiona watu wananunua magari wanavyojisikia tu, haiangalii daraja la mtu, wadhifa wake, yaani magari kila mtu akijisikia; mimi ninataka new model V8 ananunua tu na hapa ndani kuna mfano. Magari mengi ya Mawaziri wameanza kazi rasmi 2006,

walikuwa na magari lakini wengi wamebadilisha wanatumia V8 ambayo vipuri vyake ni bei ghali na yanatumia sana mafuta. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba mambo kama hayo, yaangaliwe sana ingawa Mheshimiwa Rais ameshasema kwamba, wasitishe ununuzi wa magari ya aina hiyo. Kwa sababu nchi yetu ni maskini ni sawa sawa na mama ambaye umependeza, umevaa dhahabu hadi miguuni, lakini mtoto wako anakufa kwa utapiamlo. Nchi hii kama unavyofahamu, bado tunategemea sana wafadhili wa nje ili kujiendesha, kwa hiyo, hatuna haja ya kutumia magari ya namna hiyo wakati nchi yetu ni maskini na tunategemea wafadhili kutoka nje katika bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala lingine la matumizi ya sheria ya fedha na kanuni za fedha; tumekuwa na tatizo sana hasa ukiangalia Ripoti za CAG, ameweka wazi mambo mengi ya jinsi ambavyo pesa zetu zinapotoa. Naomba nitoe mfano; kwa kutokufuata Sheria ya Fedha na Kanuni za Fedha, tumepoteza pesa nyingi, kwa mfano, nilichukua katika kurasa tofauti kwa hiyo niliweka kwenye daftari langu. Kwa mfano, masurufu yasiyorejeshwa peke yake kwa mwaka 2006/2007 ni shilingi 3,138,942,000, hayo ni masurufu peke yake. Malipo yenye shaka, shilingi 82,820,848,330; malipo yasiyo na hati za malipo shilingi 1,288,000,000; malipo hewa shilingi 10,490,000,000; yale ambayo wametoa kwa vifaa na huduma hayajaja na malipo ambayo yamefanyika kabla ya kupokea vifaa. Ofisi ya Waziri Mkuu, naona wanaongoza hapa, kwa mwaka 2007/2008 kuna shilingi bilioni 1,112,000,000. Sasa haya ni mambo ya kuangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna suala la udhaifu katika kuingia mikataba; mwaka 2006/2007 hapo bado sijaangalia kitabu hiki kipya kuna shilingi 12,444,000,000 ambazo zimesababishwa na udhaifu au uingiaji mikataba mibovu. Sasa ukiangalia pesa zote hizi ni nyingi, inabidi Kanuni za Fedha zifuatwe na watu ambao wanahusika kama ni Maafisa Masuhuli wachukuliwe hatua, ile Sheria ya Tozo ifanye kazi na kama hali hiyo itaendelea, washushwe vyeo wawekwe watu wengine, kwa sababu watu wamezoea kufanya kazi *as business as usual.* Kwa hiyo, naomba sana haya mambo yaangaliwe kwa sababu tuna matatizo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia tufanye juhudi ya kupunguza matumizi ya kawaida ya ndani, yaani *recurrent expenditures.* Kumekuwa na kawaida, katika matumizi ya kawaida bajeti ni kubwa, matumizi ya maendeleo bajeti ni kidogo. Nikichukulia mwaka 2006/2007, Serikali Kuu ilitenga shilingi trilioni moja bilioni tisini na tisa na ushee, kwa ajili ya matumizi ya kawaida mikoani. Shilingi 66,266,000,000 zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya mikoa, sawa sawa na asilimia sita tu ya ile bajeti ya matumizi ya kawaida. Sasa utaona matumizi ya kawaida ni makubwa kuliko yalivyo matumizi ya maendeleo. Kingine kinachoshangaza, Kitabu cha CAG kimeonesha mwaka 2008, shilingi 99,144,000,000 hazikufika mikoani, hizi zilikuwa ni pesa za maendeleo. Sasa nitaomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atuambie; je, Hazina hawakutoa zilichelewa au zilikuwa za wafadhili hawakuzitoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa *trend* inavyojionesha, jinsi ambavyo watu hawafuati kanuni za pesa na jinsi ambavyo tunafanya matumizi makubwa, yanakuwa ni ya kawaida halafu matumizi ya maendeleo yanakuwa ni kidogo. Naomba nitoe mfano wa Bajeti ya Mwaka 2008/2009, tulikuwa tunatakiwa kutumia shilingi trilioni 7.3, katika hizo shilingi trilioni 2.43, tulikuwa tunategemea wahisani, sasa shilingi trilioni 4.8 ndiyo ilikuwa matumizi ya kawaida, shilingi trilioni 2.5 matumizi ya maendeleo, maana yake ni kwamba, hela nyingi zitakwenda kwenye matumizi ya kawaida, halafu pesa kidogo zinaingia kwenye matumizi ya kawaida. Ukiangalia bajeti ya mwaka huu, hali ni hiyo hivo tena, sasa hivi tunategemea wahisani shilingi trilioni 3.18, maana yake ni kwamba, wasipotoa pesa hizo kama hali yao ya uchumi itakuwa mbaya, hatuwezi kwenda popote, tutakwama kibajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka, nimalizie kipengele kingine; hivi karibuni kutakuwa kuna mabadiliko ya katiba; kuna kitu ambacho napenda kushauri kama mabadiliko hayo yatafanyika, tumekuwa na Wizara zisizojulikana au zisizo na idadi, yaani Mheshimiwa Rais anaweza akaamua tu kwa sababu ni kweli Katiba inamruhusu kufanya hivyo. Nashauri kama kinavyoainisha kifungu cha 8(1)(a), naomba nisome: Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba na ibara ya 63 na 64 inaonesha kazi za Bunge na mahusiano kati ya Bunge na Wananchi.

Sasa kwa maana hiyo, nilikuwa nafikiri ni vyema, pamoja na kwamba, tuna kifungu ambacho kina-*state* idadi kamili ya Mawaziri, labda tuseme kutakuwa *may be* na Naibu Mawaziri labda kumi na Mawaziri wenyewe kumi na tano, lakini kuwepo na kifungu kingine ambacho kinaainisha kwamba, Bunge litashiriki katika kuwathibitisha kama anavyothibitishwa Waziri Mkuu. Sidhani kama hapo kuna ubaya, kwa sababu nikitoa mifano ya nyuma kwa kutokuwa na idadi kamili, kwa kipindi cha mwinyi, walikuwepo Mawaziri 40, ambapo Mawaziri *full* ni 26, Naibu Mawaziri walikuwa 14. Kipindi cha Mheshimiwa Mkapa, Mawaziri walikuwa 45; Mawaziri kamili 28 na Naibu Mawaziri 17.

Kipindi cha Awamu Nne cha Mheshimiwa Rais Kikwete, alianza na Mawaziri 61; Mawaziri 30 na Naibu Mawaziri 31, kabla ya baraza kuvunjwa na sasa ni 48 akiwemo Waziri Mkuu mwenyewe, Mawaziri 27 na Naibu Mawaziri 21.

Mimi naona kwamba, ukizingatia malipo ya stahili zao, wanahitaji magari, wanahitaji nyumba Dar es Salaam na Dodoma, wanahitaji madereva na magari na wasaidizi na kila kitu. Sasa wakiwa wengi sana, bado nchi inaendelea kubeba mzigo mkubwa kama nilivyosema kwamba, matumizi yanakuwa makubwa kuliko matumizi ya maendeleo; yaani matumizi ya kawaida yanakuwa makubwa kuliko matumizi ya maendeleo. Kwa hiyo, nilikuwa naona kuna umuhimu wa kufanya kitu kama hicho katika mabadiliko yajayo ya Katiba na tumeshaona kwamba, wingi vile vile si tija kwa sababu bado nchi yetu ina matatizo yale yale ya umaskini siku zote na tumekuwa tukiongea tu bila mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, mimi nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu na kumpongeza yeye na timu yake. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu mambo yanafanywa hawataki kuyaona, kuna maendeleo yanafanywa hawataki kuyaona wala hawataki kusikia; kuna watu wanakuja hapa na ajenda ya kututoa kwenye mwelekeo wetu na sisi tusijiingize kwenye fikra zao tukaondokana na mipango yetu mizuri ya nchi yetu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mkisimama mkatoa mwongozo hapa, mnazidi kuwapa umaarufu, waacheni waseme watashindana watashindwa. Sababu, wamezoea kushindwa, hivi leo tunampongeza Mkapa kwa kuthubutu kuanzisha Mradi wa Maji Shinyanga. Chuo Kikuu cha Waislam kimetokana na nani? Uwanja wa Taifa wa Mpira tunajivunia Afrika umetokana na nani? Jengo hili bila Mkapa tungekaa humu ndani? Watu tunasahau hatuoni, hatusikii, mnafulia mambo mazuri ya Mkapa; habari ndiyo hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Ilala, sasa haya mambo lazima uende na ki-Ilala; nampongeza Rais Kikwete kwa kuthubutu kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma, bila Rais kuthubutu tusingejenga chuo hiki na kuanzia sasa kila kiongozi athubutu kuleta maendeleo ya nchi hii. Namwomba Rais vile vile athubutu kutumia mifuko ya nchi yetu kujenga balozi zetu Washington, Uingereza na Abuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Balozi hizi hazitatumika tu kwa kazi za Serikali, zitatumika kwa kukodisha majengo makubwa ambayo yako ndani na yatatupatia mapato makubwa sana. Namwomba Rais na hili athubutu kulifanya, atajijengea heshima kubwa sana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Watumishi wa Umma, lazima tubadilike kifikra, tuachane na mambo ya kizamani, tutazame dunia inavyokwenda. Watumishi wa Umma, lazima wajue wateja wao ni nani; Watumishi wa Umma wateja wao ni wananchi. Watumishi, mteja wao sio Waziri Mkuu. Watumishi wa Umma waelewe kwamba, serikali haichapishi pesa kuwalipa mishahara, pesa hizi zinatokana na wanyonge wa taifa hili. Kwa hiyo, tubadilike sasa, tujue kwamba wateja wetu ni wananchi, tuwaheshimu, tuwaenzi na tuwathamini.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengi; kuna suala la Wakazi wa Kipawa, juzi nilikuwa na mkutano Kipawa, wananchi hawa wamekaa zaidi ya miaka kumi na tano, hawaruhusiwi kuboresha mazingira yao, lakini hawakukatazwa kuzaliana. Leo wanaongeza vizazi katika mazingira magumu, kwa sababu wamekatazwa wanangoja fidia ya kuhama Kipawa, Kigilagila, Kitunda, Kipunguni na Relini Kiwalani.

Mheshimiwa Spika, naomba kama hili suala linakuwa gumu, gharama ya fidia ni kubwa, tutafute kiwanja kingine, badala ya kulipa fidia na kujenga kiwanja kingine, hizi

pesa za fidia ziboreshe kiwanja kingine; hawa watu waachiwe wakae katika mazingira salama na wawe na amani na nchi yao na taifa lao na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza mambo ya JKT, maadili ya nchi yetu yameporomoka kwa sababu tumepuuza JKT. Serikali haitakiwi kila kitu ifanye, kama Mashirika na Serikali inapanga fungu la mafunzo sasa hivi, Makatibu Wakuu na Serikali wapange mafungu ya kutumia kuwapeleka watumishi wao JKT, kupunguza mzigo huu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la Shirika la Nyumba ni zito sana; shirika hili lengo lake lilikuwa kusaidia wanyonge waishi katika mazingira mazuri, sheria ikabadilishwa ili wafanye kazi kibiashara. Tangu waambiwe wafanye kazi kibiashara, shirika hili limekuwa linaporomoka, linavunja Kanuni ya Manunuzi, linavunja kila taratibu ya misingi ya wapangaji, misingi ya nyumba nchini Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, Shirika la Nyumba si suala la Dar es Salaam, ni suala la Tanzania nzima; tushikame na Waziri, alielewe Shirika hili kuanzia Bodi mpaka Watumishi wake hawafai.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali inashindwa nini kuvuta maji kutoka Rufiji kuja Dar es Salaam kwa awamu? Mpango wa Maji Dar es Salaam ni mradi mkubwa sana, kila mwaka watengeneze kilomita 30, baada ya miaka sita, saba, maji yatakuwa yameshakuja. Kwa hiyo, tusiwe na fikra mgando, ndiyo maana nasema Watumishi wa Serikali wabadilike, wawe na mtazamo wa maendeleo na uchungu wa uzalendo wa taifa hili, ikiwa kila mtu atakuwa anafanya kazi anavyotaka mwenyewe bila kuwa *under innovation* hatuwaweza kufika.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa nianze na michezo, lakini nikaona nianze na lile la Mheshimiwa Mkapa, kwa sababu ya umuhimu wake. Toka tuanze uhuru, bajeti ya michezo ni ndogo sana na michezo ina *program*, tukitegemea wafadhili, wahisani, hawa wanasaidia tu wakati kuna maendeleo au kuna ushindi. Siku ambazo timu hazi-*perform* vizuri na wao wanaingia mitini, nampongeza Maximo kwa kazi nzuri anayoifanya. Naipongeza Timu ya Ilala, iliyoweza kushinda Kombe la Taifa Cup na iliweza kukaa Ramada Hoteli, haikukaa machakani kama timu ya mtu fulani, simtaji mwenyewe. *(Kicheko)*

Hivi sasa tunajiandaa na Coca Cola, Mheshimiwa Waziri, Jumapili tutakuwa pamoja na Wabunge wa Dar es Salaam na Ilala ni Dar es Salaam; ni lazima kombe lije Ilala libaki Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kuwa inajiingiza kwenye kila mradi, haina pesa, haina *capacity*. Kwenye barabara iko kodi ya mafuta, lakini bado haitoshi. Mashirika ya Pensheni yangeshirikishwa, yangeweza kujenga barabara na kipindi cha miaka kumi na tano au ishirini, kutoka Mwaza mpaka Mtwara wangeshaweza kurudisha pesa zao.

Mheshimiwa Spika, kuna magari ambayo tunafikiri wanalipa kodi ya mafuta hawalipi; magari makubwa yanatoka nchi za jirani yanapeleka mizigo yao kupitia Tanzania, wanajaza mafuta wanakotoka na wanakuwa na *spare* ya mafuta zaidi ya lita 1000 kwenye gari wanarudi nayo, wanatumia barabara kwa kulipa gharama ndogo sana. Lazima kuwe na *road toll,* kungekuwa na *road toll* ya Dar es Salaam - Dodoma, kila mwaka tungepata pesa si chini ya shilingi bilioni 15 mpaka 20.

Wenye magari wanao uwezo wa kuchangia, tuisaidie serikali. Vile vile serikali ikubali *road toll* za barabara zetu, kwa kipindi hiki cha miaka mitano, tungeshaweza kabisa kujenga barabara nchi nzima kwa kutumia *road toll*.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ni *unique*, ndiyo sehemu ambayo inakusanya mapato ya nchi nzima. Kwa hiyo, utawala wa Dar es Salaam nao uwe tofauti. Leseni zimekatazwa zisikusanye kwenye Manispaa zote za Dar es Salaam. Huu ni mpango wa nchi nzima, leseni za biashara zinanyima mapato Mkoa wa Dar es Salaam; kwa Manispaa hizi tatu, sio chini ya dola milioni nane kwa mwaka. Tunaomba hili Serikali walitazame.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la ajira, Serikali itazame mfumo wake sasa wa kuajiri, huu mtindo wa mtu ukishapewa barua ya ajira unasubiri mpaka miaka sitini, tuna vijana wengi kutoka vyuoni hawana ajira kwa sababu walioko kwenye kazi hawatoki na ndiyo maana hata tija ya ufanisi wao hakuna. Watu wapewe mikataba, kutoa fursa ya wanafunzi watakaotoka UDOM, University of Dar es Salaam na vyuo vingine na wao waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Naishukuru NSSF, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kujenga Jengo la Machinga. Nataka niwatahadharishe Wananchi wa Dar es Salaam, nasikia kuna mtindo umezuka, inabidi watu walipie pesa kuingia kwenye Jengo lile! Leo nimesikia kuna watu wamepigwa picha, hatujamruhusu wala hatujatoa nafasi kwa mtu yeyote kuingia kwenye Jengo lile. Kama kuna mtu kaingizwa huko mitaani, basi mkachukue hela zenu. *(Makofi)*

Nawapongeza TRA, lakini bado iko *room* ya kuongeza mapato. TRA mnafanya kazi nzuri endeleeni. Wanajeshi wa zamani *(King African Rifle),* wazee hawa wanapita maofisini kwetu, tunajua kwamba, wanateseka. Tumewasiliana na Balozi wa Uingereza anasema; katika mchango wake wa *Budget Support* ya Tanzania, hao nao wafikiriwe. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hawa wazee wako wachache; Jengo lao la *Tanzania Legion* mmelibeba, pesa zao hamuwapi, tunabaki sisi Wabunge na Madiwani ndiyo tunapita sasa kuwabeba.

Mheshimiwa Spika, pili, tunatangaza mafiga matatu kwenye uchaguzi kuwabeba Madiwani, tukishachaguliwa tunabaki mafiga mawili, Madiwani hatuwatazami, tuwakumbuke na hii ni Wizara inayohusika, Mheshimiwa Kombani nakuomba uwatazame hao.

Mheshimiwa Spika, hospitali zetu zimepunguza vifo vya wazazi na watoto, takwimu zipo zitazameni mtaona tulipo na tunakotoka. Leo nilikuwa na mazungumzo na

Waziri wa Afya, gharama za vipimo hospitali ziko juu sana, wananchi wa kawaida hawawezi kuzimudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, TAMISEMI iweke utaratibu, wanafunzi wakiwa katika mapumziko wawe na *summer jobs* kwenye Halmashauri. Wakianza kufanya *summer jobs* kwenye Halmashauri, wataweza kupata *experience* na wataweza kupunguza deni la mikopo, ambayo nchi zote wanafanya utaratibu kama huu. Sioni sababu kwa nini sisi tusifanye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, Serikali Kuu kupenda kurukia Miradi ya Jiji la Dar es Salaam na hawarukii kwa sababu wanaweza, wanarukia kwa roho mbaya halafu wanashindwa inabaki inatereza. Tulikuwa na barabara ya Tegeta – Mwenge; 50% *road toll*, 50% *grant*, hawa nao wameharibu haribu wametunyang'anya imekufa. Tumeuanzisha Mradi wa *Dar es Salaam City Council*, zimeanza kuja pesa za World Bank, tumenyang'anywa na hauna mwelekeo, wanatuambia leo haya mabasi yatapita kwenye barabara maalumu, Mandela ile inatengenezwa kuna barabara ya mabasi pale.

Mheshimiwa Spika, wewe unajua, kuna barabara mpya inatengenezwa Mandela, kuna alama ya kupitisha basi peke yake pale. Kwa hiyo, nilikuwa naomba miradi ambayo tumeibuni na sasa Ilala inathubutu kujenga nyumba zake Mchikichini, tunaomba *support* ya Serikali.

Tulipouleta Mradi huu 2007, kwa roho mbaya tu ukaharibiwa. Tunataka kunusuru wananchi, wakae katika mazingira, nyumba safi, salama na za heshima; mwekezaji yupo. Mtu anakaa kwenye meza anasema huu haufai, akirumbana na mkewe hasira zake anatumalizia sisi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Marmo, kwa kazi nzuri ya kuisimamia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa, kama alivyosema mzungumzaji aliyemaliza kuongea sasa hivi; ukweli na uwazi ni kwamba, macho hawana, hawaoni wala hawasikii, lakini CCM itaendelea kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara hii ndipo palipo na maendeleo ya wananchi wetu huko tunakotoka. Mbali ya haja ya kuangalia wananchi wetu, maendeleo wanayapataje kupitia Wizara hii, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaanzia 2005 – 2010; hivyo mengi tumeyafanya, barabara mnaziona za lami. Inasikitisha mnasema kuna maeneo CCM haijafanya kitu wakati unaona umeme upo maeneo mengi, barabara za lami, shule za sekondari kila kata, walimu ndiyo maji kila mahali, hapa Dodoma penyewe maji

yalikuwa ya shida sasa hivi unafungulia tani yako tu unaoga, umesimama haya yote ni mafanikio ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie hali halisi ya siasa nchini. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa nne, ameelezea hali halisi ya siasa ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakufahamu tangu mwaka 2000; ni mchapakazi mzuri sana na Mawaziri wote wanaofanya kazi katika Wizara yako, wanafanya kazi vizuri sana. Sasa upole umezidi, naomba sasa utekeleze Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, upole huu ni mzuri lakini katika hali ya kisiasa, utatufikisha mahali pabaya. Katika kuimarisha demokrasi nchini kwetu, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, unieleze leo; huyu Msajili wa Vyama vya Siasa yuko likizo; haoni tunakoelekea? Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameeleza kupewa fursa sawa ya kunadi na kushindanisha sera zao, inasikitisha sasa na amenielezea kuna vyama kumi na saba; hivi Msajili wa Vyama anavyosajili hivi vyama wanaleta ilani zao? Je, wanawaeleza wananchi watawafanyia nini?

Mheshimiwa Spika, tunakoelekea mwaka kesho ndiyo uchaguzi na tunaanza mwaka huu, mimi nimejifunza mambo mabaya sana yaliyofanyika katika Jimbo la Busanda na Msajili amenyamaza kimya! Hivi kuna sheria gani kwenye mkutano wa chama fulani wengine waje kuzomea; haya maadili yanatoka wapi? Amani na utulivu vimesimamiwa na Chama cha Mapinduzi, inafikia mahali chama fulani mkutano uko upale, helikopta inakuja kutua maeneo yale inaleta vumbi kibao. Sisi tumerudi hapa tunakohoa wakati tunainadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Usumbufu unaletwa na Chama kingine, Msajili amenyamaza kimya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hili nakuomba baba uwe mkali. Msajili wa Vyama vya Siasa, aanze kuonesha mfano bora kwa chama hiki ambacho kimeshaanza kuonesha vurugu katika Jimbo la Busanda. Unachukua bendera ya chama cha mwenzio unaichoma moto, hapo ni kuonesha kwamba, tunataka kugombanishwa sisi wenyewe Watanzania. Tutakimbilia wapi; sisi ni watu wa amani, kama CCM siku ile Busanda ingeamua kubishana na wale watu waliofanya kitendo kile, ilikuwa ni hatari.

Mheshimiwa Spika, zikitokea kauli ndani ya Bunge letu Tukufu, tunapigwa kwa kanuni, sasa msajili hawezi kutumia sheria zake ambazo amekabidhiwa na Serikali hii kuhakikisha kwamba, Chama ambacho kimeshindwa kusimamia maadili ya Watanzania kinafutwa. Tuna vyama kumi na saba, tunazuiwa na nini kukifuta chama kimoja kinachochokodisha vijana kuja kufanya fujo kwa wananchi ambao wanataka kupiga kura?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika - Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kanuni ya 64 inasema kwamba, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru na mawazo na

majadiliano katika Bunge, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Spika, wakati anachangia amezungumzia suala la uchaguzi wa Busanda; katika Uchaguzi wa Busanda vilishiriki vyama vinne; CHADEMA, CCM, UDP na CUF. Katika maelezo yake amesema kwamba, kuna chama kilichochoma bendera ya chama fulani; naamini haizungumzii CCM kwa sababu ni chama chake, anavizungumzia hivi vitatu vilivyobakia; atuelezee na athibitishe ni chama gani kilichochoma hiyo bendera. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Esther Nyawazwa, alikuwa mwangalifu sana, vinginevyo itakuwa hadithi ile ya Mudhihir kwamba, kondoo mwenye manyoya mengi ndiyo anasikia baridi. (*Kicheko)*

Kwa hiyo, sioni shida; Busanda imekwisha, Mbunge wa Busanda kazungumza leo, sasa tuangalie Biharamulo tu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunilinda, nilikuwa nazungumzia hali halisi tunakoelekea. Nilikuwa natoa angalizo kubwa sana, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama tutaendelea kuangalia hali halisi ilivyo, wananchi wetu hawataweza kutumia haki yao ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, itasikitisha tutakapoanza kuchagua Wenyeviti wetu wa Vitongoji na Vijiji na hatimaye tuingie Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho, kama Msajili hataweza kurekebisha hali halisi. Nina mashaka na huko tunakoelekea. Naomba hilo walielewe, Msajili naomba afanye kazi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la kilimo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulizungumzia suala la Kilimo Kwanza. Tusingeliongelea suala la Kilimo Kwanza mwaka 2005 wakati hatuna miundombinu, tuliamua kwenda mwaka hadi mwaka, kwa kuweka vipaumbele. Sasa ni muafaka kabisa kuwa na Kilimo Kwanza, kwa sababu tumeboresha barabara zetu ili nafaka zitakapozalishwa zipite. Tumeboresha shule zetu na tumeweka kipaumbele kwenye elimu. Kwa hiyo, tuna vipaumbele ambavyo sasa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inajua watu wake inataka kuwapangilia kiasi gani.

Ninaomba basi, kama tunazungumzia suala la Kilimo Kwanza, nijaribu kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu; tumejiandaa vya kutosha kuhakikisha tunatoa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu? Zana za kilimo za kisasa zitawawezesha wananchi wetu asilimia 80 wako vijijini wapate nyezo za kisasa? Tumejiandaa vya kutosha kuhakikisha kwamba, tuna maeneo ya kutosha wananchi wetu walime mashamba ambayo yanaweza yawanufaisha?

Kwa hiyo, tukisema Kilimo Kwanza tujaribu kuangalia pande zote mbili. Naomba niwapongeze sana ndugu zetu wa Mikoa ya Kusini, wanajitahidi sana kulima. Nakuja katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, kuna Zao la Pamba, inasikitisha kuna matrekta

yametengwa lakini kwa wakulima wa pamba hatukutengewa kabisa. Mwaka huu, bahati nzuri sana, kwa mfano mimi nimesomea sana zao la mpunga, lakini mwaka jana baada ya kuhamasishwa bei ya pamba, nimehakikisha pale Malya nimepewa ekari mbili na KKKT. Nawashukuru sana na nimelima pamba.

Cha kusikitisha, bei ya pamba nayo imeshuka; tuangalieni kwa jicho la huruma Kanda ya Ziwa. Waangalieni Wakulima wa Zao la Pamba angalau tusogezwe kidogo, shilingi 360 ni bei ndogo sana; wametumia gharama kubwa kuweka mbolea na kununua mbegu. Naomba mtuangalie ndugu zangu na mtusaidie zana za kilimo kama matrekta yanaishia upande mwingine. Tumesema tunagawana hii keki, tugawane pande zote nne, tuhakikishe kila mtu anafaidika.

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba nizungumzie suala la mikopo ya wajasiriamali. Mkakati wa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuhakikisha kwamba, wajasiriamali wadogo wanafanikisha kupewa mikopo, utaratibu uliotumika kwa miaka ya nyuma kwa kweli wananchi wengi hawakuweza kufikiwa na mikopo hii. Nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu; ili tuweze kuwapata akina mama wengi walioko vijijini na tumewahamasisha kwa wingi kuingia katika SACCOS, basi mikopo iwafikie vijijini. Tuhakikishe kwamba, tunaendeleza akina mama, wana uwezo wa kuendeleza biashara zao na ni waaminifu wa kurudisha mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahakikishe kwamba, mikopo hii inafika hadi vijijini ambako miaka ile ya nyuma iliishia mijini tu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la jinsia; tumekuwa tukilizungumzia kwa nadharia tu, kwa vitendo bado hatujalitekeleza. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema kwamba, kuhusu jinsia itahakikisha jinsia zote mbili ni sawa; si kwa upendeleo si kwa kuhurumiwa, lakini ni haki ya jinsia zote mbili. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ndiyo kiongozi wetu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, jaribu kuangalia suala la jinsia bado utekelezaji wake ni mdogo sana; kwanza, jinsia moja inadhalilika sana. Mwanzoni nilianza na Msajili kwa upande wa Jimbo la Busanda, alikuwa ni mwanamke lakini matusi ambayo alikuwa anayapata kutoka kwa Wapinzani, yalikuwa si mazuri ni ya kumdhalilisha mwanamke. Kwa hiyo, niombe sheria hizi tunazotunga za usawa wa jinsia, itusimamie akina mama; popote mwanamke anapochukua fomu, niwaombe sana wanawake wenzangu, pamoja na akina baba, tuhakikishe kama ni mwadilifu, uwezo huo anao na tumuunge mkono.

Niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ihakikishe suala la jinsia nalo linatekelezeka. Mimi nilikuwa na machache hayo, lakini niliomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, suala la hali ya kisiasa uliangalie kwa macho mawili; tunakokwenda ni kubaya, kama hawawezi kulisimamia hili mwaka kesho itakuwa ni vurugu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, dakika zilizosalia hazituwezeshi kuendelea, ila ninalo tangazo moja tu; baada ya kushauria na mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati ya Uongozi ilikaa kikao cha dharura leo na tumeamua kwamba, mjadala kuhusu Hotuba ya Waziri Mkuu utaendelea kesho siku nzima. *(Makofi)*

Tunaheshimu sana michango ya Waheshimiwa Wabunge na hii itatuwezesha kesho kuwapata wachangiaji wengine 23. Kwa hiyo, namwomba Katibu atazame tena namna ya uwakilishi ili kuiweka hali vizuri zaidi, kwa sababu tumegundua mikoa mingine haikupata nafasi nzuri sana; kwa mfano, Kagera. Utafiti unafanywa, kwa hiyo, tutaangalia na nadhani Chama cha CUF kilikuwa bado hakijapata uwakilishi wa kutosha. *(Makofi)*

Hata hivyo; ni vizuri niwataje watatu wa kesho, baada ya hapo itakuwa tena mpangilio mwingine. Tutaanza na Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, halafu Mheshimiwa Charles Mwera, Mbunge wa Tarime; hao watatu. Mkiona orodha kidogo imebadilika, jamani tusilaumiane, kwa wale watakaokosa nafasi, tutatoa kipaumbele katika Wizara nyingine katika sekta ambazo zitafuata.

Baada ya hayo, nawatakia jioni njema na sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Alhamisi, saa tatu asubuhi.

*(Saa 07.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 25 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*

## VIAMBATISHO

### Vyanzo vya Fedha Zilizotumika Kutekeleza Programu Nje ya Mfuko wa Pamoja kwa Mwaka wa 2007/2008 na 2008/2009

| Mkoa | Halmashauri | Taasisi | Gharama (Sh) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | 2007/2008 | 2008/2009 |
| **Arusha** | Monduli | ADB | 11,700,000,000 | 7,400,000,000 |
| | Karatu | ISF | 41,168,022 | 97,237,220 |
| | | **Jumla** | **11,741,168,022** | **7,497,237,220** |
| **Dar es Salaam** | Manispaa ya Ilala<br>Manispaa ya Kinondoni<br>Manispaa ya Temeke | JICA | | 2,680,412,371 |
| | | **Jumla** | | **2,680,412,371** |
| **Pwani** | Bagamoyo | ARCK | 36,000,000 | |
| | | WIPAS | 6,300,000 | |
| | | LGCDG | 13,000,000 | |
| | | JICA | 20,000,000 | |
| | | Islamic Foundation | | 35,000,000 |
| | Kisarawe | MoEVT | 48,369,202 | |
| | | TASAF | | 51,956,570 |
| | | Tanzania/Japan Food Aid Counterpart (FACT) | | 115,965,328 |
| | | **Jumla** | **123,669,202** | **202,921,898** |
| **Dodoma** | Manispaa ya Dodoma | WAMMA | 279,962,712 | 138,838,200 |
| | Mpwapwa | CMSR | 647,194,000 | 24,643,400 |
| | | Water Aid | | 99,847,600 |
| | | LGCDG | | 203,309,000 |
| | Bahi | World Vision | 800,000 | 26,800,000 |
| | | TASAF | 22,235,130 | 34,875,010 |
| | | LVIA | 0 | 77,710,245 |
| | | CMSR | 0 | 30,660,000 |
| | | KOICA | 804,144,500 | |
| | Chamwino | TASAF | 26,000,000 | |
| | | **Jumla** | **853,179,630** | **636,683,455** |

| Mkoa | Halmashauri | Taasisi | Gharama (Sh) | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **2007/2008** | **2008/2009** |
| **Iringa** | Iringa | TASAF | 45,360,000 | |
| | | Kanisa Katoliki/ACRA | 1,762,178,350 | |
| | | LGCDG | 26,500,000 | |
| | | Kanisa Katoliki | 95,857,833 | |
| | Njombe Vijijini | TZ-Japan Food Aid Couterpart Fund | 17,683,200 | 12,290,001 |
| | | TASAF | 28,333,680 | 16,112,000 |
| | | SHIPO | 67,000,000 | 447,000,000 |
| | | EU/ACRA | | 4,500,000,000 |
| | | Kanisa Katoliki | | 192,000,000 |
| | Njombe Mji | Halmashauri (matumizi ya kawaida) | | 2,600,850 |
| | | TASAF | | 16,112,000 |
| | Makete | Kanisa Katoliki | | 85,600,550 |
| | | UNICEF | | 58,870,000 |
| | | KKKT | | 16,500,000 |
| | Kilolo | World Wide Fund for nature (WWF) | | 19,522,000 |
| | | IYDC NGO | | 73,080,000 |
| | | Kanisa la Kianglikana | 300,200,000 | 199,800,000 |
| | | **Jumla** | **2,343,113,063** | **5,639,487,401** |
| **Kagera** | Ngara | Concern Tz | 82,522,825 | 145,699,000 |
| | Misenyi | TASAF | 46,000,000 | 360,000,000 |
| | | World Vision | 43,000,000 | |
| | | DASIP | | 24,000,000 |
| | Bukoba | World Vision | 70,878,000 | 52,861,000 |
| | | LGCDG | | 30,000,000 |
| | Muleba | UN-HABITAT | 181,800,000 | |
| | | LGCDG | | 37,198,275 |
| | Biharamulo | Concern Tz/BDC | 16,593,400 | 401,139,000 |
| | Chato | Kanisa la Kianglikana - Tumaini | 20,000,000 | |
| | Karagwe | TASAF | 92,590,660 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kanisa la Kianglikana - Tumaini | 3,900,000 | |
| | | **Jumla** | **557,284,885** | **1,050,897,275** |
| **Kigoma** | Kasulu | TASAF | 1,055,400 | 48,866,970 |
| | | UNHCR | 10,889,900 | 40,000,000 |
| | | LGCDG | | 89,945,100 |
| | Kigoma | TASAF | | 2,065,000,000 |
| | | ISF | 922,961,681 | 1,277,943,208 |
| | | **Jumla** | **934,906,981** | **3,521,755,278** |
| **Kilimanjaro** | Mwanga | Halmashauri (Fedha za kawaida) | 8,206,520 | |
| | Same | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 23,264,000 | |
| | | TASAF | 49,000,000 | |
| | | ISF | 310,616,499 | 738,732,176 |
| | Hai | KfW | 1,200,000,000 | 1,000,000,000 |
| | Moshi | KfW | 2,627,481,600 | 5,458,972,536 |
| | | **Jumla** | **4,218,568,619** | **7,197,704,712** |
| **Lindi** | Nachingwea | TASAF | 27,021,670 | |
| | Kilwa | TASAF | | 51,000,000 |
| | Lindi | TASAF | | 135,000,000 |
| | Ruangwa | TASAF | | 330,847,000 |
| | | **Jumla** | **27,021,670** | **516,855,600** |
| **Manyara** | Simanjiro | TASAF | | 18,002,700 |
| | | Ilaramatak | | 110,000,000 |
| | Babati | WaterAid/ADRA | | 1,200,000,000 |
| | | World Vision | | 64,000,000 |
| | Mbulu | Farm Africa | | 190,000,000 |
| | Hanang’ | DMDD | | 230,000,000 |
| | | Livingwater Int. | | 120,000,000 |
| | | Farm Africa | | 94,000,000 |
| | Kiteto | Benki ya Dunia | 9,969,544,374 | |
| | | KINAPA | | 5,000,000 |
| | | TAWISA | | 6,800,000 |
| | | **Jumla** | **9,969,544,374** | **2,037,802,700** |

| **Mkoa** | **Halmashauri** | **Taasisi** | **Gharama (Sh)** |
|---|---|---|---|

| | | | 2007/2008 | 2008/2009 |
|---|---|---|---|---|
| **Mbeya** | Jiji la Mbeya | DADS | 4,640,000 | |
| | Rungwe | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 581,151,480 | 3,020,000 |
| | | DADS | 522,340,000 | 113,172,087 |
| | | HUNTER | | 30,000,000 |
| | Kyela | DADS | 17,023,000 | |
| | | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | | 9,885,000 |
| | | TASAF | 117,602,176 | 26,099,360 |
| | | LGCDG | | 209,536,800 |
| | | TOL | | 50,424,000 |
| | Mbarali | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 806,500 | 1,992,500 |
| | | DADS | 3,500,000 | |
| | | TASAF | 21,000,000 | 63,845,800 |
| | | TANAPA | | 43,399,998 |
| | Ileje | TASAF | 17,210,048 | |
| | | DADS | 22,694,500 | |
| | | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | | 1,455,000 |
| | | LGCDG | | 11,706,000 |
| | Mbeya | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 8,338,150 | 16,000,000 |
| | | DADS | 41,319,127 | |
| | | LGCDG | | 24,500,000 |
| | Chunya | UNDP | 9,875,000 | 0 |
| | | TASAF | 75,649,000 | 156,762,370 |
| | | HUNTER | 53,000,000 | |
| | | DADS | 212,001,803 | |
| | | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 2,250,000 | |
| | Mbozi | DADS/ Halmashauri (Matumizi ya | 93,320,000 | 596,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kawaida) | | |
| | | TASAF | 131,302,000 | 0 |
| | | **Jumla** | **1,935,022,784** | **1,357,798,915** |
| **Morogoro** | Kilosa | Benki ya Dunia | 650,660,579 | |
| | | LGCDG | 25,720,000 | |
| | | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 57,503,600 | |
| | | TASAF | 73,268,450 | |
| | Mvomero | | 7,500,000 | |
| | Ulanga | CARITAS | 173,232,592 | |
| | | South Korea Embassy | 5,696,600 | |
| | | LGCDG | 12,000,000 | |
| | Kilombero | CARITAS / AUSTRALIA DEVELOPMEN T | 1,768,400 | 28,000,000 |
| | Morogoro | PLAN MOROGORO | 122,152,293 | 39,208,307 |
| | | LGCDG | 242,821,533 | |
| | | **Jumla** | **1,372,324,047** | **67,208,307** |
| **Mtwara** | Masasi | Abasia Ndanda | | 120,000,000 |
| | | ROSDO - NGO | | 199,000,000 |
| | | Chingulungulu Mission | | 12,000,000 |
| | Mtwara | TASAF | 7,500,000 | 521,754,830 |
| | | Clinton HIV/AIDS | | 190,000,000 |
| | | AMREF/EU | 65,200,000 | 8,999,359,200 |
| | | TWESA WATER Finns | | 13,000,000 |
| | | CHAI | 117,800,000 | |
| | Manispaa ya Mtwara | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 3,414,000 | |
| | Tandahimba | ACTION AID INTERNATION AL | | 7,000,000 |
| | Newala | TASAF | 42,000,000 | 25,000,000 |
| | | **Jumla** | **235,914,000** | **10,087,114,030** |

| **Mkoa** | **Halmashauri** | **Taasisi** | **Gharama (Sh)** |
|---|---|---|---|

| | | | 2007/2008 | 2008/2009 |
|---|---|---|---|---|
| **Mwanza** | Misungwi | TASAF | | 11,500,000 |
| | Wilaya ya Kwimba | TASAF | 398,000 | |
| | | **Jumla** | **398,000** | **11,500,000** |
| **Rukwa** | Manispaa ya Sumbawanga | TASAF | 56,850,140 | 211,000,000 |
| | | Sumbawanga (Matumizi ya kawaida) | | 15,000,000 |
| | | **Jumla** | **56,850,140** | **226,000,000** |
| **Ruvuma** | Namtumbo | TASAF | 10,806,000 | |
| | Manispaa ya Songea | TASAF | 73,260,674 | |
| | | **Jumla** | **84,066,674** | |
| **Shinyanga** | Bariadi | KOICA | 804,144,449 | |
| | Bukombe | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | | 13,793,320 |
| | | **Jumla** | **804,144,449** | **13,793,320** |
| **Singida** | Manyoni | Benki ya Dunia | 1,424,453,253 | |
| | | TASAF | 160,609,440 | |
| | Iramba | Benki ya Dunia | 2,801,751,320 | |
| | | TASAF | | 384,703,585 |
| | | WaterAid | | 183,988,670 |
| | Singida | Benki ya Dunia | 1,435,663,160 | |
| | | LGCDG | | 45,000,000 |
| | | **Jumla** | **5,822,477,173** | **613,692,255** |
| **Tabora** | Igunga | Benki ya Dunia | 2,664,828,120 | 2,765,757,158 |
| | | Halmashauri (Matumizi ya kawaida) | 72,220,000 | |
| | Sikonge | TASAF | 36,000,000 | 24,000,000 |
| | Manispaa ya Tabora | TASAF | 100,033,875 | 104,663,226 |
| | Nzega | TASAF | 0 | 63,852,950 |
| | | LGCDG | 0 | 44,190,000 |
| | | **Jumla** | **2,873,081,995** | **3,002,463,334** |
| **Tanga** | Pangani | TASAF | 10,700,000 | |
| | Kilindi | TASAF | 32,000,000 | |
| | Lushoto | CARITAS | 135,600,000 | |
| | Jiji la Tanga | TASAF | 151,704,816 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Jumla** | **330,004,816** | |
| **Jumla Kuu** | | | **44,282,740,524** | **79,127,894,650** |
| **Jumla Kuu kwa mwaka 2007/2008 na 2008/2009 (Machi 2009)** | | | **123,410,635,174** | |

**Maelezo:**

| | |
|---|---|
| ACRA | Association Cooperation Rural Africa |
| AMREF | African Medical Research Foundation |
| CARITAS | *Charity-expression of love* (Shirika la Kikristu la Kusaidia Wenye Shida) |
| CMSR | Central Mondialita Sivillioppo Reciproco |
| DADS | District Agricultural Development Support |
| EU | European Union |
| FACT | Food Aid Counterpart |
| IDA | International Development Agency |
| IFAD | International Fund for Agricultural Development |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| KOICA | Korea International Cooperation Agency |
| SHIPO | Southern Highlands Participatory Organization |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| UNDP | United Nations Development Programme |
| UNHCR | United Nations High Commission for Refugees |
| WIPHS | World Islamic Propagator & Humanitarian Services |
| ARCK | African Relief Committee of Kuwait |
| WAMA | Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya |
| LGCDG | Local Government Capital Development Grand |
| LVIA | Lay Volunteers International Association (Associazione di Cooperzione e Volontariato Internazionale) |
| CHAI | Clinton HIV Aids Initiative |

**Jedwali Na.3**

**Hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kupata wataalam washauri kwa ajili ya Halmashauri hadi tarehe 17 Juni 2009**

**(a) Kundi la Halmashauri 99**

Kundi hili ni la Halmashauri zilizowahi kupata mapendekezo ya Wataalam Washauri

**1. Halmashauri 38 ambazo zimekwishapata ridha ya kusaini mikataba kati yake na wataalam washauri**

| | Mkoa/ Halmashauri | Jina la Kampuni | Tarehe ya Kusaini Mkataba |
|---|---|---|---|
| | | **Arusha** | |
| 1 | Manispaa ya Arusha | | |
| 2 | Karatu | | |
| 3 | Longido | M/S Howard Humphreys (T) Ltd in association with Howard Humphreys (EA) Ltd | 28.5.2009 |
| 4 | Monduli | M/S Howard Humphreys (T) Ltd in association with Howard Humphreys (EA) Ltd | 21.5.2009 |
| | | **Dodoma** | |
| 1 | Kongwa | M/S O & A Company Ltd in association with Grontmij/Carl Bro and ODATE FSP | 28.5.2009 |
| 2 | Mpwapwa | | |
| | | **Iringa** | |
| 1 | Kilolo | | |
| 2 | Njombe Mji | | |
| | | **Kagera** | |
| 1 | Manispaa ya Bukoba | M/S O & A Company Ltd in association with Grontmij/Carl Bro and ODATE FSP | 25.5.2009 |
| 2 | Chato | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 26.5.2009 |
| 3 | Misenyi | | |
| | | **Kilimanjaro** | |
| 1 | Hai | M/S CES Consulting Engineers Salzgitter GmbH in association with MEL Consult Ltd | 11.5.2009 |
| 2 | Moshi Vijijini | M/S O & A Company Ltd in association with Grontmij/Carl Bro and ODATE FSP | 13.5.2009 |
| 3 | Mwanga | | |
| | | **Lindi** | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa | M/S Don Consult Ltd in association with Relief to Development Society (REDESO) | 19.5.2009 |
| 2 | Lindi Vijijini | M/S Don Consult Ltd in association with Relief to Development Society (REDESO) | 11.5.2009 |
| 3 | Liwale | M/S Don Consult Ltd in association with Relief to Development Society (REDESO) | 21.5.2009 |
| | | **Manyara** | |
| 1 | Babati Vijijini | M/S Free World Company Ltd in association with People Voice in Development (PEVODE) | 13.5.2009 |
| 2 | Hanang’ | | |
| 3 | Mbulu | | |
| | | **Mara** | |
| 1 | Bunda | M/S Network for Water and Sanitation Tanzania Ltd (NETWAS) | 25.5.2009 |
| 2 | Serengeti | M/S Network for Water and Sanitation Tanzania Ltd (NETWAS) | 29.4.2009 |
| | | **Mbeya** | |
| | Mbeya Vijijini | M/S Network for Water and Sanitation Tanzania Ltd (NETWAS) | 22.4.2009 |
| | | **Morogoro** | |
| | Ulanga | | |
| | | **Mtwara** | |
| 1 | Mtwara Vijijini | M/S Don Consult Ltd in association with Relief to Development Society (REDESO) | 1.6.2009 |
| 2 | Nanyumbu | M/S Don Consult Ltd in association with Relief to Development Society (REDESO) | 20.5.2009 |
| | | **Mwanza** | |
| 1 | Geita | | |
| 2 | Magu | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult | 22.5.2009 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Limited | |
| 3 | Sengerema | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 25.5.2009 |
| | | **Pwani** | |
| | Rufiji | M/S Network for Water and Sanitation Tanzania Ltd (NETWAS) | 29.5.2009 |
| | | **Rukwa** | |
| | Mpanda Vijijini | M/S O & A Company Ltd in association with Grontmij/Carl Bro and ODATE FSP | 8.5.2009 |
| | | **Ruvuma** | |
| 1 | Namtumbo | | |
| 2 | Songea Vijijini | | |
| | | **Singida** | |
| | Singida Vijijini | M/S Network for Water and Sanitation Tanzania Ltd (NETWAS) | 20.5.2009 |
| | | **Tanga** | |
| 1 | Korogwe Mji | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 20.5.2009 |
| 2 | Lushoto | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 25.5.2009 |
| 3 | Muheza | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 19.5.2009 |
| 4 | Jiji la Tanga | COWI Tanzania Consulting Engineers and Planners Limited in association with ENV Consult Limited | 19.5.2009 |

**2. Halmashauri 54 ambazo rasimu za mikataba kati ya Halmashauri na wataalam washauri ziko Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kusaini mikataba:**

| Mkoa | Halmashauri |
| --- | --- |
| **Arusha** | Arusha Vijijini, Ngorongoro |
| **Dar es Salaam** | Kinondoni |
| **Dodoma** | Bahi, Chamwino, Manispaa ya Dodoma, Kondoa |
| **Iringa** | Manispaa ya Iringa, Iringa Vijijini, Ludewa, Makete, Mufindi, Njombe Vijijini |
| **Kagera** | Biharamulo, Bukoba Vijijini, Karagwe, Muleba, Ngara |
| **Kigoma** | Kasulu, Kibondo, Kigoma/Ujiji, Kigoma Vijijini |
| **Kilimanjaro** | Rombo, Same, Siha |
| **Lindi** | Lindi Mji, Nachingwea, Ruangwa |
| **Manyara** | Babati Mji |
| **Mara** | Manispaa ya Musoma, Musoma Vijijini, Tarime |
| **Morogoro** | Manispaa ya Morogoro, Morogoro Vijijini, Kilombero, Kilosa |
| **Mtwara** | Masasi, Manispaa ya Mtwara, Newala, Tandahimba |
| **Mwanza** | Mwanza Jiji |
| **Pwani** | Mji wa Kibaha, Kibaha Vijijini, Kisarawe, Mafia, Mkuranga |
| **Rukwa** | Mji wa Mpanda, Nkasi, Manispaa ya Sumbawanga, Sumbawanga Vijijini |
| **Ruvuma** | Mbinga |
| **Singida** | Iramba, Manyoni, Manispaa ya Singida |

**3. Halmashauri 2 ambazo rasimu za mikataba kati ya Halmashauri na wataalam washauri ziko Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kufanyiwa mapitio kabla ya kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kusaini mikataba:**

1. Moshi Manispaa
2. Temeke

**4. Halmashauri 5 ambazo rasimu za mikataba kati ya Halmashauri na wataalam washauri bado zinafanyiwa marekebisho na Halmashauri:**

1. Ilala
2. Bagamoyo
3. Meru
4. Bariadi
5. Mvomero

**(b) Kundi la Halmashauri 33**

Kundi hili ni la Halmashauri zilizorudia kutangaza kupata Wataalam Washauri.

**1. Halmashauri 32 ambazo kati ya tarehe 15.5.2009 na 3.6.2009 zilipata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kufungua mapendekekezo ya kifedha na kuandaa rasimu za mikataba kati yake na wataalam washauri:**

| Mkoa | Halmashauri |
|---|---|
| **Manyara** | Kiteto |
| **Mara** | Rorya |
| **Mbeya** | Mbarali, Kyela, Jiji la Mbeya, Ileje, Rungwe, Mbozi, Chunya |
| **Mwanza** | Kwimba, Misungwi, Ukerewe |
| **Ruvuma** | Tunduru, Manispaa ya Songea |
| **Shinyanga** | Shinyanga Vijijini, Manispaa ya Shinyanga, Maswa, Kahama, Meatu, Kishapu, Bukombe |
| **Tabora** | Igunga, Nzega, Manispaa ya Tabora, Sikonge, Urambo, Uyui |
| **Tanga** | Handeni, Kilindi, Korogwe Vijijini, Mkinga, Pangani |

**2. Halmashauri 1 ya Simanjiro taarifa yake ya mapendekezo ya kiufundi ya wataalam washauri iko Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya kufungua mapendekekezo ya kifedha**

**Jedwali Na.4**

**Ujenzi wa Mabwawa**

| Na. | Jina la Bwawa | Wilaya Husika | Mwaka wa kuanza ujenzi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mugumu | Serengeti | Kabla ya 2007/2008 | Ujenzi umekamilika |
| 2. | Nyambele | Bunda | 2007/2008 | Ujenzi unaendelea |
| 3. | Nyashitanda | Misungwi | 2007/2008 | Ujenzi unaendelea |
| 4 | Seke Ididi | Kishapu | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 5. | Mti Mmoja | Monduli | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 6. | Ingodin | Longido | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 7. | Nyambori | Rorya | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 8. | Masuguru | Bagamoyo | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 9. | Mwanjoro | Meatu | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 10. | Kawa | Nkasi | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 11. | Sasajila | Chamwino | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 12. | Wegero | Musoma Vijijini | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 13. | Habiya | Bariadi | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | Iguluba | Iringa Vijijini | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 15. | Matwiga | Chunya | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 16. | Loonderkes | Simanjiro | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 17. | Mariwanda | Bunda | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |
| 18 | Bulenya | Igunga | 2008/2009 | Ujenzi unaendelea |